ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Nane – Tarehe 21 Juni, 2010

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Thuwaibah Eddington Kissasi) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kny (Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto naomba kuwasilisha Mezani taarifa ya utekelezaji wa haki za watoto Zanzibar mwaka 2010. Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 102

Maharamia wa Kisomali Kuishambulia Meli ya Namtuma:

Mhe. Fatma Abdalla Tamim – Aliuliza:-

Inadaiwa kuwa Maharamia tisa wa Kisomali waliotaka kuiteka Meli ya Namtuma katika eneo lililo baina ya Kisiwa cha Unguja na Pemba wamekimbilia Pemba.

(a) Je, Mhe. Waziri swali hili ni kweli.

(b) Kama ni kweli maharamia hao walikamatwa au walifanikiwa kutoroka.

(c) Kama walitoroka serikali ilichukua juhudi gani ya kuwasaka.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 102 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli zipo taarifa zilizopokelewa na vikosi vya Ulinzi na Usalama kuwa Maharamia wa Kisomali

walitaka kuteka Meli ya Namtuma katika eneo la bahari kuu na baadaye kukimbilia katika Kisiwa cha Pemba;

(b) Maharamia hao bado mpaka leo hawajakamatwa; na

(c) Serikali kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Polisi, KMKM na JWTZ vinaendelea kufanya doria katika Mwambao wa bahari ya Visiwa vya Unguja na Pemba. Aidha Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na uongozi wa Mikoa unaendelea kutafuta taarifa mbali mbali kwa Masheha na watu wa karibu na fukwe kujua kuwepo kwa wageni wowote au Maharamia hao.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, huu utaratibu au mpango wa vitendo hivyo vya uharamia vinakuwa kila siku kwanza ulianzia katika mwambao wetu wa Visiwa vya Unguja na Bara. Hivi karibuni wananchi wangu wa Kisiwa cha Uzi walikuwa wanafanya biashara walivamiwa i na watu wasiojulikana, mbali na Wasomali hao lakini pia na wananchi wenyewe baina ya Bara na Zanzibar kuna balaa hili la uharamia. Kwa sababu kitendo hiki sasa kimeshakuwa mpaka kwenye bahari kuu.

(a) Je, hawa vikosi vyetu vya (SMZ) wanavyo vyombo madhubuti vya kuweza kupambana nao?

(b) Je, pia kwa vikosi vinavyohudumiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama polisi marine ni kweli wamewekwa baharini lakini hawana boti wala nini, Hili nalo Mhe. Waziri analisemeaje ili na polisi nao wakeweza kupewa boti wakasaidia jambo hili, anatwambiaje Mhe. Waziri?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mkema amezungumza kwamba huu uharamia ukiacha wa Wasomali lakini ndani ya Bandari yetu ya Tanzania inaonesha kuna vitendo vya kiharamia. Kwa kuwa yeye anao mfano wa wavuvi wake au wafanyabiashara wake ambao wanasafiri pengine kwa vyombo vidogo vidogo kutoka Zanzibar kuelekea Bara anavyosema waliwahi kupata matatizo ya kuvamiwa.

Kwanza kitu ambacho ninachokiomba kwa wavuvi wetu na wale wote ambao wanatumia bahari ni vizuri wanaposafiri wawe wanatembea na simu za mkononi. Sasa hivi ulimwengu umekuwa kijiji kidogo. Ulimwengu wote

unauweka kiganjani, hasa ukiwa unatumia simu ya mkononi ili vitendo vyovyote vinavyotokezea kinyume cha sheria kati kati ya bahari au ndani ya bahari basi uweze kupiga simu nchi kavu waweze kupata msaada na huduma ya haraka.

Pili vyombo vyetu au vikosi vyetu vya KMKM je, vinavyo vyombo madhubutii vya kuweza kulinda doria bahari yetu.

Mhe. Mwenyekiti, KMKM sasa hivi wanazo boti nzuri za kisasa lakini vile vile wanazo ngwanda za kuweza kufukuza kwa haraka. Kuna baadhi ya mambo mengi ambayo yanatokezea katika Visiwa vyetu ambavyo sisi kama raia tunakuwa hatuvijui lakini wao kwa kuwa ndio kazi yao ya kila siku wanahakikisha ulinzi na usalama katika visiwa vyetu. Ingawa vyombo walivyokuwa navyo bado havijatosha lakini kwa kuweza kulinda visiwa vyetu vyombo hivyo KMKM wanavyo.

Lakini pia amezungumzia suala la Polisi Marine kuwa na boti.

Mhe. Mwenyekiti, hili tutaendelea kulifanyia na nataka niwahakikishie Watanzania na Wazanzibari wote kwamba visiwa vyetu vipo salama. Jeshi la wananchih wa Tanzania linaboti za kuweza kufukuza, zinaboti za kufanya doria na hata ile meli iliyokamatwa ya uvuvi ilikuwa ni kushirikiano wa Kikanda. Kwa sababu katika ulinzi sasa hivi kuna ulinzi kama Zanzibar, tuna ulinzi kama Tanzania lakini vile vile tuna ulinzi wa kikanda ambao tunashirikiana na wenzetu kutoka Afrika ya Kusini na hizi nchi za karibuni.

Kwa hiyo bado naendelea kusema kwamba Zanzibar sisi tuna bahati moja kwanza tuna vikosi vyetu vya ndani ambavyo vinatulina halafu, tuna vikosi vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinatulinda navyo vile vile. Lakini tuna vikosi vya Kikanda ambavyo vinashiriki na vikosi vyetu kwa kuweza kufanya doria katika kuwasilisha usalama wa Tanzania na Zanzibar kwa jumla.

Mhe: Hija Hassan Hija: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Hivi karibuni baadhi ya vyombo vya habari viliripoti kukamatwa kwa wageni eneo la Tumbatu wanadhaniwa kwamba ni Wasomali. Je wageni hao walikuwa ni wakimbizi au ni maharamia?

(b) Hatuo hiyo ya kukamatwa kwa wageni hadi kuendeshwa kwa kesi yao ilimalizika ndani ya wiki moja. Kwa nini serikali ilikuwa rahisi kuwaachia wageni hao ndani ya wiki moja?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni kuna raia ambao wanasadikia ni Wasomali na baadhi yao na Waithiopia walikamatwa katika Kisiwa cha Tumbatu. Kimsingi sitaki kusema kwamba walikamatwa isipokuwa naweza kusema waliokotwa kwa sababu wale raia waliingia nchini na siko kwamba waliingia wao wenyewe kihalali isipokuwa walipata matatizo baharini na taarifa hizo serikalini zilipatikana na kuna baadhi ya miili ya wenzao ilipatikana ikielea. Kwa hivyo kuna chombo ambacho wenyewe walivyokuwa wakisema walikuwa wanaelekea Msumbiji na Afrika ya Kusini kilizama baharini.

Serikali kwa kuangalia na ubinaadamu kwa sababu mtu unapomkamata kuna mambo mawili, umemkamata kama ingelikuwa wameteremka katika chombo pale serikali ingelikuwa imechukua hatua ndefu za kuhakikisha kutafuta ile sababu waliyoingia nchini kinyume cha sheria. Lakini wale walikuwa ni raia ambao wanapita, wamepata mtihani. Kwa hivyo sisi kwa upande wetu kama serika tulijaribu kuangalie kile chanzo cha lile tukio mpaka wao wakaweza kuingia Zanzibar.

Ndio maana kwamba baada ya kuonekana kwamba wale hawana hatia ni raia ambao hawakukusudia kuja Tanzania walikuwa wanapita ndio maana serikali ikaweza kuharakisha lile suala lao. Kwa sababu mtu anapopata matatizo basi si vizuri na wewe ukamzidishia matatizo. Kwa shivyo serikali tukatumia busara ndio maana lile suala lao tukalimaliza kwa haraka. Lakini kama ingelikuwa wameingia kinyume cha sheria basi mpaka leo wangelikuwa wanaendelea kusota lupango.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mhe. Waziri inasemekana kuwa maharamia hao waliwahi kutupa mizinga katika kambi ya KMKM Msuka Pemba. Je, Mhe. Waziri hili ni kweli.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, sijapata hiyo taarifa kwamba maharamia hawa walitupa mizinga huko Msuka Pemba. Lakini kimsingi maharamia hao walipokuwa wakifukuzwa huko katika bahari Kuu walikimbilia katika maeneo ya Kisiwa cha Pemba. Kimsingi sisi hatukuwaona na kwa sababu ukiangalia ki- *geography* Kisiwa cha Pemba unapotoka katika ukanda wa bahari kuu unapoingia kisiwa cha Pemba basi ukikwepa kidogo basi tayari umeshaingia mwambao wa Mombasa na Somali.

Kwa hiyo inawezekana maharamia wale walitishia kama wanakuja katika visiwa vya Pemba na kwa kuwa wale waliokuwa wakiwafukuza nadhani ni meli za IYU zilipokuwa zikiwafukuza pamoja na erkopta walipoona wanaingia katika anga ya Tanzania wakaona kwa mujibu wa sheria kwa kuwa hawakupata

ruhusa wakawaachia, inaonesha na wao baada ya kuona kwamba wale waliokuwa wamewafukuza wamewaachia wakaamua ku- *cross* kurejea kwao. Kwa hivyo bado tunaendelea kuthibitisha kwamba maharamia hawa hawakukimbilia Pemba.

Nam. 35

Uhamasishaji Taasisi za Kiraia Katika Utunzaji Mazingira

Mhe. Amina Iddi Mbrouk Kny/(Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi) - Aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kukabiliana na uharibifu wa mazingira sio la serikali pekee, na kwa kuwa moja ya sababu kuu inayosababisha kuongezeka kwa hali ya joto duniani ni ukataji wa miti ovyo na kwa wingi.

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako imehamasisha kiasi gani taasisi za Kiraia *(Civil Societies)* kuhusu umuhimu wao katika kusaidia kukabiliana na tatizo hilo?

(b) Iwapo zipo taasisi ambazo tayari zimeshaandaa, kimaandishi *(write-up)* juu ya mpango wao wanaotegemea kuutumia katika kusaidia kukabiliana na tatizo hilo, Wizara yako itakuwa tayari kusaidia katika kuwapatia wafadhili.

(c) Unawashauri nini wana taasisi hao ili waweze kufanikisha malengo yao mazuri waliyoyaandaa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 35 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kupitia Idara ya Mazingira imeshiriki kwa kiasi kikubwa kuzishajisha Taasisi za Kiraia *(Civil Societies)* juu ya kuielimisha jamii katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani. Njia zilizotumika katika kuzishajiisha ni pamoja na kutumia vyombo vya habari, makongamano, semina na warsha, midahalo pamoja na kuiomba Jumuiya Mama ya ANGOZA kuzipa miongozo jumuiya inazozisimamia juu ya ushiriki wao katika kuielimisha jamii kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani.

(b) Miongoni mwa kazi zinazofanywa na wizara yangu kwa taasisi za kiraia zilizoshajiishika na kuandaa miradi ni kuwatafutia wafadhili wa miradi hiyo. Kuna taasisi nyingi Unguja na Pemba zimeshapata ufadhili kupitia utaratibu huu. Miongoni mwao ni Jumuiya ya CODECOZ, JUMAKA, MECA, JEMA, VECA, WECOC, KIDIKE na taasisi nyingi nyenginezo. Aidha, Wizara yangu inaendelea na juhudi za kuitafutia wafadhali miradi mengine kupitia Mradi wa MACEMP na ReCoMaP.

(c) Ushauri wangu kwao ni kuongeza kiwango cha taaluma kwa wana-taasisi hao, kuongeza ushirikiano miongoni mwao na wasichoke katika kutafuta wafadhili wa ndani na nje ili kuendeleza majukumu waliyojipangia.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa na uchimbaji mchanga ovyo ni moja ya uharibifu wa mazingira. Je, Mhe. Waziri analishuhulikiaje suala hili?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Thuwaibah kwa tika suala lako ulisema kwamba unakubaliana na uharibifu wa hali ya hewa na uchimbaji mchanga au mazingira kwa jumla si suala la taasisi au Idara ya Mazingira au Wizara yatu bali ni suala la kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu imechukua juhudi pamoja na kuanza kushajihisha kuunda vikundi ambavyo kwa kweli ni vingi tu kwa Unguja na Pemba vinavyoshuhulikia mazingira ikiwa pamoja na suala la tatizo la uchimbaji wa michanga na ukataji wa miti ovyo Unguja na Pemba. Tunaendelea kuwaelimisha jimii kupitia vikundi hivyo na sisi wenyewe kama ni Idara au Wizara kupitia vyombo vyetu vya habari kuelimisha jamii katika suala zima la hatari ya uharibifu wa mazingira ikiwa pamoja na uchimbaji mchanga.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Menyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika maeneo ambayo yanaonekana kwamba hakuna mazingira mazura ni ukanda wa pwani kuanzia fukwe mpaka kilimita 2 inakuwa hakuna miti ambayo inaweza ikasaidia kuvuma kwa upepo mkuwa na kupunguza nguvu ya hali ili mvua nayo inyeshe, ikiwemo Pwani Mchangani, Matemwe.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kushajihisha wananchi kupanda miti ambayo itaweza kupunguza kasi ya upepo na kusababisha mazingira yanawiri vizuri hasa kwa kuwa ukanda huu mikoko haiyoti?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kazi hii ni ya jamii yaani kitaifa. Nimesema kwamba suala la ukataji miti, suala la uchimbaji mchanga ni masuala yetu sote kila mmoja linamuwajibikia.

Kwa hivyo kwa mara nyengine tena tunatoa wito kupitia Baraza lako tukufu kwamba sote kwa pamoja kila mwananchi ha hasa uongozi wa tawala za Mikoa, vijijini huko waweze kusaidia serikali kuu kupambana na wale wote ambao wanakata miti ovyo bila ya kibali ili tunusuru hali hiyo aliyoisema Mheshimiwa Ame Mati.

Vile vile na sisi kama ni viongozi Wawakilishi tuna jukumu kuwa sana la kuweza kuisaidia hifadhi hii ya mazingira katika sehemu zetu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo ambalo linakatwa miti kwa wingi ni Jimbo langu la Mtambwe. Hili suala nimepiga vita kweli kweli, mpaka hivi karibuni kiasi mwezi mmoja kupita pale Bahanasa nilimkuta Afisa kazi yake ni kuhisabu gari zinazopita na mizigo ya miti na vigogo na kutoa kibali. Katika kugombana naye alisema kuwa usinionee bure ni Wizara yenyewe ndio inayotoa ruhusa hii kuwa kila mtu aende akakate miti katika jimbo lile.

Ikiwa wizara ndiyo inayofanya hivyo sijui Mhe. Waziri suala hilo analijua na kama halijui atalifuatilia na kutoa maelekezo gani.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, suala hilo mimi silijui. Lakini imekuwa vizuri sana na namuomba Mheshimiwa.. Mwakilishi afanye kama anavyoweza kunipatia ripoti kamili ya mtu huyo ili tuweze kumjua huyo mtu katika wizara au taasisi ya Wizara yangu anayetoa kibali cha kuwa miti ikatwe ovyo na tutazichukua hatua za kinidhamu mara moja.

Nam. 55

Barabara Zisizofikia Viwango

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Baadhi ya Barabara zetu zilizojengwa na Wakandarasi kama vile Barabara ya Chake - Mkoani, haziko katika hali nzuri kwa sababu zilijengwa kwa kiwango duni.

(a) Mhe. Waziri, kama Kampuni haikujenga barabara kwa kiwango kinachohitajika. Hatua gani zinachukuliwa kwa Kampuni hiyo; na

(b) Mpaka sasa kuna Kampuni ngapi zilizowahi kuchukuliwa hatua kutokana na tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi, mara nyingi tumekuwa tukieleza kwamba barabara ya Mkoani-Chake Chake haikujengwa chini ya Kiwango. Kwani makubaliano hasa ya ujenzi wa barabara hiyo yalikuwa ni kuijenga barabara hiyo kutoka Mkoani hadi Mtuhaliwa, hivyo barabara ya Mtuhaliwa hadi Chake Chake haikujengwa upya bali ilifanyiwa *overlay* tu.

Aidha hadi sasa hakuna Kampuni hata moja iliyochukuliwa hatua kama hiyo kwa upande wa ujenzi wa barabara isipokuwa Kampuni ya Cogefar ilipelekwa Mahkama kutokana na kujenga Gati chini ya kiwango.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Naibu Waziri wa Mawasiliano kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa barabara hasa anayefadhiliwa au unapata msaada kutoka nje huwa una mkandarasi na mshauri ujenzi na msimamizi ujenzi. Katika barabara ambazo zimejengea vibaya sana na mbobu sana ni barabara hii inayotoka Kidimni kwa kupitia Gana katika Wilaya ya Kaskazini “B”.

Mhe. Naibu Waziri Ujenzi ule ulifadhiliwa je, hakukuwa na mshauri wa ujenzi na kama alikuwepo barabara ile hadi sasa inavyoonekana muda wake haujafika

na barabara yote imechimbika. Je, kuna hatua gani ambayo Wizara hii imechukua kwa uharibifu huu ambao nimeuzungumzia.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza barabara hii kutoka Kidimni hadi Kitope haikujengwa chini ya kiwango kama alivyosema Mhe. Mwakilishi lakini barabara hii inatokana na ardhi ya eneo lenyewe sio nzuri. Na ukizingatia maeneo haya hata barabara ambayo imejengwa kwa kiwango kizuri vile vile kwa mfano barabara ya Kiwengwa hadi Kinyasini, barabara ile ukiitizama yote ni nzima lakini eneo la Upenja eneo lile lote barabara imeharibika kutokana na ardhi yake kuwa sio zuri. Kwa hiyo si sababu kubwa zaidi kwamba imejengwa chini ya kiwango lakini na ardhi ambayo imetumika nayo vile vile haikubwa nzuri. Suala la kuwa na mshauri nakubaliana na wewe kwamba maelezo yake ni sahihi na yote ambayo anayasema kwamba washauri tulikuwa nao na walishauri vizuri lakini kilichojitokeza ni hicho nilichokizungumza.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Mwenyekiti nashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi hii nikauliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Kidimni hadi Kitope ilijengwa na Kampuni ya SSMehta lakini katika eneo la Kiboje *culvert* zilizowekwa ni ndogo sana hivyo hupelekea mafuriko katika eneo moja. Je, kuweka *culvert* ndogo ni kosa la kampuni ama michoro ya ujenzi.

Lakini kwa kuwa wananchi kila ikija mvua wanapata mafuriko je, wizara itawasaidia vipi ili kuondokana na yale mafuriko kwa sababu *culvert* zilizotiwa ni ndogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi ametushauri au kutuelekeza kwamba kuna tatizo la *culvert* kuwa ndogo katika eneo hilo. Kwa hivyo, naomba tushirikiane mimi na yeye pamoja na wataalamu wangu tutakwenda kuona eneo hilo na tutafanya masahihisho kuona kwamba kero hiyo inaondoka.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake mama alikiri kwamba barabara ya Chake Chake-Mkoani haikujengwa kwa kiwango kilichokubalika. Pia amekiri kwamba hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kwa mkandarasi yule.

Je, haoni SMZ kulinyamazia kimya suala hili ni kupoteza pesa za walipa kodi.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nirekebisho kidogo maelekezo yake anasema kwamba tumejibu

kuwa haikujengwa kwenye kiwango kilichokubalika. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mimi sikujibu hivyo tulichosema ni kwamba barabara kutoka Mkoani hadi Mtuhaliwa ndio ambapo tulikuwa na *contract* pale eneo lililobakia kutoka Mtuhalia mpaka Chake Chake ni eneo ambalo tulilifanyia *over license* wenyewe. Kwa hivyo, suala lake Mhe. Mwakilishi nafikiri halikuwa sahihi kama pengine alivyoliuliza.

Nam. 61

Uvamizi wa Eneo la Chuo cha Afya Mbweni

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Chuo cha Sayansi ya Afya Mbweni kimepata Mfadhili (*ADB*) kwa ajili ya kuongeza majengo ya Chuo hicho, lakini eneo kubwa la Chuo hicho limevamiwa kwa makaazi ya watu na kwamba eneo lililobakia ni finyu na halina uzio. Je ni lini wavamizi wataondoshwa katika eneo la Chuo na lini eneo hilo litajengwa uzio ili kulihifadhi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, awamu ya pili ya Mradi wa *ADB* kwa upande wa Chuo cha Afya ulilenga mambo yafuatayo:-

- Ujenzi wa majengo 6 yakiwemo mawili ya taaluma yaani madarasa, maabara na ofisi za walimu;

- Majengo mawili ni nyumba za walimu ambapo kila jengo moja linakaliwa na koo nne; na

- Na majengo mawili ni dakhalia za wanafunzi pamoja na nyumba za mlezi kila dakhalia moja inakaliwa na wanafunzi 56.

Majengo hayo yamejengwa kwenye eneo la chuo na kufunguliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Amani A. Karume mnamo tarehe 23 Machi, 2010.

Mhe. Mwenyekiti, katika ujenzi huu wa *ADB* suala la ujenzi wa uzio halikuwemo tangu asili. Hata hivyo, hivi sasa wizara yangu imeanza

kushughulikia suala hili la uzio kwa kutia maombi ya suala hilo katika makisio ya mwaka huu wa fedha 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la uvamizi wa eneo la Chuo cha Afya ni kuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inatambua kuwa ardhi ni mali ya Serikali na ipo wizara maalum iliyowekwa kusimamia umiliki, ugawaji na matumizi ya ardhi hapa nchini. Ni matumaini yangu kuwa wizara inayohusika itaendelea na utekelezaji wa kazi zake ikiwemo kusimamia vyema majukumu hayo ya umiliki, ugawaji na matumizi mazuri ya ardhi hapa nchini.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri anasema kwamba wizara yake inaelewa kwamba ardhi ni mali ya serikali, lakini unaweza ukawa na ardhi lakini ukawa huna hatimiliki. Hivyo, eneo la Chuo cha Afya Mbweni je, wanayo hatimiliki. Pia anajua mheshimiwa kwamba maeneo ambayo wanaishi wanafunzi wanawake kuna wahalifu wanavamia na kuwaibia vifaa vyao, na wakiliachia hilo kuna siku itakuwa ni kilio kwa Wazanzibari.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, hatimiliki tunayo ya chuo chetu kile na ni ya uhakika kabisa. Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya kuwa kuna wahalifu katika eneo hilo la chuo ni kwamba hatujaipata, lakini kama hilo suala lipo basi tutalishughulikia na tutajitahidi kadri tunavyoweza kuliweka sawa suala hili ili uhalifu usiweze kuendelea.

Mhe. Omar Ali Jadi: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri amekubali kama eneo la Chuo cha Afya Mbweni lina hatimiliki.

Je, ni sababu gani wakati wana hatimiliki na hatimiliki ina mipaka inaonesha wananchi wakavamiwa na halafu suala akalipeleka kwa Waziri wa Ardhi ndiye anayehusika na masuala hayo?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, sisi tunayo hatimiliki, suala la ardhi kama tulivyosema ni suala la serikali, unaweza ukawa na hatimiliki lakini wenyewe wakihisi kwamba eneo hili linataka kutumika kwa shughuli nyengine wanaweza hatimiliki yako ukawa nayo na pia wakasema kwamba eneo hili kidogo tunataka kutumia kwa shughuli zetu. Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la uvamizi pia linahusika na wenyewe watu wa ardhi sisi tumekabidhiwa hati tunayo katika eneo lile. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, masuala ya kuvamia hayako katika mikono yetu.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nataka kusema kwamba haikubaliki hata kidogo jibu lake.

Mhe. Mwenyekiti, hati ya ardhi inampa uwezo mwenye kupokea ile hati na hakuna sababu nyengine ya kupatikana eneo hilo isipokuwa kwa ridhaa ya yule mwenye hati. Hivi Mhe. Naibu Waziri anataka kutwambia kwamba hii Idara ya Ardhi na Upimaji ina uwezo wa kutoa hati mbili kwa kiwanja kimoja na kama inatoa hivyo haioni inafanya kosa kubwa la kugombanisha baina ya taasisi moja na nyengine. Mhe. Mwenyekiti, na kama hivyo ndivyo lini atashauriana na Idara ya Ardhi ili kuona kwamba wanapambanua mipaka baina ya hati ya mwanzo na hiyo hati ya pili ambayo imetolewa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema mimi sijibu maswali ya kuchekesha nasema vile hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ardhi sote tunajua kama ardhi ni mali ya serikali na wakati wowote ardhi unapopewa unapewa na ardhi hiyo hiyo serikali ikitaka kutumia kwa suala jengine hata kama unayo hati wao wanao uwezo wa kukwambia kama hapa tunachukua kwa suala hili kwa hivyo wanakutengenezea hati nyengine. Kwa hivyo, ndio na sisi tunayo hati nyengine tuliyotengenezewa baada ya hilo eneo jengine lote baada ya kuchukuliwa ndio tunayo hati halisi ya sasa hivi na hivi sasa wanafanya jitihada watu wa chuo hicho ili sasa waonekane kama hapa ndio mwisho.

Nam. 94

Ongezeko la Bei ya Umeme kwa *TANESCO*

Mhe. Ali Abdalla Ali (Kny: Ramadhan Nyonje Pandu) – Aliuliza:-

Mnamo tarehe 24 Disemba 2007, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) ilipandisha bei za umeme kwa wateja wa *TANESCO* likiwemo Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*). Bei hiyo kwa upande wa Zanzibar iliongezeka kwa asilimia 168% kutoka shilingi 28 kwa Unit moja ya Kwh hadi kufikia shilingi 75 kwa unit moja, na kwa upande wa wateja kwa Tanzania Bara, umeme ulipandishwa kwa asilimia 21.7% tu.

(a) Je, Mhe. Waziri ni *EWURA* walitumia vigezo gani kuipandishia bei Zanzibar kwa kiwango kikubwa sana kulinganisha na Tanzania Bara?

(b) Kwa kuwa *TANESCO* wanaendelea kuifanyia bili *ZECO* kwa ongezeko la asilimia 168% na kupelekea kudaiwa TZS 29,000,000,000/=, Je, shirika lako liko tayari kulipa deni hilo la kubambikiziwa?

(c) Na kama liko tayari kulipa ni kiasi gani cha fedha kimeshalipwa hadi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 94 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Ewura ni kwamba kiwango walichokipandisha kilikuwa ni sahihi kwa vile *ZECO* kwa muda mrefu ilikuwa inalipia umeme katika kiwango cha chini ikilinganishwa na makundi mengine ya wateja wakubwa. Kwa hivyo, walichokifanya ni kuiongezea *ZECO* bei kulingana na makundi mengine yalio sawa, hata hivyo hoja hio sio sahihi na haikubaliki kwa vile *ZECO* inachukuwa umeme wa 33kV, 11kV kama walivyo makundi mengine. Vigezo hivyo ni kinyume na vigezo vya kiumeme vya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, majadiliano kuhusu suala hili bado hayajafikia maamuzi na katika hali hiyo, wizara yangu haikua tayari kulipa deni hilo, hata hivyo wizara inaendelea kulifuatilia tatizo hili na hatua zitakazofikiwa tutaliarifu Baraza lako Tukufu. Ifahamike pia kwamba hata Afisi ya Mhe. Waziri Mkuu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania ishawaandikia *TANESCO* na Ewura kurekebisha hali hii lakini hadi leo hawajachukua hatua yoyote, kwa upande wa Zanzibar. Afisi ya Mhe. Waziri Kiongozi ilisaidia kupatikana maelekezo ya Serikali zote mbili. Wizara yangu ikishirikiana na *ZECO* itaendelea kulifuatilia suala hili.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Mhe Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, sijui tumepanga tarehe gani au siku gani kulifuatilia hili suala na kulimaliza.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hatukupanga tarehe hasa lakini nitakumbuka kwamba Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi Mhe. Waziri aliiagiza kwenda Tanzania Bara kukutana na Waziri wa Nishati Mhe. Ngeleja kuzungumzia juu ya suala hili pamoja na suala la Mjumbe wa Bodi ambaye yuko kule kwa sasa anashiriki vikao vipi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi nilimpigia kwanza simu Mhe. Ngeleja lakini pia wizara ilimuandikia barua ya ujio wa kamati hii kukutana nae kuzungumzia juu ya suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwa bahati mbaya Mhe. Ngeleja hatukuweza kukutana nae na aliagiza tuonane na Naibu Waziri Mhe. Malima. Kwa uzito wa kamati za kudumu za Baraza na ambazo zina uamuzi wa mwisho, kupitia kwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu walikataa

kuzungumza na Naibu Waziri, na haikuwa kosa kwa sababu walisema kwamba kitendo cha Waziri kutokuhudhuria kwenye kikao kile ni kuidharau kamati hiyo. Kwa hivyo, bado nasema sisi kama serikali kupitia *ZECO* tutaendelea kufuatilia suala hili.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa deni hili linaongezeka kila siku, na kwa kuwa tuna kiwango tunachokiamini kuwa deni letu stahiki.

Je, *ZECO* inalipa kiasi gani hivi sasa kuwalipa *TANESCO* kila mwezi kwa ajili ya umeme tunaotumia au hatulipi kabisa tunasubiri mpaka tatizo litakapotatuliwa. Mhe. Mwenyekiti, kama hatulipi haionekani kama linaweza likakusanyika hata hapo tutakapoamuliwa ikaja ikawa nalo limeshakuwa kubwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, *ZECO* inalipa deni lake la umeme kila mwezi na kumbukumbu ni kwamba *ZECO* wanalipa bilioni 1.2 kila mwezi, sina hakika hii ya Pemba kwa sasa hivi kwa sababu ni ya juzi tu lakini kila mwezi ZECO inalipa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nilifahamishe Baraza lako tukufu kwamba tatizo lipo na kwa sasa hivi *ZECO* kufuatana na bili ya ongezeko la umeme ambayo wanailipa *ZECO* ni kwamba *ZECO* inadaiwa bili iliyopo sasa ni bilioni 29 na hiyo inaongezeka. Lakini sio hilo tu, mbaya zaidi hivi karibuni kama mwezi mmoja uliopita hivi *TANESCO* wameleta ongezeko jengine la asilimia 34 ukiacha ile ya 168 kwa hiyo jumlisha 168, jumlisha na 34 kwa hiyo kutakuwa na ongezeko la asilimia 202 kitu ambacho hakuna mwananchi yoyote wa Zanzibar atakayeweza kulipia gharama hiyo ya umeme. Hii ndugu wajumbe inatuelekeza, inatusisitiza ile haja ya lazima kwamba Zanzibar iwe na *source* yake wenyewe ya umeme, ikiwa ni ya *wind power* au ikiwa ya *solar power.* Nasema hili jambo la lazima.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili la kuwa na umeme mbadala tayari tunaendelea na mazungumzo na wenzetu wa Israil na Shirika la Umeme tayari limeshalipa milioni 15 kwa Idara ya Mazingira kwa ajili ya kufanya *study,* unajua sasa hivi lazima ukifanya jambo hilo ufanye *study* tusije tu tukenda kwenye umeme wa mawimbi ya bahari yakaathiri wavuvi. Kwa hivyo, tunafanya hivyo na pia juzi kishindo cha jana nilikuwa nazungumza na Mr. Leo Alexender kutoka Marekani katika Mradi wa Umeme wa Jua wa kiwango kikubwa kabisa sio huu wa matumizi ya nyumbani.

Mhe. Mwenyekiti, juzi alinithibitishia kwamba tayari ameshaweza kupata fedha na kampuni ambayo itakuja kufanya hiyo *physibility study* kwa ajili ya umeme wa jua.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba wenzetu sasa hivi wanatuelekeza kwamba lazima tuwe na umeme mbadala na kwa kuwa suala hili limekuwa ni sugu na kila kukicha linaongezeka kuwa donda ndugu.

Je, atakubaliana na mimi Naibu Waziri kama suala hili si la kuwekwa kwenye orodha ya kero za muungano ni suala la kushughulikiwa mara moja ili tusije tukapata tena tatizo la kukatiwa umeme tukakaa giza. Ni lini serikali italishughulikia suala hili na kulimaliza haraka.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, jitihada za kulimaliza tatizo hili zimekuwa zikiendelea na ndio maana Afisi ya Waziri Mkuu kule Tanzania Afisi ya Waziri Kiongozi wamekuwa wakishughulikia tatizo hili, na tutaendelea kuona linazungumzwa ili tatizo hili limalizike.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme wakati mwengine hata kama tutapopata maelekezo ya viongozi wa juu basi tunapaswa kuzingatia maelekezo hayo na tuyafanyie kazi, huwa haipendezi hata kidogo upande mmoja wa serikali unapata maelekezo kutoka ngazi ya juu wakapuuza maelekezo hayo, hili ndilo lililoonekana limefanyika kwa wenzetu kule Tanzania Bara.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa lakini kuna sehemu ndogo tu ambayo nikitaka nielimishwe.

Mhe. Mwenyekiti, na huu umeme wa Pemba tulionao umo katika mazingira haya haya ya malipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, *TANESCO* ndio ile ile ikiwa iko Kigoma, ikiwa Mwanza, ikiwa Dar es Salaam ndio hiyo hiyo.

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na pili nimshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunisimamisha na mimi nitoe mchango wangu mdogo na baadae niuunge hoja mkono.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa katika kujadili hotuba hii niseme kwamba namshukuru sana kabisa Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zake kupitia sekta zote katika kuleta maendeleo ya Zanzibar na ustawi wa jamii yetu. Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Rais amefanya kazi nzuri ya kupigiwa mfano, hata mabubu waliokuwa hawasemi wamefanya kuashiria kwamba mambo ni mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine kubwa la kupigiwa mfano alilolifanya Rais wetu kwa Afrika na Ulaya na mataifa yanayopigania demokrasia ya kweli na yenye matokeo ya maana kwa jamii zetu wameona jinsi gani Rais wetu mpendwa Dk. Amani Abeid Karume alivyochukua hatua za usuluhishi wa kisiasa na utawala bora ili nchi yetu iendelee kuishi na kuwa na amani na utulivu ambao utatupelekea kuimarika kwa uchumi wetu. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana kwa jambo hilo, hili sio la upendeleo ni jambo la uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nasema jambo hili sio dogo ni kubwa na tumekuwa tukilitafuta siku nyingi sasa natoa wito kwa Rais anayekuja anawajibu wa kuliona hili kwa umakini wake mkubwa, umahiri wake uonekane kuanzia kwenye kampeni hadi atakapoingia madarakani, ili utulivu wa nchi yetu uzidi kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwambia sitakupotezea muda nasema kwamba lazima nimshukuru Rais wa Zanzibar kwa kuharakisha kutatua tatizo la umeme kisiwani Pemba, sasa hivi Pemba inang'ara sio kwa majumba tu lakini na kwa mataa, shemeji yangu Mhe. Haji Faki Shaali alipozungumza pale alisahau kidogo kulisema hili kwamba sasa hivi Pemba waa waa umeme hauna matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwaambie wanawake sio wa Mkoa wa Kusini lakini Wapemba nzima kwamba tuutumie umeme huu ili tuzalishe ili tuendelee

na tuzidi kuimarika, suala la kusubiri bwana atakuja saa ngapi aniletee kama tutautumia umeme huu vizuri basi nadhani litatuondokea kabisa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba naunga mkono hoja hii iliopo mbele yetu mia kwa mia na nawaambia kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba kwamba tumefarijika sana pamoja na yote barabara zimejengwa na zimeimarishwa lakini na umeme umetutoa kizani, *inshaallah* Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu kesho mbele ya haki nae awe kweupeni. Ahsante nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nikushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka nianze kwa shukurani. Mhe. Mwenyekiti, shukurani zangu naanza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Shukurani hizi ni maalum na za pekee. Kwanza kwa kuweza kuniteuwa kumsaidia kutekeleza majukumu yake, kwa kunipa nafasi ya kuwa waziri katika Afisi ya Waziri Kiongozi. Ingawa nimechukua muda mrefu kumshukuru, lakini nilikuwa naona kwanza niwajibike, nisije nikashukuru halafu nikaboronga. Sasa lakini niliona kwanza nitekeleze majukumu aliayonipa, lakini kabla hajamaliza muda wake basi na mimi niweze kutoa shukurani zangu za dhati kwake.
Vile vile sio shukurani zangu mimi mwenyewe tu binafsi, lakini shukurani pia kwa wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura. Kwa sababu wanaamini kwamba chaguo lao hawakukosea na ndio maana Mhe. Rais akawaongezea nguvu. Kwa hivyo, kwa hili Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri atufikishie salamu zetu kwa Mhe. Rais kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Kwamtipura sio wanamshukuru rais kwa kuniteuwa mimi tu nikawa waziri, lakini hata kabla sijawa waziri Mhe. Rais tayari ameshatupa michango yake mingi ndani ya Jimbo letu la Kwamtipura yeye kama yeye.

Mhe. Mwenyekiti, wewe mwenyewe utakuwa shahidi, lakini ingawa kipindi hicho ulikuwa bado hujaingia humu Barazani katika miaka ya 2002. kwa kweli nilikuwa hapa sikamatiki nilipokuwa naanza kujenga hospitali ya Jimbo la Kwamtipura. Nilikuwa nikizungumza mpaka *microphone* zinakaribia kupasuka. Kwa sababu nilikuwa natetea wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura.

Namshukuru sana Mhe. Rais alisikia kilio chetu, akasema nini wewe tatizo mbona kelele nyingi, huishi kelele. Nikamwambia Mheshimiwa sio kelele ngoma nzito, chuma kikubwa kile. Akanambia basi poa moto, kwa kuwa nia yako ni nzuri basi tutakusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana Mhe. Rais tulimualika katika kuweka jiwe la msingi ujenzi wetu wa hospitali. Kwa bahati nzuri alipokuja pale katika risala yetu tulimueleza, sisi wenyewe kama wananchi wa Jimbo la Kwamtipura tayari tulikwishatumia shilingi milioni 12 bila ya msaada wowote. Akasema kwa kuthamini mchango wa wananchi wa Kwamtipura basi na mimi naongeza nguvu sawa sawa na walizozitoa wao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wananchi wa Kwamtipura tulifarijika sana siku ile na kwa kweli tukaona *Alhamdulillah* tumeanza kupata mwanga. nashukuru kipindi kile Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ alikuwa ndio waziri anayeshughulikia masuala ya fedha, tulishirikiana kwa pamoja hatua kwa hatua tukaweza kupata zile fedha na tunashukuru tukafikia hatua nzuri.

Kwa hivyo, lazima nimpe pongezi kwa hili na kwa sababu hata yeye mwenyewe alikuja kuifungua hospitali ile. Kuanzia siku hiyo mpaka leo wananchi wa Kwamtipura sasa hivi wanamiliki hospitali yao wenyewe mali yao ukiwemo na mchango wa Mhe. Rais. Kwa hivyo, hatuwezi kumsahau kwa mchango wake huo.

Lakini sio hivyo tu, siku ambayo amekuja kuzindua hospitali ile, tulimuomba jengine, unajua ndio kawaida yetu sisi mkubwa akija tena wewe kazi yako kulia tu, tunadeka. Kwa sababu kulia kwenyewe kwa kudeka sio kama tunalia kwamba tunachukia aa, tunadeka maana mkubwa kaja. Tukaomba jengine tukasema hii hospitali haina maji, tatizo letu Kwamtipura maji. Kwa hivyo, tumechimba kisima kwa nguvu zetu sisi wenyewe na kisima kile kipo pale *Trade School*. Tukamwambia lakini tunahitaji nguvu zako, tulitegemea kisima hiki tungekitumia kwa hospitali, lakini kwa bahati nzuri kisima kile kina maji mengi ya kutosha kinaweza kuwasaidia na wananchi kiasi kama 800 ambao wako karibu na ile hospitali.

Mhe. Rais akatuuliza tena tatizo lenu nini? Nikamwambia tunataka *roll* 10 za mipira ya maji. Sasa yeye aliitikia akasema sawa basi tutalifanyia kazi. Sasa kumbe alikuwa hakufahamu vizuri, alisema *roll* 10 za maji tuwapelekee malori mawili ya maji au vipi? Akaja akamuuliza Mhe. Mkuu wa Mkoa kwa bahati mbaya sasa hivi hayupo hapa.

Mhe. Mkuu wa Mkoa akaja akanambia Mhe. Rais kanambia alikukubalieni ombi lenu kwa sababu ni suala ambalo litawasaidia wananchi. Mlitaka malori mawili ya maji au *roll* 10 za mipira ya maji? Nikamwambia zile *roll* ilikuwa ni yale maringi ya mpira wa maji, akasema kama ni hivyo basi wiki ijayo kanambia niende nikachukue. Tunamshukuru sana Mhe. Mkuu wa Mkoa akaenda kwa Mhe. Rais akapewa ma-*roll* 10 ya mipira ya maji na mpaka sasa hivi wananchi wa Kwamtipura tunashukuru tunayatumia maji yake katika kisima kile na ule usambazaji alitumia nguvu zake yeye. Kwa hivyo, katika mambo haya kwa kweli hatuwezi kumsahau hata kidogo.

Lakini vile vile kuna jengine. Tulimualika katika kufungua ujenzi wa kituo cha Chekechea katika Jimbo letu la Kwamtipura ambacho kipo katika Shehia ya Kwamtipura. Siku ile tulipokuwa tumemsomea risala yetu kama tunavyosema mkubwa akija lazima tudeke, tukadeka tena, tukamuomba Mhe. Rais kwamba hii njia yetu tunataka tuboreshewe, tutiliwe kifusi na baadae hali ikiruhusu tutiliwe lami.

Kwa hivyo, katika risala ile wananchi walipoomba basi Mhe. Rais akatoa ahadi kwamba bsi nimesikia sasa nitawaagiza watendaji wangu wamwambie Mkurugenzi wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara basi waje waiangalie njia hii ili tuweze kuifanyia huo ukarabati. Na kipindi kile wananchi walikuwa wanataka wapatiwe daladala. Lakini tulikuwa tunashindwa kwa sababu njia ilikuwa mbovu. Tunashukuru Mhe. Rais alituahidi kwamba njia ile itatengenezwa.

Sasa hapa ndipo kwenye maombi yangu. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum usimzungumzishe Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tuna maombi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ndipo kwenye maombi yangu. Namuomba sana Mhe. Waziri amkumbudhe Mzee, lakini sio amkumbushe Mzee, kwa sababu siku ile Mhe. Rais alifuatana na watendaji wake. Pale palikuwa na Waziri wa Zamu, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini bado ile kumbukumbu mimi ninayo. Kwa hivyo, Mhe. Rais aliagiza wale maafisa aliofuatana nao kwamba waende kwa Mkurugenzi wa Utunzaji na Ujenzi wa Barabara kuja kuiangalia barabara ile inayotoka kwenye Makao Makuu ya *CUF* au Afisi ya Wilaya ya *CUF*, maarufu Daraja Bovu au *Radio* O*ne* mpaka inatokea kwa Abasi Hussein eneo la Shauri Moyo.

Sasa mimi nadhani sasa hivi Idara au Wizara ya Mawasiliano kupitia kitengo chake cha *UUB*, kwa kweli sasa hivi Mhe. Waziri amekijenga kweli kweli. Tunamshukuru sana Dr. Mwinyihaji, amekijenga, amewapa fedha nyingi, wamenunua vifaa vya kisasa na wanafanya kazi nzuri kweli kweli.

Tunashukuru jirani zetu Jimbo la Chumbuni tayari sasa hivi wameshatia wanja kwenye jicho lao. Sasa nadhani tunajua tunakwenda hatua kwa hatua. Sasa hivi mimi namuomba sana Mhe. Waziri basi wale watendaji wanaofuatana na Mhe. Rais wamkumbushe Mkurugenzi wa *UUB.* Kule kulikuwa tayari kuna ahadi ya rais kwa wananchi wa Kwamtipura ili ile njia yetu pale kwa sababu sasa hivi daladala zinapita lakini ikija mvua kunachafuka sana hasa maeneo ya Mboriborini. Sasa mimi nadhani wangemkumbusha Mkurugenzi wa *UUB.*

Kwa sababu hata mimi mwenyewe niliandika barua hivi karibuni kwa Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kumkumbusha ahadi ya Mhe. Rais na nakala nikampelekea Katibu wa Rais. Sasa leo kwa kuwa wananchi wa Kwamtipura usiku wataangalia kioo sasa nataka wajue kwamba yale maombi yao kwa Mhe. Rais tayari nimeshamkabidhi Mhe. Waziri mwenyewe. Na ninaamini kabla ya kumaliza awamu yetu hii, basi yale makarandinga, ma-*grader* yatakuja kwa ajili ya kutia lami njia ile. Na kwa bahati nzuri njia ile ina watu wengi sana.

Sisi mwanzo tulitegemea kwamba labda kungekuwa kuna daladala tatu, lakini sasa hivi kuna daladala hazipungui 12, ikienda watu wamejaa, ikirudi watu wamejaa. Ni kwamba kweli kumbe tukitengeneza njia zetu za ndani ile programu ya kuondoa umasikini MKUZA kwa kweli ndio tutakuwa tunaitekeleza kwa vizuri. Kwa sababu mwananchi baada ya kutumia dakika 20 anakwenda kuitafuta barabara na mizigo, leo baada ya dakika mbili yuko barabarani kama anatoka shamba kapata mzigo wake kidogo, kagaiwa mashelisheli basi hana haja ya kumtafuta mchukuzi ili akazidisha umasikini. Kwa sababu akitafuta mchukuzi ina maana ile pesa itabidi atoe ampe mchukuzi, lakini kwa kuwa masafa yatakuwa yamepungua basi tutakuwa tumeweza kupunguza yale masafa. Sasa nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri hili awaagize watendaji wake wamfuate Mkurugenzi wa *UUB* ili tuweze kufanya kazi hii kwa kutekeleza ile ahadi ya Mhe. Rais.

Na kwa kuwa hivi karibuni tunakamilisha ujenzi wa chekechea nyengine Kwamtipura, mnajua Kwamtipura maendeleo tu kule hakuna blaa blaa, tunategemea katika mwezi ujao baada ya kura ya maoni tukishapata ushindi wa kishindo pale tunazindua chekechea. Kwa sababu tukizindua sasa hivi tutasema aa kampeni, aa. Tunasubiri tayari wananchi wameshasema mzee hapa mambo yake mazuri basi tunakwenda kuzindua chekechea ile. Tunategemea kwa kuwa Mzee anamaliza muda wake tutamuomba tena aje atuzindulie chekechea ile. Sasa pale anapokuja kuzindua chekechea ile basi angalau wale watendaji wa *UUB* japo kuja na zile kamba tu, wakaanza kupima pima wananchi wasije wakamkumbusha tena ile ahadi tuliyomuomba katika kile kipindi cha nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya salamu ndefu za wananchi wa Jimbo la Kwamtipura sasa hivi nataka nielezee utekelezaji wa ilani ambao Mhe. Rais wetu ameusimamia ndani ya kipindi chake cha miaka kumi.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna asiyejua wala kuona, Zanzibar tumebadilika ndani ya miaka 10. Mhe. Mwenyekiti, sisi ndio tuliokuwa wapigaji kelele wakubwa hapa, tumeanzisha utalii lakini barabara hatuna. Sasa hivi kilio kile kimetoweka, unaanza Makunduchi unakwendazako mpaka Nungwi, unasinzia kwa sababu barabara zinateleza. Haya kwa kweli ni mafanikio makubwa.

Katika eneo la miundombinu Mhe. Mwenyekiti, rais anayekuja hapati tabu. Sasa hivi yeye anakuja kuingiza mapesa mifukoni kwa wananchi. Rais Amani Karume kaweka miundombinu barabara tayari na kila kitu. Kwa hivyo, hatutegemei rais atakayekuja kuanza kuumiza kichwa katika suala la zima la barabara, kwa sababu sasa hivi tunajua hizo ambazo zimekwama tayari programu yake imeshakuwa tayari, sahihi zimeshatiwa, tayari ujenzi nyengine zimeshaanza na nyengine hatua zinaendelea.

Kiwanja cha Ndege Mhe. Mwenyekiti, wenyewe tunakiona, ilikuwa ukiteremka na ndege pale ki-*charter* basi utafikiri uko Kiboje kwenye matuta, lakini sasa hivi unateleza, unaweza kujiuliza tushafika? Kumbe vile ushatua zamani. Sasa hivi ni jitihada zake yeye na usimamizi wake Mhe. Rais wetu.

Lakini vile vile tunategemea kabla ya kuondoka na kumaliza muda wake, tunategemea atatuwekea jiwe la msingi la ujenzi wa *New Terminal Building* katiak eneo la Uwanja wa Ndege wa Zanzibar. Sasa haya kwa kweli ni mafanikio makubwa sana, kwa sababu nchi haiendelei bila ya miundombinu, kwa hivyo, tayari miundombinu ameshatuwekea kazi iliyobakia ni kuumiza vichwa kuangalia ni namna gani tutaweza kuboresha maisha ya watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali tulikuwa tumezowea kukaa katika majumba haya ya Mji Mkongwe. Waziri yuko ukumbini Katibu Mkuu yuko chooni, Wakurugenzi wako katika vyumba vya uwani, ndio majumba ya Mji Mkongwe yalivyo kwa sababu yalikuwa majumba ya watu. Sasa Mhe. Rais akasema nyinyi mtakaa humu ndio maana mambo yanakuwa hayendi mtu unakaa chooni? Wewe Katibu Mkuu uko chooni hata huoni tabu. Sasa tumeanza kuamka na kuanza kujenga majengo yetu.

Tunashukuru Mhe. Waziri wa Fedha kamuwezesha Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kajenga jengo lake, mwenyewe anaita *twin towers*, ana majengo mawili pale anaita *twin tower*, japo gorofa tano, nne zile lakini mwenyewe kwa uwezo wake anaita *twin tower* anadeka. Hizi ni jitihada za rais

wetu. Lakini vile vile Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na yeye kafuata nyayo tayari ameshajenga jengo lake pale Mazizini.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Waziri Kiongozi maana yake tusiwe tunanyoa wenzetu tu, na sisi lazima tunyoelewe kidogo. Tunamshukuru sana Mhe. Waziri anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi kwa sababu huyu ana tepe mbili, Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi lakini vile vile Waziri Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi. Ametuwezesha ametupa zaidi ya shilingi 500 milioni tayari tumeshajenga jengo zuri kabisa mwanana na la mwanzo katika maofisi kule Pemba.

Kwa hivyo, sasa hivi watendaji wetu wa Afisi ya Waziri Kiongozi Pemba tayari wameshahamia, hatujalifungua, lakini kwa vile walivyokuwa wanajiramba ramba tayari wameshahamia kwa sababuwanaona tunachelewa. Kwa kweli tumshukuru sana Mhe. Rais.

Kwa sababu tuna kipindi tulikwama, tukenda kwa Mhe. Rais, shilingi milioni mia moja tulikwama, akasema hili si uzungumze na rafiki yako Mhe. Waziri wa Fedha, nilipokuja hakuniangusha rafiki yangu, shilingi milioni mia moja zimekwenda tukamlipa mkandarasi tumemaliza sasa hivi jengo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuzungumza mafanikio tutafika asubuhi hapa. Lakini sio hivyo tu, wizara inayoshughulikia masuala ya wanawake na watoto ambayo bajeti yake ndio hii hapa leo tunategemea kuanza kuisoma. Samahani, hapoa kuna kauli ya waziri, lakini tayari Mhe. Waziri na yeye amejijengea jengo la wizara yake yeye mwenyewe. Utamaduni huu kabla ya miaka 10 tulikuwa hatuna, tulikuwa hatuamini kama tunaweza kujenga.

Sio hivyo tu, sasa hivi wale wala unga wamepungukiwa na maeneo ya kufanyia shughuli zao Michenzani. Majumba ya Michenzani pale Miembeni ilikuwa ndio *head quarter* ya wala unga, kila siku tulikuwa tunapeleka polisi pale kwa sababu yale majumba yalikuwa yameshakuwa magofu, mbu walikuwa wanazalishwa wengi pale, ukienda chni kule mbu tele. Mhe. Rais tunamshukuru yeye mwenyewe, kwa sababu sisi alipokuwa anazungumza kuwa atajenga majumba yale tukasema hee, Mhe. Rais majumba yale atayaweza? Lakini ndio yale pale sasa hivi watu wananyang'anyiana nipishe mimi, nipishe mimi. Hizi ni jitihada zake yeye mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi taasisi zetu zinajenga majengo yake wenyewe. Ukienda pale kwenye kiwanja cha Mao-tse-tung pembeni shirika la Bima tayari wanajenga jengo lao wenyewe. Wanahama pale, kwa sababu tulikuwa tumejikusanya Mji Mkongwe huko sijui tulikuwa tunafuata kitu gani, tulikuwa tunampa tabu sana Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji hapati kujifaragua. Sijui

mara imepita gari ya Katibu Mkuu, mara ya nani, kule wanatakiwa wakae wenyewe makhalati kule kina Mhe. Fatma Ferej. Sasa hivi tumehama huko tunakwenda zetu tunajenga majengo yetu ili tujinafasi.

Lakini sio hivyo tu, *ZRB* sasa hivi wanajenga jengo lao pale Mazizini. Wamehangaika walikuwa wamekodishwa na wenzao wa *ZSSF*, lakini sasa hivi na wao wanajenga. Unajua mambo haya ukiona mwenzako kafanya na wewe unaanza kuona choyo, unajiuliza kwani yeye kaweza ana nini sisi tushindwe tuna nini? Sasa ile sio nyimbo tu, lakini ile ni utendaji. Wale wasanii wanatoa mifano mizuri, wanatuamsha, leo *ZRB* tayari nadhani baada ya mwaka mmooja watakuwa na jengo lao la kisasa kabisa.

Vile vile MFuko wa Hifadhi ya Jamii wana jengo lao pale wamejenga Kilimani. Hizi ni jitihada jamani ndani ya miaka kumi. Sisi tulikuwa tunatoa mfano tunasema aa, Mzee Karume kajenga nchi miaka minane tu, sijui na nini. Kwa sababu ukiwa kiongozi unatakiwa uwe na mitazamo. Sasa wenzetu hawa Mwenyezi Mungu kawajaalia wana kipaji cha kujenga, baba yake kajenga mpaka leo tunatoa mifano na yeye kajenga, tutaendelea kumtolea mifano na atakayekuja basi na yeye aige mifano hii ndio tunavyotaka. Kwa sababu ukishajenga sio kama utajenga tena, utaendelea kujenga vyengine.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kama nilivyosema kwamba jitihada ni kubwa zilizofanyika, lakini si hivyo tu. Chuo cha Fedha, Chwaka wamejenga jengo la kisasa. Sisi mwanzao tulipokuwa tunakwenda kwenye kamati kule walikuwa wamekodishwa jengo la Benki sijui wanatumia, baada ya muda mfupi tukenda tukawakuta tayari wameshazindua jengo lao. Juzi nilitembelea mimi nikakuta wameshajenga jengo jengine na sasa hivi wanajaribu kuomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili waweze kuwapa eneo kule wajenge *hostel.* Sasa haya ni mafanikio makubwa kweli kweli.

Zanzibar tulikuwa hatuna vyuo vikuu sisi, sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, tuna vyuo vikuu kila uchochoro, ukienda Tunguu, Chukwani. Sasa hivi pale Tunguu kuna Chuo chengien cha Taifa ambacho kinajengwa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mambo haya kama kiongozi hana mitazamo ya maendeleo hatuwezi tukafanya.

Mhe. Rais yeye hakusikiliza malumbano, sisi wanasiasa tulikuwa tunalumbana, akikaa pale Mhe. Abubakar Khamis ananipiga kijembe mimi na mimi nampiga kijembe Mhe. Hamad Masuod, yeye anampasia Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapundizi. Yaani humu ilikuwa tunapeana *pass*, lakini yeye mwenzetu hata habari hana, yeye kashika maendeleo. Tena alikuwa anatwambia nyinyi kazi yenu kulumbana tu, hebu fanyeni kazi huko, fanyeni kazi kila mtu ataona.

Sasa hivi yale aliyokuwa anayasema kweli, unajua tatuzo ni Waswahili. Mswahili hupewi sifa mpaka ushafukiwa, pale watu wanapiga pauro *Lailahailallah*, *Lailahailallah*, pale ndio inasomwa risala alijenga nyumba, alitia barabara lami, kaacha pengo. Sasa kaacha pengo vipi bwana, halizibiki, halizibiki kasema nani? Jamani hebu tufanyeni utamaduni wa mtu anapofanya kitu tumsifu na yeye mwenyewe anasikia.

Mhe. Mwenyekiti, vurugu zilizokuwepo Zanzibar ilikuwa hakuna anayeona, ilikuwa ikifika wakati kama huu hapa. Kuna safari moja tulikuwa tunafanya Kikao cha Baraza hapa huko nje tunasikia tu, tu, Mhe. Jusab tulikuwa tunamtafuta yuko wapi? Alikwua Mwakilishi wa Jimbo la Amani yuko huko anapiga simu njoni leteni *FFU* mje mnitoe sipati kutoka. Pamezuka mabomu Mtendeni sijui na Mchangani hatoki, tukampelekea *FFU* ndio akaja Barazani hapa, leo usiku mtu anatembea hata habari hana. Mhe. Haji Faki Shaali yuko wapi? Analala ndani ya jimbo langu wala simuulizi, tuko vizuri. Hizi ni jitihada za Mhe. Rais Karume.

Sasa jamani kama hatukusema leo tukasema lini? Tukisubiri keshafariki Wallahi tutakuwa sote wanafiki hapa, sasa pale unamsifu nani, msifu mwenyewe asikie ili ajue kwamba hii miaka kumi ambayo wenzangu walinipa ridhaa basi wameshukuru na vile vile katika ule mchango wangu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, maendeleo haya nikiyasema mpaka asubuhi kama nilivyosema na najua Mhe. Waziri anataka ku-*wind up*. Sasa nataka nije Tume ya Utumishi, hayajesha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni waziri ambaye Idara ya Watu Wenye Ulamavu iko chini ya afisi yangu. Mheshimiwa naomba sana, Zanzibar katika nchi za Afrika Mashariki sisi ndio tuko mstari wa mbele katika kuwajali walemavu. Katika kuitikia wito wa kimataifa sisi Zanzibar tumeshatekeleza kwa asilimia kubwa, tayari tuna Sera ya Watu wenye Ulemavu na tayari tuna Sheria. Katika sera zetu na sheria tumetoa miongozo mbali mbali, moja katika haki za walemavu ni haki ya ajira. Naomba sana mawaziri wenzangu, naomba sana Makatibu Wakuu, naomba sana Wakurugenzi hasa Idara ya Utumishi Serikalini. Tunapotoa nafasi za ajira basi moja katika *priority* watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, hili bado hatujalitekeleza. Tutakuwa tunakwenda kinyume na matakwa ya Baraza la Wawakilishi. Baraza la Wawakilishi limeshaagiza, tumeshatunga sera na sheria. Sasa kama tutakuwa hatutekelezi kwa kweli tutakuwa tunakwenda kinyume. Kwa sababu hapa yote tunayoyasema baadae mwisho waziri anasema naomba fedha, fedha hizi mnikubalie nitumie katika bajeti yangu ya mwaka 2010/2011. Miongoni mwa fedha zile kwa yale maombi, maoni au ushauri au maelekezo yaliyotolewa na Baraza la

Wwakilishi. Sasa kama tutakuwa tunaruhusu fedha zitumike, lakini katika zile sheria zilizotungwa hatuzitekelezi, kwa kweli tutakuwa hatutendi haki.

Sasa nilikuwa naomba sana Idara ya Utumishi Serikalini basi wanapofanya masuala ya ajira watu wenye ulemavu waweze kuangaliwa kwa jicho la huruma. Na sio watu wa kuonewa huruma tu, kwa sababu wana uwezo. Sasa hivi walemavu wamesoma wengi, lakini vile vile kazi nyengine mbali mbali wanaweza kuzifanya na hata zinapotolewa hizi fedha za mifuko mbali mbali basi walemavu ni watu ambao wakuangaliwa kwa jicho la karibu ili na wao wajisikie kwamba hawana tofauti na watu wengine.

Kwa sababu kama hatukuwapa hizi nafasi za ajira ndio pale watakapoaendelea kudharaulika na ndio watapokuja kutuomba na wakiwa wanatuomba sana sisi wenyewe tutaanza kulalamika au tutakuwa tunawakimbia. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana ili ndugu zetu hawa waweze kupatiwa nafasi za ajira.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia malizia nadhani sasa hivi nchi yetu iko katika maendeleo makubwa kabisa. Bandari yetu ile pale sasa hivi inafanya kazi vizuri, makontena usiku na mchana yanateremshwa. Kwa hivyo, tunaomba watendaji wetu wazidishe jitihada lakini pia waweze kuchunga kile kinachopatikana katika hizi bandari zetu.

Kwa sababu jitihada zote hizi, hii miundombinu yote, hapa Mheshimiwa alikuwa anatega mfyusa, mfyusa wenyewe nini? Ili fedha ziweze kunasa. Haya yote niliyoyazungumza tumejenga hapa, tumefanya hiki na hiki, ili maeneo haya yaweze kufanya kazi tuweze kupata fedha na kuweza kuboresha maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunaendelea tena kumpa shukurani zetu za dhati Mhe. Rais. Lakini vile vile Mhe. Waziri ambaye amemuweka pale anamsaidia kazi zake kwa kweli anamsaidia kwa umakini mkubwa na sisi anatupa mashirikiano makubwa sana.

Kwa hivyo, kwa niaba ya wananchi wa Kwamtipura naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipatia wasaa huu wa kuja kufanya majumuisho katika hotuba yangu ya makadirio ya fedha ya Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, lazima nikushukuru kwa dhati kabisa wewe pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza kwa kuweza kuisoma, kuisikiliza na kuitafakari kwa undani kabisa hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nilizungumza wakati wa hotuba ya bajeti ya serikali kwamba michango ya mwaka huu ni ya aina yake na nazidi kutoa kauli hiyo tena kwamba michango ya mwaka huu ni ya aina yake na ya kupigiwa mfano kabisa. Hii yote inaonesha umoja, ustahamilivu kati yetu, mashirikiano na nathubutu kusema kumkubali kwa dhati kabisa Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Njia aliyotuonesha, mustakbali aliotuwekea huko tunakotaka twende nafikiri ni kigezo tosha kwa waheshimiwa wote kuweza kuikubali hotuba hii na kutupa moyo sisi watendaji kwamba tuzidishe juhudi za kuwa nae bega kwa bega kufanikisha yale malengo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, takriban waheshimiwa wote waliochangia wameikubali hotuba hii kwa asilimia mia moja, labda nikiondoa waheshimiwa wawili watatu tu, nao wamesema wataikubali lakini kwa asilimia 50 kwanza au thamanini mpaka wapate maelezo mawili matatu tu. Hayo tutawatolea lakini kwa sababu ya muda kama binadamu sikuwapa vizuri basi naomba wasinipigie buti sana tukutane nje huko nitawapa ufafanuzi mwingi tu. Lakini nitajitahidi kadri ya uwezo maana yake Mhe. Mwenyekiti, umetupa dakika 45 za majumuisho. Kwa hiyo, nitajitahidi kwenda ndani ya hizo dakika 45 kama kanuni zinavyosema kama itayumkinika.

Unajua majumuisho huwa ni mengi na Mhe. Mwenyekiti, ni vizuri kila mmoja tumguse kwa hoja yake kwa sababu zote ni za msingi na zina manufaa katika nchi yetu na majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti: Ni sawa Mhe. Waziri na tutawaomba wale waheshimiwa walioko nje waje basi ili wasije wakapiga buti kumbe huku majumuisho yanaendelea.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa ujumla tulikuwa na michango 22, waheshimiwa 20 walipata nafasi kuchangia hapa ukumbini na wawili walichangia kwa maandishi. Kwa hiyo, naomba niwataje mmoja baada ya mwengine:-

1. Mhe. Haji Mkema Haji
2. Mhe. Zakiya Omar Juma
3. Mhe. Ali Suleiman Ali

4. Mhe. Haji Faki Shaali
5. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
6. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
7. Mhe. Rashid Seif Suleiman
8. Mhe. Hija Hassan Hija
9. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
10. Mhe. Moh'd Ali Salim
11. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
12. Mhe. Abass Juma Muhunzi
13. Mhe. Ali Abdalla Ali
14. Mhe. Abdulla Juma Abdulla
15. Mhe. Salmin Awadh Salmin
16. Mhe. Juma Duni Haji
17. Mhe. Mzee Ali Ussi
18. Mhe. Ame Mati Wadi
19. Mhe. Zainab Omar Moh'd
20. Mhe. Hamza Hassan Juma

Mhe. Mwenyekiti, hao wote ndio walipata fursa ya kuchangia hapa ukumbuni na kulikuwa na waheshimiwa wawili walipata fursa ya kuchangia kimaandishi. Nao ni Mhe. Ame Ussi Juma na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji. Wote tunawashukuru sana kwa michango yao mingi. Kama nilivyosema wote kwa kweli wameiunga mkono hotuba yetu isipokuwa wametaka tu ufafanuzi wa baadhi ya mambo hapa na pale.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru sana kwa mawazo yao ambayo yalikuwa mengi na yote yalikuwa katika kuiendeleza au kuifanya Kiswahili cha kisasa Mhe. Haroun Ali Suleiman hakipendi, kuboresha. Lakini ni ukweli kwamba wametaka tuiendeleze ofisi yetu iwe na utendaji mzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla kulikuwa na mambo matano makubwa ambayo Waheshimiwa Wajumbe haya ndio hasa wengi waliogelea. Mbali ya *specific issues* lakini wengi waliogelea kwenye mambo haya matano ambayo naomba niyataje.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ni suala la ukomo wa mageuzi ya utumishi wa umma. Wajumbe waliochangia mada hii ni Mhe. Zakiya Omar Juma, Mhe. Moh'd Ali Salim, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na Mhe. Salmin Awadh Salmin. Hao walizungumza sana suala la ukomo wa mageuzi ya utumishi wa umma yamekuwa muda mrefu, yataanza lini, tumefikia wapi. Nitajaribu kutolea ufafanuzi hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, pili suala la utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa umma na suala zima la uelewa wa *G.O.* Mhe. Mwenyekiti, waheshimiwa wengi walisema kwamba *G.O* ipo lakini watu wetu hawaijui, wanakwenda kwenye *G.O* mpaka pale wanapokuwa na haja tu kafukuzwa kazini au kuna matatizo, huo si utaratibu mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, tunakubaliana nao Mhe. Haji Mkema Haji, Mhe. Moh'd Ali Salim, Mhe. Zakiya Omar Juma na Mhe. Haji Faki Shaali walizungumzia sana masuala ya *G.O*.

Mhe. Mwenyekiti, tatu ilikuwa suala la wafanyakazi katika sekta hasa za elimu na afya. Kuna nafasi za upendeleo kidogo watu wanapatiwa hasa kwa mfano Chuo cha Afya Mbweni. Lakini pia katika utendaji watu wanabaguliwa. Si kweli, katika serikali yetu hakuna ubaguzi huo, si sera ya serikali. Sasa kama kuna utashi wa mtu mmoja au wawili hilo ni masuala yake na si suala letu, lakini nao ni wa kukemewa.

Hayo yapo wazi kabisa katika wizara zetu zote, huko Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunakosema, huko Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuna watu tunaowafahamu hasa kwamba wako vyama vya upinzani lakini hawabaguliwi. Muhimu kwamba usitekeleze mambo ya siasa kwenye kazi. Wao wanafanya kazi zao vizuri, wana dhamana zao, michango yao mikubwa kweli kweli, ni wataalam wazuri tu na tunawaheshimu kama inavyostahiki.

Kwa hiyo, kwa kweli si sera ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwabagua wafanyakazi hapana. Hilo tunakanusha kabisa na tutalipiga vita kwa nguvu zote, mtu atakayeleta masuala ya ubaguzi ya kijinsia, ya kidini, ya kikanda au ya kiitikadi ndani ya utendaji wetu wa serikali. Hayo Mhe. Mwenyekiti, siku zote tunayakemea na tutazidi kuyakemea.

Hili suala lilizungumzwa na Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Moh'd Ali Salim, Mhe. Ali Abdalla Ali na Mhe. Ame Mati Wadi.

Lakini pia kulikuwa na suala la kuboresha maslahi ya wafanyakazi na ongezeko la pencheni. Tuliambiwa kwamba kuna watu bado wanapata shilingi elfu tano namna gani? Tulishauriwa kwamba kile tulichoongeza juzi ni kidogo tukiongeze, mpaka wengiene wakashauri labda ifikie laki moja. Sasa tukiweka leo laki moja kwa mfanyakazi wa chini, yule anayestaafu nae tumpe laki moja, basi kila mtu angetaka astaafu apate lakini moja. Kama mimi sasa hivi nastaafu nataka laki moja na yule mfanyakazi wa chini laki moja, kila mmoja angeacha kazi akaikimbilia laki moja.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli kwamba uwezo tunataka tuwanyanyue, kadri ya uwezo wetu unavyokwenda kidogo kidogo basi tutawanyanyua. Tusingependelea kweli ile mnayosema omba omba mitaani humo si lengo letu. Ndio maana serikali kwa makusudi ikajenga zile nyumba za wazee Sebleni kuwastiri wazee wetu na kuwasaidia.

Hawa wafanyakazi labda waheshimiwa ningesema mapema hawastaafu, kuna wengine wazee wana mifuko yao maalum wanapewa mikoani kule kama kuwasaidia na wao. Sasa tusichanganye na hawa ambao wengine ni wastaafu wa mawizara kidogo kuna *category* tofauti. Unajua ndivyo ilivyo wakati fulani tulikuwa tuna wizara inayoitwa Wizara ya Kuweka Hali za Wananchi Sawa. Hii yote kuwasaidia wazee wetu wasiadhirike baada ya maisha. Lakini sasa kadri tunavyokwenda mipango tunaiweka mizuri zaidi mpaka tumefikia sasa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mfuko huu nao tunauendeleza zaidi ili mambo yakae vizuri zaidi.

Lakini pia kulikuwa na suala zima la tano katika masuala ya jumuiya za kikanda tunazoshiriki kama Zanzibar kama ni nchi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeulizwa tuna faida gani. Mhe. Ame Mati Wadi alisema naona mnaandika mnajaza makaratasi tu, si kweli kama tunafaidika.

Mhe. Mwenyekiti, namhakikishia Mhe. Ame Mati Wadi kwamba tunafaidika na nitakuja kueleza maelezo yetu. Huu ulimwengu tunauita ulimwengu wa *globalization* yaani wa utandawazi. Hatuwezi kujitenga sisi tukasema tuwe peke yetu tu kama kisiwani aaa hatwendi hivyo. Si kibiashara, si mashirikiano, si chochote, lazima ushirikiane na wenzako. Mashirikiano yanaanza kwanza ndani ya Muungano, kikanda na kimataifa. Kwa hiyo, Mhe. Mati faida zipo nyingi na ninafahamu kwa falsafa zako ulitaka kuuliza tu lakini naamini unafahamu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, hili limechangiwa vizuri sana na Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Zakiya Omar Juma, Mhe. Hija Hassan Hija, wote walitaka kujua na nitajaribu kueleza kadri ya muda utakavyoruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, waheshimiwa wengi wametoa sifa kama nilivyosema nyingi sana kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa niaba yake na kwa ofisi yake na wafanyakazi wote wa Wizara ya Nchi (AR) Ikulu tunazipokea sifa hizi na tutaziwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema tu kwamba mara nyingi sana Mhe. Rais akipokea sifa hizi yeye kauli yake au mara nyingi huwa anasema sifa hizi kwanza nawarejeshea nyinyi Waheshimiwa Wajumbe. Nawarejeshea nyinyi wananchi kwa sababu nyinyi ndio mlioniwezesha mimi kama Kamanda

kuyasimamia vizuri. Bila ya ushirikiano wenu, bila ya ujasiri wenu tusingefanikiwa hapa. Hayo mara nyingi Mhe. Rais huwa ana-*attribute* mafanikio yake kwa wananchi na viongozi wengine kwa kukubali kufanya kazi nae pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nachukua fursa hii kwa niaba ya Mhe. Rais kukushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza na wananchi kwa ujumla kwa miaka 10 hii kufanya kazi vizuri kabisa na kumkubalia yale aliyokuwa akiyaongoza Mhe. Amani Abeid Karume hata kufikia mafanikio yaliyopatikana. Mhe. Mwenyekiti, sifa tumezipokea na kama nilivyosema tutaziwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mhe. Haji Mkema Haji alizungumzia suala zima la ukarabati wa Ikulu zetu za nyumba za Chake Chake, Wete na Dar es Salaam ambazo zipo katika hali ya kuridhisha. Tunashukuru sana. Ni mara nyingi kwa kweli kamati hii imekuwa ikitushauri sana juu ya *maintenance* ya nyumba zile na kwa kweli mara nyingi hushauri baada ya kutembelea wao *physical* kwenda kuona. Ushauri tumeuchukua na tutaufanyia kazi. Tutazidi kuziendeleza kadri hali ya kifedha inavyoruhusu.

Mhe. Haji Mkema Haji alituuliza hatua gani zinachukuliwa katika kupata kiwanja cha kujenga nyumba ya makaazi ya Mhe. Rais kwa Dar es Salaam. Nataka kusema kwamba kulikuwa na juhudi mbali mbali tokea Mkuu wa Mkoa wa zamani aliyepita Mhe. Abass Tarimba, halafu huyu Mhe. William Lukuvi ili kuweza kupata kiwanja. Juhudi hizo tunaendelea nazo na naamini ushirikiano mzuri wameonesha wenzetu na *inshaallah* tutafanikisha hili suala.

Mhe. Haji Mkema Haji pia alitaka kujua majina sahihi ya miradi inayoratibiwa na Idara ya Mipango na Sera katika Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Labda kulikuwa na majina huku kwenye buku yanasema vyengine na kwenye hotuba yetu tulisema vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli kwamba Afisi ya Rais Ikulu ina miradi miwili, wa kwanza ni Mradi wa Uimarishaji Mawasiliano Ikulu na wa pili ni Ukarabati wa Ikulu na Nyumba za Serikali *(Rehabilitation and Construction of State House and State Lodges).* Hayo ndio majina halisi, kama yametajwa vyengine basi labda ni kwa makosa tu, naomba isomeke hivyo.

Aidha, Mhe. Haji Mkema Haji alitoa ushauri kwa Idara ya Mawasiliano Ikulu kwamba usambazaji vipindi vingi zaidi Pemba vioneshe maendeleo yaliyopatikana katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Tunamshukuru Mhe. Makamo Mwenyekiti, Mhe. Mkema na ushauri wake tumeupokea. Kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo tutajitahidi

kushirikiana nao ili tuone kwamba na wenzetu wa Pemba juu ya matatizo ya kwamba TV haifanyi kazi lakini wanaona mafanikio tuliyoyapata katika hizi nyanja alizosema za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Kuhusu kuongezwa kwa kiwanja cha ujenzi wa Chuo cha Utawala wa Umma. Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema kwamba tutajitahidi kushirikiana na wizara inayohusika, yaani Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na wao wameshaahidi kwamba watalifanyia kazi suala hili. Tume-*note concern* ya Mhe. Haji Mkema Haji tumeona kweli kwa kadri tutakavyokuwa lazima tupate kiwanja zaidi. Kwa hiyo, hilo tumelichukua tutashauriana na wenzetu.

Mhe. Haji Mkema Haji pia alitushauri kwamba tuyafanyie kazi yale mapungufu yaliyobainika kwenye *NACTE*. Nasema mapungufu hayo tayari yamebainika na yameshafanyiwa kazi na kuwasilishwa tena katika Baraza hilo kwa idhini yao. Kwa hiyo, hili tayari tumeshalishughulikia.

Aidha, Mhe. Haji Mkema Haji alitoa ushauri kuhusu suala zima la uandaaji wa mafunzo kwa watumishi wa umma katika kada ya huduma. Ushauri huu nao nasema tumeupokea na pia tutaufanyia kazi. Kwa ujumla Mhe. Mkema tunakushukuru sana kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na haya yote mliyotushauri tumeyasikia na tutayafanyia kazi kama nilivyosema kuiendeleza Afisi yetu hii ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara hii, Mhe. Zakiya Omar Juma nae tunamshukuru sana kwa michango yake kwa kweli ametusifia sana na tumezipokea hizi sifa alizozitoa. Pia alitaka kujua kwamba mageuzi ya utumishi wa umma lini yatafikia kikomo au yanaanza, kila siku tunaimba tu nyimbo hii, yataanza lini yatafikia kikomo.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema kwamba *concept* ya mageuzi inaendelea, hayako kwamba umefanya leo tena ukae miaka 10 ndio uanze tena. *Concept* ya mageuzi katika utumishi siku zote kadri maisha yanavyobadilika na kadri sera zinavyobadilika basi na hili suala nalo linabadilika. Hilo nataka tulifahamu kwamba haya mambo yanabadilika kwa hiyo na sisi lazima twende na wakati, kadri mambo yanavyobadilika na sisi twende na wakati tuyabadilishe.

Hatuwezi mfano tukasema *scheme of service* yetu hii kwa miaka 20 na mshahara huu aaa, lazima tubadili hali na tuziboreshe. Kwa kweli tunajitahidi kuyafanya haya kwa kushirikiana na wenzetu hasa wafadhili kwa kulinganisha na labda nchi nyengine wanafanya vipi. Wafadhili wetu wakubwa katika masuala haya ni *World Bank* na tunashukuru tunakwenda nao sambamba.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema zaidi kwamba mchakato wa mageuzi ya utumishi wa umma tayari yamefikia pazuri. Miundo ya utumishi tayari imekamilika kwa baadhi ya wizara. Kwa mfano, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wao wameshafaidika na miundo hiyo mipya.

Aidha, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii nao pia kwa sehemu moja wamefaidika. Sasa kama nilivyosema tunakwenda kwenye wizara nyengine za serikali zilizobakia. Pia suala hili pia Mhe. Moh'd Ali Salim aliliulizia tunamshukuru na niseme hayo tu kwa sasa.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri alioutoa Mhe. Zakiya Omar Juma wa kupatiwa mafunzo ya *G.O* kwa watumishi wa umma. Ushauri huu nao tunaupokea na tunamhakikishia kwamba mafunzo yatakuwa endelevu, tutayaendeleza kwa watumishi wote na kwa muda wote. Nakumbuka hata Mhe. Haji Faki Shaali aliuliza swali hili na yeye mara nyingi huwa ana-*insist* suala la *G.O* kusomeshwa watumishi. Tusingoje tu mpaka inapotokea shida tena ndio tunakwenda kufanya *reference* ya *G.O* lakini wasomeshwe kwa muda wote. Hilo tumelisikia nalo tutalifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu maslahi ya wafanyakazi na kupandishwa kwa pencheni naomba nichukue fursa hii kumhakikishia Mhe. Zakiya Omar Juma kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitasita kufanya hivyo kila hali itakaporuhusu kwani inajali sana maslahi ya wananchi wake. Hali itakaporuhusu basi tutajitahidi na sisi kurekebisha haya maslahi ya wafanyakazi wetu ili twende na wakati na hali ya maisha ilivyo.

Kuhusu ahadi za Mhe. Rais anapotembelea maeneo mbali mbali kama vile ujenzi wa barabara iliyopo ndani ya Chuo cha Utalii. Tunamshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi kwa kulitolea ufafanuzi suala hili. Si lengo kwamba ahadi za Rais zichelewe isipokuwa labda ni tofauti ya wakati tu kama itafanywa leo, itafanywa kesho lakini kwa kweli ahadi zote za Rais tunazipa kipaumbele kwamba zifanywe kila anapotuagiza. Kwa sababu kwetu si ushauri lakini ni agizo, kiongozi wetu anapotoa agizo hatuna budi kulitekeleza. Kwa hiyo, tunakuahidi Mhe. Mwenyekiti, ahadi zote za Mhe. Rais alizozitoa tutajitahidi kwa kushirikiana na wizara husika kuzitekeleza mapema kadri inavyoyumkinika.

Halafu kulikuwa na suala zima la uratibu wa uchumi na uhusiano wa kimataifa. Hapa kama nilivyosema waheshimiwa wengi waliogelea sana katika suala hili. Kwa kweli ni suala muhimu sana kwa sababu kama nilivyosema sisi Zanzibar tuko kisiwa, sasa ushirikiano wetu uwe wa kisiwa tumetengwa tengwa sivyo, lazima na sisi tujihusishe na wenzetu. Hata hiyo biashara yetu hatuwezi ku-*deal*

na *population* ya watu milioni moja tu lazima tutoke nje tutafute masoko. Hapo sasa ndipo yanapokuja hayo masuala tunayoyaita ya *integration*.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala yeye ametupongeza kwa kazi nzuri na kutupa ushauri. Kwa kweli tumezipokea pongezi zake na tumeupokea ushauri wake na tunamuahidi tutaufanyia kazi.

Mhe. Waziri Kivuli kwa upande wake alitaka kujua Zanzibar inanufaika vipi na lipi katika mashirikiano ya kikanda. Vile vile alitaka kuelewa kwa nini isiende peke yake katika mashirikiano hayo badala ya kuwakilishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Si yeye tu kama nilivyosema waheshimiwa wengi waliulizia suala hili la *integration*, Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Zakiya Omar Juma, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Ame Mati Wadi na wengine wengi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema kwamba masuala haya ya ushirikiano wa kikanda ni mojawapo ya sera kuu ya biashara inayofuatwa na nchi nyingi ulimwenguni. Ushirikiano huu unaweza kuchukua sura zifuatazo:-

1. Usimamizi wa uchumi mkuu *(micro economic policies).*
2. Mzunguko wa rasilimali mbali mbali za uchumi.
3. Uhuru wa biashara baina ya mataifa yaliyokubaliana kujenga ushirikiano *(integration).*

Lazima mnakubaliana, mkishakubaliana tena ndio mnaanza hayo mashirikiano. Kwa utaratibu huu hakuna nchi mwanachama ambaye atakuwa mfadhili ila wanakubaliana kupanua masoko. Hayo masoko hamuwezi kuingiliana kuuziana bila ya kukubaliana. Kwa hiyo, suala la msingi kwanza ni kukubaliana.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar nayo inayo nafasi ya kushiriki na kufaidika hata kama ikiwa chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Suala kubwa hapa ni kwa vipi Zanzibar inaweza kutumia fursa ya ushirikiano unaojengwa. Ndio maana hivi karibuni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na sekta binafsi kupitia Baraza la Biashara iliandaa mkutano maalum uliozingatia masuala ya ushirikiano kwa ujumla wake na hususan maandalizi ya Zanzibar kuhusu namna gani itaweza kufaidika na ushirikiano huo katika Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, kikao cha *Business Council* kilichopita tuliwaalika wanachama wote na wafanyabiashara takriban wote wa Unguja na Pemba na walikuja pale wakatoa maoni yao vipi Zanzibar tunaweza kufaidika na ushirikiano huu. Kwa kweli kikao kile kilikuwa kizuri na ushauri wao wote

waliotupa serikali tutauzingatia na hususan Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile suala la kwa nini Zanzibar isishiriki peke yake. Suala hili naweza kusema kwamba halina utata kwa Zanzibar kuweza kushiriki peke yake. Hata hivyo, ushirikiano wa kimataifa unategemea sana *sovereignty* na kwa upande wetu kama tunavyofahamu kwamba suala hili kwa sasa linaendeshwa kimuungano. Tukienda kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki tuko chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hata hivyo, inawezekana kuwepo kwa makubaliano ya kukasimu uwezo kwa Zanzibar kwenda peke yake katika eneo lolote la ushirikiano wa kimataifa ilimradi mazungumzo yawepo tu. Mhe. Mwenyekiti, hayo tunayafanya na *issue* nyingi sana tumeshawahi kuzipeleka ambapo Zanzibar tunaomba sisi tufikiriwe kipekee pekee. Wametukubalia wenzetu tumezungumza hilo na tumefanikiwa. Ipo baadhi ya mifano si mingi ambayo tume-*pause* kwamba kwa Zanzibar jamani hili haliwezekani. Kwa hiyo, wametusikiliza na wametukubalia.

Mhe. Haji Faki Shaali alitaka kuelewa kuhusu miradi ya Zanzibar iliyopelekwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni mingapi, itafanya kazi wapi na gharama zake. Miradi iliyopelekwa ni hii ifuatayo:

1. Ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar.
2. Uwekaji wa vituo vya umeme wa upepo Zanzibar.
3. Ujenzi wa bandari ya Maruhubi.
4. Miradi mitano ya kilimo.
   (a) Utafiti wa kilimo cha baharini hasa biashara ya uzalishaji wa zao la mwani;
   (b) Magonjwa ya wanyama;
   (c) Teknolojia ya kuongeza ubora wa mazao;
   (d) Uimarishaji wa karantini za mazao na mifugo; na
   (e) Uimarishaji wa miundombinu ya uvuvi katika bahari kuu.
5. Mradi wa Uanzishwaji wa Huduma za *Roll on and Roll off* kati ya bandari za Dar es Salaam, Zanzibar na Mombasa.
6. Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Pemba ambao umeshapata ufadhili wa *ADB* na pia utatekelezwa kikanda.

Mhe. Mwenyekiti, kati ya miradi iliyopelekwa *East African Community* kwa ushirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mradi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar tayari umeshapatiwa ufadhili kwa utekelezaji wake kwa mkopo ambao unadhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Watu wa China yaani *Exim Bank* tayari wameshapata kazi hiyo na tunashukuru kwamba matayarisho yote ya ujenzi huu wa *terminal building* yameshakamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza wakati wowote.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu gharama za miradi hiyo kazi ya usanifu wa kuweza kujua gharama halisi bado haijafanyika. Hata hivyo, sekta husika zimetayarisha gharama za awali za miradi hiyo. Kwa mfano, kule Uwanja wa Ndege kulikuwa kama dola za Kimarekani 70.2 milioni na baadae zikafikia 72 milioni.

Mradi wa pili mfano mradi wa Vituo vya Umeme wa Upepo dola za Kimarekani 70 milioni. Tatu, Ujenzi wa bandari ya Maruhubi dola za Kimarekani milioni 400. Nne, Utafiti wa Kilimo cha Baharini dola za Kimarekani 60 milioni. Tano, Utafiti wa Magonjwa ya Wanyama dola za Kimarekani milioni 10. Sita, Teknolojia ya kuongeza ubora wa mazao dola za Kimarekani 11.5 milioni. Saba, Uimarishaji wa karantini za mazao na mifugo dola za Kimarekani 22 milioni. Nane, Uimarishaji wa miundombinu ya uvuvi katika bahari kuu mradi huu utatekelezwa kama sehemu ya mradi wa ujenzi wa bandari ya Maruhubi. Tisa Mradi wa Huduma za *Roll on / Roll off* hesabu za awali hazijatayarishwa kuhusu ghamara halisi za utekelezaji. Miradi yote hii tumepanga ifanyike hapa kwetu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na yeye pia alitaka kujua namna gani Zanzibar itafaidika kuhusu utaratibu mpya unaotaka kuanzishwa wa *SADC* wa *uni-visa*. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwamba suala hili bado ni tete ambalo lina athari ya moja kwa moja ya kimapato na kiusalama kwa nchi yetu. Hata hivyo, hatua inayoendelea kwa kamati maalum imeundwa kulichunguza kwa undani suala hili kwa ajili hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mwengine aliyechangia ni Mhe. Hija Hassan Hija ambaye alitaka kufahamishwa hatua za mazingatio ya miradi ya Zanzibar iliyowasilishwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili itekelezwe kikanda.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya kuwasilisha mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nilieleza mchakato uliopita kukubaliana na idadi na kipaumbele cha miradi ya Zanzibar. Nilieleza kwa undani kuwa kamati maalum ya wataalam kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Sekretarieti iliundwa kuzingatia maombi ya miradi ya Zanzibar. Miradi iliyowasilishwa kwa ujumla ilionekana inafaa na ni muhimu kwa uchumi wa Zanzibar.

Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa utafiti yakinifu na usanifu wa miradi hiyo, ilikubalika kuanza na hatua ya kuifanyia utafiti na usanifu ili kuweza kupata gharama halisi za miradi hiyo na baadae kuanza kuitafutia ufadhili wa kikanda.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kupata gharama halisi za utekelezaji wa miradi itawezekana pia kuelewa ratiba ya utekelezaji. Hata hivyo, kwa miradi ambayo kwa sasa imepatiwa ufadhili kwa upande wa Pemba na Unguja matayarisho ya utekelezaji yameshaanza.

Mhe. Mwenyekiti, mwengine ni Mhe. Ali Abdalla Ali ambaye aligusia suala zima la ushirikiano la shirikisho la Afrika Mashariki kwa kueleza kuwa taarifa za mikutano huwa zinachelewa.

Mhe. Mwenyekiti, suala hilo ingawa huwa linatokea kwa baadhi ya mikutano ya kisekta lakini halijaathiri ushiriki wa Zanzibar katika mikutano mbali mbali iwe ya kitaalam au ya kisera ambapo watendaji na mawaziri hushiriki. Mikutano hii kwanza mara nyingi huwa inaanza kwa wataalam, halafu wanakuja Makatibu Wakuu ambao ndio wataalam wakubwa, baadae wanafuatia Mawaziri na mwisho viongozi wa nchi.

Mhe. Mwenyekiti, siku zote huwa imeshatoka ratiba ya muda mrefu ya mikutano hii. kwa hivyo wewe mwenyewe kama unakumbushwa tu. Hapa tunamshukuru sana Mheshimiwa wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Naibu wake, Mhe. Kamal na Mhe. Moh'd Aboud, mara nyingi wanatuletea barua na wako wepesi sana, wakijua mkutano uko wiki ijayo basi wanatuletea barua. Kwa hivyo, wenyewe tunajipanga kushiriki.

Pia tunamshukuru Katibu Mkuu wa Afisi hii yeye ndiye anayewasiliana na wizara zote. Anawaandikia kwanza wataalamu mpaka Makatibu Wakuu na sisi mawaziri anatukumbusha kwamba jamani kuna kikao fulani, ngazi ya wataalamu siku fulani, Makatibu Wakuu siku fulani na mawaziri siku fulani.

Vile vile mambo ya fedha yote anayaratibu yeye. Kwa hivyo, hakuna tena kile kilio kama zamani kwamba fedha hakuna. Kwa hivyo, ushiriki wetu ni kikamilifu na tunashiriki katika ngazi zote zinazopaswa.

Kwa upande wa maandalizi ya shirikisho kama nilivyoeleza katika hotuba yangu kuwa suala hilo bado linajadiliwa katika kamati ya wanasheria, na kwamba taarifa tulizonazo mikutano ya kamati hiyo haijakumbwa na tatizo la ucheleweshaji au uchelewaji wa taarifa.

Mhe. Mwenyekiti, mchangiaji mwengine ni Mhe. Abdalla Juma ambaye alisema hajazoea lakini anajifundisha kusema kwamba anakubali hotuba hii.

Ndio kama tulivyosema Mhe. Abdalla Juma kuwa tubadilike. Mimi nakushukuru kuwa umeshakubali ile *concept* ya kubadilika. Kwa hivyo, umezoea zamani kusema nitakubali baadae, leo umeanza kusema nakubali mwanzo. Mheshimiwa tunakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdalla alitaka kufahamishwa kuhusu hatua iliofikiwa ya Tanzania kujiunga na Jumuiya ya Kiislam yaani *OIC*. Mhe. Mwenyekiti, suala hili liliulizwa pia kwenye hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi alipowasilisha mapato na matumizi ya afisi yake kwa mwaka wa fedha 2010/11.

Mhe. Waziri Kiongozi aliitolea maelezo mazuri kuhusu hatua iliyofikiwa juu ya suala hili. Sitaki nirejee tena yale maelezo ningeomba tufanye kumbukumbu tu.

Mhe. Mwenyekiti, mjumbe mwengine alikuwa ni Mhe. Salmin Awadh ambaye kwanza alishauri kuimarisha kwa Afisi ya Uratibu wa Uchumi na Ushirikiano wa Kimataifa na kuomba kueleweshwa zaidi ya miradi ya ki-Zanzibar iliyowasilishwa katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na vipi miradi imetafutiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, naamini hayo nimeyazungumza kwa undani. Lakini nakubaliana na yeye kwamba ipo haja afisi yetu kuimarishwa, unajua kitengo kile ni kipya na tunazidi kukiendeleza kadiri siku zinavyokwenda.

Kuhusu idadi ya miradi. Naomba apokee taarifa niliyoitoa hapo awali wakati nikiwajibu waheshimiwa wengine. Kwa upande wa upatikanaji wa fedha sekreterieti ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki huanzisha mchakato wa kutafuta fedha kwa miradi ambayo imepangwa kutekelezwa kikanda, kutoka kwa wafadhili mbali mbali kwa njia ya aina ya mkopo au ruzuku. Wao wenyewe kama sekreterieti au Jumuiya hawana pesa ya kusema kuwa hizi za miradi fulani, wao ni kama *facilitate* tu wanasaidia kutafutia *World Bank*, ADB na kwengineko, hiyo hasa ndio *concept* wanayokwenda nayo.

Mhe. Mwenyekiti, mchangiaji mwengine wa hotuba yangu alikuwa ni Mhe. Ame Mati Wadi ambaye kama nimemuelewa vizuri, kidogo alitaka kufahamu zaidi zile *concept* nzima au ushirikiano wa kimataifa. Nafikiri kwa maelezo niliyotoa hapo awali nafikiri sasa ametufahamu, naamini anafahamu na atatusaidia kuwafahamisha wengine. Kwa sababu tumeandaa semina nyingi na mikutano. Mhe. Ame Mati Wadi huwalikuwa mchangiaji mzuri tu na huwa anatoa fikra nzuri tu za kunufaisha haya ambayo ninayasema. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Ame Mati Wadi, sasa yeye awe balozi kwa hawa watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Ame Mati alitaka kujua juhudi zaidi Baraza litafahamishwa vipi kuhusu haya mawasiliano au haya mambo ya Jumuiya kati ya Baraza na wananchi kwa jumla. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema semina tulikuwa tukifanya mikutano. Nafikiri tulimualika mpaka Waziri wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na mikutano yetu ya *business council* hii yote na waheshimiwa wengi tunawaalika. Nafikiri hizi hasa ndio njia zetu za mawasiliano. Naamini kama nilivyosema kuwa wao sasa wawe mabalozi kwa wananchi wetu kufahamu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo liliibuka zaidi ni suala zima la biashara, ambapo Mhe. Ame Mati Wadi alisema kwamba uanzishwaji wa soko huru la biashara la *SADC* kwamba halina maana tunafanya haya kwa kujaza makaratasi tu kwa Zanzibar hayana maana yoyote.

Naomba kumfahamisha Mhe. Ame Mati Wadi kwamba nchi zilizokubaliana kwa soko la uhuru la biashara yaani *FTA*, hatua ya kwanza inayochukuliwa ni kuondosheana kodi baina yao kwa bidhaa zinazozalishwa katika nchi zao. Ingawa wanaweza kutoza tofauti kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi wanachama wa soko hilo.

Kwa upande wa *SADC* nchi wanachama walianza utaratibu wa kuondosheana kodi za ndani tokea mwaka 2000 na kwamba sasa viwango vya kodi hiyo vimeweza kuanzisha soko huru la biashara. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nayo imechukua hatua hiyo na kuihusisha Zanzibar. Nasema hilo kwa upande wa *SADC* lakini nataka tukumbuke tu mbali ya *SADC* lakini pia sisi ni wanachama wa Jumuiya hii ya Afrika ya Mashariki. Sasa hizi ni kanda za kibiashara ambazo zote inabidi tutizame yale mambo yanayotuhusu na tunashirikiana vipi.

Mhe. Ame Mati vile vile naomba nimtowe wasi wasi, alisema kuwa kitengo cha *GSO* hakifanyi kazi, kinafanyakazi kwa itikadi za kisiasa. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali kwamba hakuna kitu hicho na wala sio lengo letu. *GSO* ni chombo kinachofanyakazi kwa kufuata taratibu za utunzaji usalama, siri na nyaraka za serikali. Hili ndio suala la msingi, kinajitahidi kuangalia usalama, siri, nyaraka za serikali na utendaji. Unajua wakati mwengine haidhuru baadae mtu anabadilika, lakini kabla hajaingia angalau tujuwe yeye ile picha yake ikoje. Basi huko mbele tena kama atabadilika aah! Hiyo ni bahati mbaya. Lakini hapa mwanzo tusiseme do! Baada ya siku tatu tumeshamuajiri tunajuta kwa nini tumemuajiri. Hilo ndio haswa *essence* ya suala zima la *vetting* na ndugu zetu hawa wa *GSO* na kazi zao. Tusiwe na wasi wasi nao.

Mwisho tunakubaliana na ushauri alioutoa kuhusu uimarishaji wa umoja miongoni mwetu. Naamini sote tumeshuhudia utandikaji wa misingi imara wa safari ndegu iliopo mbele yetu. Mhe Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mhe. Ame Mati Wadi kwa *philosophy* yake kubwa sana.

Unajua anapoongea Mhe. Ame Mati, utaona kama anafanya masihara, lakini ukimsikiliza kila neno lake moja zito, lina undani wake na lina falsafa moja. Kwa hivyo, utulie tu kumsikiliza anasema nini, lakini utaona kama anachekesha, huwa hachekeshi ndio ongea yake tu hiyo. Mimi nakupongeza sana Mhe. Ame Mati Wadi.

Mhe. Ali Suleiman Ali na yeye tunampongeza kwa falsafa kubwa aliyoitoa na kwa sifa nyingi kwa Mhe. Rais na kwa wizara yetu kwa ujumla kwa kazi njema tunazofanya. Tunaungana naye aliposema anamshukuru Mhe. Rais, kama nilivyosema hapo awali tunazipokea salamu hizo. Zaidi alisisitiza suala zima la kutekeleza ilani ya uchaguzi ya chama tawala. Tunamshukuru kwa falsafa na upeo wake mkubwa wa kisiasa.

Mhe. Haji Faki Shaali na yeye alizungumzia suala zima la GO, hasa kwa upande wa kanuni za utumishi. Naomba nimtowe wasi wasi kwamba idara husika inahakikisha kwamba kanuni za utumishi zinafuatwa ipasavyo na kwamba Tume ya Utumishi inaandaa mafunzo ya utumishi katika mwaka wa fedha 2010/11.

Vile vile tunamuhakikishia kwamba mchakato wa ajira kwa wahitimu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali bado ni kipaumbele chetu na tutaendelea ku-*maintain temple* hiyo hiyo, kuona kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ambao bado wanahitaji wataalamu hasa kwa afya na elimu. Kwa hivyo, tunajitahidi kusomesha na kuwapatia ajira hao wanaosomeshwa.

Aidha, naomba kumjulisha Mhe. Haji Faki Shaali kwamba Ikulu ya Mkoani nayo imo katika mpango wa kazi wa mradi wa ukarabati Ikulu na ujenzi wa nyumba za serikali kwa mwaka fedha 2010/11.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Haji Faki Shaali vile vile alitaka kujua kuna faida gani inayopatikana katika kufanya upekuzi kabla ya kuajiriwa? Nafikiri hili nimeshalizungumza. Naomba kumuhakikishia au kumthibitishia Mhe. Haji Faki Shaali kuwa upekuzi wa kiusalama ni utaratibu unaotumika katika nchi nyingi kwa waajiriwa katika sekta ya umma. Faida kubwa inayopatikana ni kupata watumishi waaminifu, waadilifu na wenyekuweza kutunza siri za wafanyakazi. Hasara inayopatikana ni kinyume cha hayo.

Kuhusu safari za Mhe. Rais kwamba ziorodheshwe anazokwenda nje. Ushauri wake tumeupokea na tutajitahidi kuzifanyia kazi kwa siku zijazo.
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na yeye tunamshukuru kwa michango yake na alishauri kuhusu kujaza mapungufu yanayojitokeza katika sekta za afya na elimu. Ushauri wake tumeupokea kama nilivyokwishautolea maamuzi. Pia alitoa ushauri kuhusu suala la magari katika Afisi ya Mhe. Waziri Kiongozi, hasa Mhe. Waziri Kiongozi. Ushauri wake nao tumeuchukua na tutaufanyia kazi. Nataka kusema tu Mhe. Mwenyekiti, serikali hivi sasa imeshaagiza ma-benz matano mapya ambayo mengine ni ma-*cruiser* matatu mapya. Kwa hivyo, suala la matatizo ya usafiri kwa viongozi wetu lote litaondoka kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Makame Mshimba kidogo akaangalie tena lile gari la Mhe. Waziri Kiongozi, inayovuja pale sio *diesel* yale ni maji ya *AC*. Naomba kidogo akaangalie tena, ningeomba bora amchukuwe fundi akaangalie. Unajua kutoa picha kama hiyo kidogo haipendezi yeye ni mwakilishi ni mtu mkubwa sana. Unaposema gari inavuja *diesel* kwa kweli inaonekana kama sote hatufanyi kazi zetu ipasavyo, sio sahihi. Gari inavuja maji na yale maji ni ya AC. Naomba Mhe. Makame Mshimba, nadhani yuko nje maana yeka ananisikia bora akaangalie gari ile inavyofanyakazi. Gari ni nzima na iko sawa na inachekiwa kila siku, na vyombo vya usalama wenyewe wanahakikisha kwamba gari ile inafanyakazi na iko kwenye hali nzuri.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui tunakushukuru sana, ulishauri utekelezaji wa sera na sheria ya utumishi wa umma uanze kwa mwaka fedha 2010/11. Tunashukuru. Nafikiri tumesema kwamba utekelezaji wa hayo mambo tunajiandaa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman, ametoa ushauri juu ya kuwekwa uzito katika maeneo ya uvuvi wa bahari kuu na uhandisi. Maeneo hayo kwa kweli ni muhimu sana na ushauri wake juu ya hayo tutaufanyiakazi.

Mhe. Hija Hassan Hija, yeye amegusia zaidi ushirikiano wa kikanda na kwa namna gani Zanzibar watafaidika na uhusiano huo? Nafikiri nimejitahidi sana kulijibu suala hili kwa waheshimiwa wengine. Kwa hivyo, Mhe. Hija Hassan atakubaliana na majibu ambayo nimekwishayatoa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, yeye ameonesha huruma zake kwa wastaafu wa Idara ya Majenzi. Kutokana na maelezo yake wastaafu hawa wanalipwa Shs.5,000/=. Suala hili bado linatupa utata, kwa hivyo namuomba Mhe. Mwanajuma atustahamilie kidogo tukalifanyie kazi vizuri. Kama nilivyosema kuna *category's* mbali mbali za wastaafu, wengine walikuwa *daily paid*, wengine walikuwa wa kudumu lakini kwa misingi fulani. Kwa hivyo, nitamuomba na nitamfuata ili anipe undani zaidi kuhusu hili suala

hasa kwa mfanyakazi mmoja au wawili aliozungumza nao, ili tulifuatilie na tuone vipi tunaweza kurekebisha kama kuna matatizo au kama ndio hicho anachostahiki iwe ndio hicho.
Mhe. Mwenyekiti, inaonekana kweli ni kidogo kwa wakati. Lakini kama nilivyosema tunajitahidi kuboresha au kuendeleza kadiri tunavyokwenda.

Mhe. Mwanajuma vile vile alitaka kujua wataalamu walivyofanya upekuzi, je ni wafanyakazi wangapi wamebainika na makosa? Naomba kumjulisha Mhe. Mwanajuma kwamba ni wafanyakazi wanne tu ndio waliobainika na makosa ya kughushi vyeti vya masomo. Kwa kweli hili limekuwa ni tatizo na vijana wamekuwa wajanja sana siku hizi, kujituma wengine hawataki, wanataka kughushi matokeo yale ili waweze kupata kazi. Kwa hivyo, ningewaomba waheshimiwa tusaidiane sana kwa hili tulipige vita sana. Nakumbuka sote humu tuliposoma katika wakati wetu haya hayakuwepo, kwa nini leo yawepo kwa vijana wetu. Kwa hivyo, nawaombeni sana tusaidiane tulipige vita kabisa suala la kughushi vyetu.

Vile vile Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi alitaka kujua kati ya wafanyakazi 19 Unguja na Pemba waliofanyiwa uchunguzi wa HIV /AIDS ni wafanyakazi wangapi waligundulika kuathiriwa na virusi vya UKIMWI ?

Mhe. Mwenyekiti, nina furaha kumjulisha Mhe. Mwanajuma kwamba wafanyakazi wote waliohusika na zoezi hili wameonekana kuwa salama, yaani HIV *negative*. Labda nitowe takwimu kwa ufupi tu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa wanawake kwa Unguja walifanyiwa 75 na wanaume 78 kwa ujumla ni 153. Kwa Pemba wanawake waliofanyiwa 18 na wanaume 26 jumla 44. Kwa hivyo jumla ya wanawake waliofanyiwa ni 93 na jumla ya wanaume waliofanyiwa ni 104. Kwa hivyo, jumla kuu kwa Unguja na Pemba waliofanyiwa wote ni 197 na wote wameonekana wako salama, tunashukuru *Alhamdulillah.*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohamed Ali Salim aliuliza juu ya mageuzi ya utumishi wa umma. Suala hili nafikiri nimeshalijibu. Alinukuu kwenye kifungu cha Fungu 10 cha jadweli kwenye ukurasa wa 68, Afisi ya Rais Ikulu mbona patupu au kompyuta imeruka. Nataka kumwambia tu kuwa kompyuta haikuruka. Ukiangalia jadweli kwanza kuna fungu 8 Afisi ya Baraza la Mapinduzi, sasa ule mstari wa mbele wote ulikuwa patupu kuonesha *subtitle* hii ambayo ina *sub items* mbili. Mpango wa marekebisho ya utumishi wa umma na ujenzi wa chuo. Halafu chini fungu 10 Afisi ya Rais Ikulu nalo mradi wake uliopo ni mradi wa kuimarisha mawasiliano Ikulu. Hii ni miradi ya maendeleo, kwa hivyo pale hakuruka ni sawa sawa kwa kweli.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohamed Ali Salim pia aliulizia kuhusu ujenzi wa Ikulu ya Mkoani. Mhe. Mwenyekiti, jengo hili tunategemea kulishughulikia katika mwaka wa fedha 2010/11 kama nilivyosema na kuhusu ujenzi wa Afisi ya Afisa Mdhamini katika eneo lile ambalo afisi ipo. Tunakubaliana na ushauri huo na waheshimiwa wengi wamezungumza kwamba ni vyema tukajenga pale pale. Kwa kweli ushauri waliotupatia tunauchukua na tumeona ni kweli kujenga pale ni vyema. Kwa hivyo tutatafuta afisi kwa muda ili pale lile jengo tuvunje halafu tujenge pale pale afisi iwe ni pale pale eneo lake ni zuri. Ushauri tuliopewa tunashukuru tunauchukua na tutaufanyia kazi.

Aidha, tunapokea ushauri juu ya kuimarisha taarifa za watumishi wa umma ili kuepuka malalamiko wakati wa marekebisho ya mishahara. Kweli tulikuwa huko nyuma tuna matatizo makubwa ya *debase*, ma- *file* yale yanapotea, lakini sasa kutokana na mambo haya ya teknolojia ya kompyuta nafikiri tunakwenda vizuri na tutajitahidi kuweka mambo vizuri.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis, na yeye tunamshukuru alitaka kujua kwa nini *Rest House* ya Micheweni haijamaliza kujengwa. Ni kweli nakubali kwamba *Rest House* ile haijamalizika kujengwa. Lakini nataka kumjulisha Mhe. Bihindi kwamba ujenzi ule haiko katika Idara ya Huduma za Rais. *Rest House* ile ujenzi wake uko chini ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, kwa kupitia Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi ule ulipata matatizo kutoka na yule *contractor* hasa mwenyewe alitangulia mbele ya haki, kwa kweli hali kuwa na matatizo na kampuni. Yeye alikuwa analichukua lile suala kama lake mwenyewe binafsi. Kwa hivyo, alipofariki mambo yote tena kafa nayo, kwa hivyo kulikuwa na matatizo sana katika mawasiliano hasa ya kifedha, kati yake na kampuni yake pia na serikali. Sasa imekuwa tunazungumza na watu ambao walikuwa hawashughuliki na ule ujenzi. Kwa hivyo, tulikuwa na matatizo makubwa sana, lakini tunaamini tutafikia mahala. Hicho hasa ndio kiini cha matatizo kilichokumba ujenzi ule.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abass Juma Muhunzi, tunamshukuru sana kwa falsafa zake kama kawaida, hasa juu ya ushauri wa uanzishwaji wa mfuko wa wastaafishaji. Pia kuhusu suala la kutenganisha Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Mipango. Mhe. Mwenyekiti, masuala ya Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Mipango, mara nyingi yanakuwa pamoja au yanatengwa, inategemea na ule ukubwa wa serikali na Rais mwenyewe anavyotaka na anavyoona.

Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti, hata Tanzania Bara siku hizi wanayo Wizara ya Mipango lakini utakuta haina waziri, Tume ya Mipango lakini mambo ya

mipango yote yako chini ya Waziri Mkuu. Ndio maana wizara ile inaitwa Wizara ya Fedha na Mipango. Nakumbuka Waziri Mkuu leo alisoma *speech* mbili. Asubuhi alisoma hotuba ya mipango na jioni akasoma hotuba ya makadirio ya fedha. Mimi sasa ndio nikachanganya pamoja yote hayo. Kwa kweli hiyo ni mipango ya serikali, lakini ushauri wake tumeusikia.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abass Juma Muhunzi, pia alitoa ushauri kwenye suala la Spika na Naibu Spika. Alishauri kuwa Naibu Spika na yeye afuate mkondo wa Spika. Mimi nafikiri hili tusome kanuni zikoje na zimeelekeza vizuri tu, Naibu Spika uchaguzi wake ukoje na Spika uchaguzi wake ukoje. Lakini ushauri alioutoa basi nafikiri Baraza tumesikia na tutauzingatia tena katika marekebisho yetu ya kanuni kwa siku za mbele.

Mhe. Ali Abdalla Ali, aliuliza suala zima la ujenzi katika eneo la Chuini. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Hamza kwa ufafanuzi wa majenzi mengi ya serikali katika *section* mbali mbali. Kwa mfano Chukwani, Mazizini, Tunguu na Chake Chake haya majenzi mapya kwa kweli inaonesha wazi vipi serikali yetu imejitanua katika harakati zake. Mji Mkongwe pale pamekuwa hapatoshi ni lazima tutoke nje, lakini na hayo maeneo ambayo tumekimbilia, mfano Mazizini tumeamua kupakata pameshajaa. Kwa hivyo, ipo haja labda na Chuini tutarudi nako sio mbali, kwa hivyo hatu-*roll out* ile programu ya Chuini imekufa, hapana. Bado serikali inalidhibiti lile suala na *Inshaallah* pengine huko mbele tutakuja kulizingatia. Hatusemi kwamba tumeshaacha ile *idea* moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, mwanzo ilikuwa labda tujenge makao makuu ya serikali nzima pale. Sasa kutokana na mawazo hayo kupitwa na wakati, kwa hivyo tumejenga afisi mbali mbali kama Mhe Hamza Hassan alivyosema. Lakini bado eneo la Chuini ni la serikali na tutajitahidi kuzingatia nini tufanye katika ujenzi wa afisi za serikali huko mbele.

Mhe. Ali Abdalla Ali, alizungumzia suala zima la ZSSF. Alishauri kwamba mafao ya ZSSF yatoke kabla mtumishi hajatimiza miaka 60. Ushauri huo waheshimiwa mara nyingi tumekuwa tukiutoa, lakini siku zote tunasisitiza kwamba lengo la mafao ya ZSSF ni kumnufaisha mfanyakazi baada ya kustaafu yaani baada ya miaka 60, ile akiba yake inayoiweka basi ije imsaidie. Kama kuna matatizo katika uajiri akawacha ajira kabla ya miaka 60 basi zile pesa zake zipo, atafute ajira nyengine pale ataendelea. Lakini kwa kweli kumpa kabla ya miaka 60 kidogo ni tatizo, itakuwa lile lengo letu tulililoliweka halijafikiwa. Lengo letu ni kumsaidia yeye anapostaafu. Kwa hivyo, muhimu kama ana matatizo kwengine basi bado hajafikia miaka 60 aombe ajira kwengine, achacharike aje aongezee pale alipoachia. Haya mambo kwa kweli ni makubwa na ni mazito.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kitengo chetu cha ZSSF wako wanatafakari kwa undani zaidi *concept* hii vipi labda kama tunaweza kuitoa. Lakini kwa sasa maelezo niliyokuwa nataka kuyatoa ni hayo tu kwamba hapana kanuni haziruhusu hivyo, mpaka hapo labda baadae tutakapokuja na mtizamo mpya.

Mhe. Abdallah Juma, ametutanabahisha juu ya ufinyu wa bajeti kwa ajili ya mradi wa ukarabati wa Ikulu na ujenzi wa nyumba za serikali. Naomba kumjibu Mhe. Abdalla Juma kwamba mradi huu ni mradi wa miaka mitano ambao umeanza mwaka wa fedha 2009/2010 hadi mwaka 2013/2014. Utekelezaji wa maradi huu unakwenda kwa awamu pamoja na kipaumbele kilichowekwa kwa kila mwaka. Tunakwenda kidogo kidogo kwa mujibu wa hali ya fedha, hatuchukui yote kwa mpigo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin, na yeye tunamshukuru kwa ushauri wake juu ya ujenzi wa Ikulu ya Mhe. Rais jijini Dar es Salaam. Aidha, tunamshukuru kwa ushauri wake, lakini kwa sasa hivi nyumba iliopo Laiboni kama alivyosema mwenyewe, tunakubaliana naye kwamba inakidhi haja.

Kuhusu ushauri wake juu ya nyongeza za mishahara, utunzaji wa wazee na miundo ya utumishi, tayari kama nilivyokwishasema nimeshayatolea maamuzi huko nyuma. Lakini nasema huu ni utaratibu ambao siku zote tunaendelea kuufanyiakazi.

Mhe. Juma Duni Haji, na yeye tunamshukuru sana kwa falsafa kubwa kama kawaida yake, yeye kweli ni mwalimu maana unapotoa *lecture* ile unakuwa ni mwalimu aliyebobea hasa na mwenye uzoefu mkubwa sana. Tunamshukuru sana kwa michango yake na ushauri wake. Pia alitushauri sana juu ya suala zima la upangaji wa wafanyakazi kwa mujibu wa taaluma zao. Tumesikia na wale wafanyakazi aliosema wako Idara ya Utumishi pale ambao zamani walikuwa makatibu wakuu, pia ushauri wake tumeusikia wa kuwapangia kazi tusiwaache tu pale wakakaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, tunamshukuru sana kwa ufafanuzi alioutoa juu ya masuala mbali mbali yakiwemo ujenzi wa barabara ya Chuo cha Utalii na kadhalika.

Mhe. Ame Mati Wadi, na yeye tunamshukuru kwa kuelimisha wananchi namna mbali mbali juu ya ushirikiano wa kikanda, na ushauri wake mwingi alioutoa wote tumeuchukua kama alivyosema pamoja na falsafa kubwa nayo tutaifanyia kazi.

Mhe. Bi Zainabu Moh'd vile vile tunamshukuru kwa michango yake na ushauri alioutoa. Mwisho nimshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye ni Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, kwa michango yake na lile suala lake la barabara ambalo alisema tulifanyie kazi. Suala hili tutasaidiana yeye ni waziri na ni mwakilishi, kwa hivyo hatutomuangusha tutajitahidi kufanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa michango ya maandishi kulikuwa na michango ya Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, tunamshukuru sana kwa upande wake. Aliuliza kuhusu suala la uajiri, alisema ni vizuri tukaelezwa ni wanawake wangapi walioajiriwa katika sekta iliyorasmi? Nakiri kwamba ni kweli hatukuonesha kwenye ukurasa wa 64, nafikiri tutajitahidi huko mbele kupambanua ni wanawake wangapi na wanaume ni wangapi. Hizi ni *figures* inabidi zitafutwe tu. Alitushauri zaidi kwenye Idara ya Uratibu wa Uchumi na Uhusiano wa Kimataifa kwamba mwezi Julai tunategemea kutia saini soko la pamoja. Je, mbona sisi tuko kimpya, Marais wenzetu huko wanazungumza, wanawaambia wananchi wao na wanawatayarisha.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hatukukaa kimpya na sisi tunawaelimisha watu wetu. Hayo ndio maazimio yaliyotokea kwenye *business council* ya hivi majuzi. Kwa sababu *business council* ya hivi majuzi ili-*attribute* suala zima la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kwa kweli tunashukuru michango ya wafanyabiashara ilikuwa mingi. Wengine pale pale walisema hata hiyo *common market* hatuna habari kabisa ndio kwanza tunasikia leo hapa. Tukaona kumbe kweli iko haja ya changamoto, juu ya suala zima la taaluma kwa wafanyabiashara wetu na wananchi wetu ni lazima tukaze kamba ili tuwaelimishe ipasavyo.

Kwa hivyo nakubaliana na yeye kwamba tutachukua jitihada tukisaidiana na wizara husika ili tuone kwamba suala zima la ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na kanda nyengine basi wananchi wetu wanahusishwa, wanafahamishwa na wasaidiwe ili na sisi tuweze kusimama Zanzibar kama nchi katika suala zima la biashara na uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nakushukuru sana kwa kunipa wasaa huu wa kufanya michango na majumuisho katika michango ya waheshimiwa. Kama nilivyosema kama sikutaja jambo fulani la mheshimiwa naomba wachukulie kwamba ni kutokana na muda, tumejitahidi kwa kushirikiana na wenzangu kuchambua kadiri hali ilivyoruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 07 - AFISI YA RAIS URATIBU WA UCHUMI NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

Kifungu 06 - Uratibu wa Uchumi na Ushirikiano wa Kimataifa 651,000,000/-

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 08 - AFISI YA RAIS BARAZA LA MAPINDUZI

Kifungu 05	-	Baraza la Mapinduzi	534,908,000/-
Kifungu 10	-	Tume ya Utumishi Serikalini Unguja	166,034,000/-
Kifungu 11	-	Idara ya Utumishi Serikalini	171,668,000/-
Kifungu 13	-	Chuo cha Utawala wa Umma	145,390,000/-
		Jumla ya Fungu	**1,018,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 10 - AFISI YA RAIS IKULU

Kifungu 03	-	Afisi Kuu Pemba	199,207,000/-
Kifungu 04	-	Idara ya Mipango na Sera	

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri lakini kuna kitu ambacho nataka anifahamishe kuhusiana na fungu hili. Kwa kweli nilihoji kwamba wamenunua gari tatu aina ya *Land cruiser*, pia nilisema kwamba Afisi ya Rais inakabiliwa na matatizo ya usafiri kwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, nilitaja nijue gari hizo zimepelekwa wapi, yaani Unguja au Pemba.
Vile vile kwa sababu ya kupanua demokrasia mawasiliano na Rais sasa tuyafanye moja kwa moja, ili Wazanzibari wapate kuzungumza na Rais kupitia vyombo vya habari, ambapo sikupatiwa majibu *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Baraza la Mapinduzi Ikulu: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Mjumbe aliuliza maswali hayo mawili. Kuhusiana na suala la gari, hivi majuzi tulipopata gari tatu tumezigawa, moja tumeipeleka Pemba, moja imebaki Unguja na nyengine tumeipeleka Dar-es-Salaam *(Makofi)*.

Kuhusu suala la mawasiliano ya moja kwa moja na Mhe. Rais. Kwa kweli wazo hilo ni zuri, basi awamu ijayo Afisi ya Rais itaandaa utaratibu mzuri *(Makofi)*.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, namuombea Mhe. Waziri ashinde, tuendelee *(Makofi)*.

Kifungu 04	-	Idara ya Mipango na Sera	436,263,000/-
Kifungu 07	-	Huduma za Rais Unguja	1,035,968,000/-
Kifungu 16	-	Kitengo cha Afisi ya Usalama wa SMZ	29,858,000/-
Kifungu 18	-	Kitengo cha Mawasiliano na Habari	39,704,000/-
		Jumla ya Fungu	**1,741,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 08 – AFISI YA RAIS BARAZA LA MAPINDUZI

Kifungu 05	-	Baraza la Mapinduzi	1,250,000,000/-
		Jumla ya Fungu	**1,250,000,000/-**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 10 - AFISI RAIS IKULU

Kifungu 04	Idara ya Mipango na Sera	1,500,000,000/-
	Jumla ya Fungu	**1,500,000,000/-**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Baraza la Mapinduzi Ikulu: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa wizara yangu bila ya mabadiliko yoyote. Sasa naomba kutoa hoja makisio hayo Baraza iyakubali.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi)*.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, mimi ndiye Kaimu Waziri wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Kwa hivyo, naomba kwa sababu mwenyewe waziri mhusika atakuwepo jioni na atajiandaa vizuri kwa ajili ya kuweza kuwasilisha vizuri.

Kutokana na hali hiyo naomba Baraza lako tukufu liahirishwe mpaka jioni, ili tumpe nafasi mwenyewe Mhe. Waziri mhusika atakuwepo *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tatizo limetokea asubuhi wakati wa kuwasilisha hati mezani, ambapo Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira ndiye aliyewasilisha na ameleta hapa karatasi kwamba amepata dharura. Kwa hivyo, tutaisikilisa kauli yako hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa shughuli zetu tulizozipanga hivi sasa zimemaliza pamoja na Mhe. Waziri mhusika ambaye atakuja kusoma hii Taarifa inayohusu Haki za Watoto atakuwepo jioni mwenyewe.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako tuahirishe kikao hiki mpaka saa 11:00 jioni. Naomba kutoa hoja *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi)*.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, ahsanteni sana kwa kunipa mashirikiano ya hali ya juu katika kikao hiki cha asubuhi. Kwa hivyo, ninakuombeni kikao hiki nikiahirishe mpaka saa 11:00 jioni.

(Saa 5:40 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

KAULI ZA MAWAZIRI

Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Watoto katika kilele cha siku ya Mtoto wa Afrika tarehe 16 Juni, 2010-06-21

Mhe. Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote tunamshukuru M/Mungu kutujaalia kutukutanisha hapa katika hali ya uzima pia tunakushukuru kwa kupata nafasi hii ya wewe ndugu yangu kuwa mwenyekiti wangu kwa mara ya kwanza nakupongeza sana na Mungu atazidi kukufungulia.

Mhe. Mwenyekiti, inakumbukwa kwamba kila ifikapo tarehe 16 Juni ya kila mwaka ni siku ya mtoto wa Afrika. Siku hii maalumu inaadhimishwa kuwakumbuka watoto wasio na hatia waliouwawa na askari wa Makaburu katika kitongoji cha Soweto nchini Afrika ya Kusini. Mauaji hayo ya kinyama yalitokea wakati wanafunzi walipoandamana kupinga amri ya Serikali ya Kikaburu ya kutaka lugha ya kikaburu kuwa lugha rasmi ya Afrika ya Kusini kwa lengo la kuwatawala zaidi wazalendo wa nchi hiyo.

Kitendo hicho cha watoto kupinga ukoloni na ukandamizaji wa waafrika kilikuwa ni hatua ya kishupavu na kishujaa. Jambo hili ndilo lililoifanya siku hii kuwa ni ishara ya kuwakumbuka watoto hao wakombozi wa Afrika.

Mhe. Mwenyekiti,Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto huadhimisha siku hii kwa kufanya shughuli mbalimbali ambapo shughuli Kubwa ni ya kukusanya taarifa kutoka katika sekta mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali zinazoshughulikia watoto, kuzichambua, kuzitathmini na kuziwasilisha katika baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia na kutia saini Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto mwezi Septemba 1990 wenye lengo la kutoa msukumo katika kuinua haki za watoto ulimwenguni kote. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto imeweka mazingira mazuri kwa kuanzisha Sera ya Uhai.

Hifadhi na Maendeleo ya Mtoto na kutekeleza mpango wa Uhai, Hifadhi na maendeleo ya Mtoto unaoratibiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi kwa mashirikiano na Shirika la kuhudumia Watoto *UNICEF*. Mpango huo ni kuinua na kuimarisha hali za mama na mtoto kwa mtazamo wa maeneo manne makuu kama ilivyoainishwa ndani ya Mkataba huo.Maeneo hayo ni: Haki ya Kuishi, Kuendelezwa, kulindwa na Haki ya Kushiriki na Kushirikishwa katika masuala yanayowahusu katika jamii.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kipindi hiki Jumla ya maafisa afya 67 walifundishwa juu ya uangalizi na ufuatiliaji wa chumvi yenye madini joto kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo, bandarini, madukani, maghalani na sokoni. Mafunzo hayo yaliendeshwa Unguja na Pemba

Mhe. Mwenyekiti, Utoaji wa matone ya vitamini A na dawa za minyoo kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano bado unaendelea katika Wilaya zote za Unguja na Pemba, katika zoezi hilo la mwezi Januari 2010, jumla ya watoto 198,607 walipatiwa matone ya Vitamin A. kati 207,582 sawa na 95.7%.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji iliahidi kutekeleza miradi 14 pamoja na miradi mingine itakayoanzishwa kwa juhudi za wananchi na kubahatika kupata ufadhili. Jumla ya miradi 12 imetekelezwa na 2 haikutekelezwa kutokana na kutoingiziwa fedha. Aidha miradi mingine 5 ambayo iliibuliwa na wananchi pia ilitekelezwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii

Mhe. Mwenyekiti, Idadi ya skuli za Maandalizi zimefikia 261, kati ya hizo za serikali ni 32, na za binafsi ni 229. Skuli za maandalizi za serikali zina jumla ya wanafunzi 4,476 kati yao wanawake ni 2,290 na wanaume 2,186. Skuli za binafsi zina jumla ya wanafunzi 16,742, kati yao wanawake ni 8,563, na wanaume ni 8,179. Idadi hiyo inafanya wanafunzi wote walioko

katika ngazi hii kuwa ni 21,218, ambayo ni sawa na asilimia 17.8 ya watoto wenye umri wa miaka 4 – 6 wanaostahiki kuwepo katika ngazi hii ya elimu

Mhe. Mwenyekiti, Mwaka 2010, idadi ya wanafunzi walioandikishwa na kupatiwa nafasi darasa la kwanza ni 31,092, ikilinganishwa na watoto 30,012 walioandikikshwa mwaka 2009 .Wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi yaani darasa la saba (7) mwaka 2009, ambao walifanya mtihani wa Taifa walikuwa 22,179, wanawake walikuwa 11,707, na wanaume 10,472. Waliofaulu mtihani ni 18,812 sawa na asilimia 84.8, ikilinganishwa na asilimia 84.6 ya mwaka 2008.

Hii inaonesha ongezeko la kufaulu kwa mwaka 2009. Kutokana Sera ya elimu ya mwaka 2006, wanafunzi 22,179 wameendelea na elimu ya kidato cha kwanza.Aidha wanafunzi wapatao 788, ambao wamefaulu vizuri zaidi mitihani yao ya darasa la saba wamechaguliwa kuingia skuli za michepuo kwa fani tofauti katika skuli mbali mbali Unguja na Pemba. Jadweli na.9 linatoa maelezo zaidi

Mhe. Mwenyekiti, Jumla ya walimu 730, wamepewa mafunzo ya elimu mjumuisho mwaka 2009/2010. Mafunzo hayo yalihusisha mada kama vile lugha ya alama, dhana ya elimu mjumuisho, njia na mbinu za kufundishia katika darasa la mjumuisho, jinsi ya kumtambua na kumsaidia mwanafunzi mwenye kifafa. Idadi ya walimu nayo pia imeongezeka kutoka 2255 hadi kufikia 2290

Mhe. Mwenyekiti, Vijana wetu wenye umri wa miaka 13 na kuendelea ambao waliacha masomo yao njiani kutokana na sababu mbali mbali, wanaendelea kupatiwa huduma kupitia ngazi hii ya elimu. Kwa mwaka 2010, Vituo vya Elimu Mbadala vimeongezeka kutoka vituo 29 vya mwaka 2009, hadi kufikia vituo 49, Unguja na Pemba. Idadi ya wanafunzi nayo imeongezeka kutoka 863 mwaka 2009, na kufikia 1566, kati yao wanawke ni 187 na wanaume 1379, hadi mwezi Mei 2010

Mhe. Mwenyekiti, Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo hadi kufikia Mei 2010, kina jumla ya wanafunzi 347, wakiwemo wanawake 107 na wanaume 240, badala ya 327, wakiwemo wanawake 97 na wanaume 230 waliosajiliwa mwaka 2009.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Tume ya Ukimwi ya Zanzibar *ZAC* iliendesha kampeni maalum ya kuwalinda wanafunzi dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia na maambukizi ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi.

Kampeni hiyo ilijumuisha skuli 20, zikiwemo skuli 2 katika kila wilaya za Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ustawi wa Jamii hutoa msaada wa maziwa kwa kinamama wanaojifungua watoto zaidi ya wawili kwa mimba moja na wote wakiwa hai, akina mama hao hupatiwa msaada wa shilingi 15,000/= kwa mwezi kwa kipindi cha miaka miwili. Kwa mwaka huu kinamama 11 kutoka katika Wilaya tofauti wamepatiwa msaada huo.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ustawi wa Jamii imeanzisha kitengo cha hifadhi ya mtoto mnamo mwezi Novemba 2009 na kuzinduliwa rasmi tarehe 17/2/2010**.** Kazi kuu za kitengo ni kushughulikia kesi zote za udhalilishwaji wa watoto hapa Zanzibar kwa kufuatilia matukio hayo katika maeneo mbalimbali ikiwemo Polisi na kutoa ushauri nasaha kwa waathirika wa vitendo vya udhalilishwaji.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya wanawake na watoto imepokea malalamiko yapatayo 201 waliotendewa watoto yakiwemo kutelekezwa, mvutano wa malezi, ujauzito, kutoroshwa, kufukuzwa na kudhalilishwa. Malalamiko haya huchambuliwa baada ya kusikilizwa wahusika na baadae hupelekwa taasisi husika (Polisi, Hospitali, Mahkama ya Kadhi, Kanisani au Mahakama za Wilaya na Mikoa).

Mhe. Mwenyekiti, Kwa upande wa asasi zisizo za kiserikali *ILO* kupitia *IPEC/TBP* iliziwezesha asasi mbili *COWPZ* kwa Unguja na *PIRO* kwa Pemba, kuwatoa watoto 2400 katika ajira. Watoto 1400 walitoka katika Wilaya ya Micheweni kweye shehia ya Tumbe, Maziwa ng'ombe na Shumba Mjini.Kwa Unguja *COWPZ* iliwatoa watoto 1000 katika Wilaya ya Kaskazini "A" Shehia ya Nungwi, Mkokotoni, Matemwe na Pwani Mchangani

Mhe. Mwenyekiti, Jumla ya mabaraza 10 ya Wilaya yameundwa Zanzibar, kati ya mabaraza hayo Unguja 6 na Pemba 4. Madhumuni ya kuundwa mabaraza haya ni kuhamasisha na kuwashirikisha watoto katika masuala ya kijamii kwa kutoa mawazo, maoni na matatizo yao vilevile kunawezesha watoto kujiamini.

Mhe. Mwenyekiti, Jumla ya watoto 37 wa Zanzibar, Unguja 22 Pemba 15 walipatiwa mafunzo ya kujua Haki na Wajibu wao ambapo pia wameshirikishwa na kutoa maoni yao katika uandishi wa ripoti hii ya mtoto. Maoni yaliyotolewa na watoto yamejumuisha haki na wajibu wa watoto, wazazi/walezi na jamii na taasisi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya kutoa taarifa ya Sekta naomba nichukue nafasi hii nitoe taarifa iliyoandaliwa na watoto na kuwasilisha Maoni ya watoto

Mhe. Mwenyekiti, mwaka huu Wizara imeweza kutekeleza kifungu cha mkataba kuhusu kushirikisha watoto katika kuandaa ripoti yao kwa kutoa mawazo katika utaratibu mzima wa maendeleo yao. Katika ripoti yao watoto wameweza kueleza umuhimu wa kuwa na mabaraza ya watoto pamoja na mafanikio yao.

Mhe. Mwenyekiti, Watoto wametoa mapendekezo yao kwa serikali ili kuyafanyia kazi ili kuhakikisha watoto wanaendesha maisha ya kila situ, kwa upande wa afya wamependekeza wahudumu wa afya wapewe mafunzo zaidi na kuboresha huduma hospitalini.

Mhe. Mwenyekiti, suala la wa ulinzi, watoto wamependekeza Serikali kufuatilia na kuchukua hatua kali za kisheria kwa wanaodhalilisha watoto na wanaozorotesha kesi za watoto pamoja na kutoa elimu kwa wazazi na jamii juu ya Haki na ya ulinzi baada ya wazazi kutoa lawama.
Mhe. Mwenyekiti, Watoto wameiomba Serikali kuanzisha kwa makusudi sehemu maalum ya kuwapa watoto ushauri nasaha kwa watoto wenye matatizo mbalimbali.

Mhe. Mwenyekiti, katika maoni ya watoto kwenye sekta ya Elimu wameiomba serikali kuweka miundo mbinu bora kwa watoto wenye ulemavu kuanzia barabarani, hospitalini na maskuli, vilevile huduma ya maji maskulini iongezwe kukidhi haja ya watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Suala la michezo maskulini kwa watoto limekuwa linawakereketa watoto hivyo wanaiomba serikali kurudisha michezo maskulini na kushindana ili waweze kujenga afya zao.

Mhe. Spika Watoto kwa maoni yao wanaziomba mahakama zisimamie vyema kesi zinazowahusu na kujenga mazingira mazuri pindipo watakuwa na hatia au kudhulumiwa. Watoto wanaiomba serikali kutoa adhabu kali kwa wale wote wanaokiuka sheria.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza wale wote wanaozisimamia na kutekeleza Haki za watoto, nikianzia kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Amani Abeid Karume kwa kujali watoto wa Zanzíbar na kuweka mazingira bora kwa jamii ili watoto wapate haki zao, watendaji wa sekta zote za serikali na zisizo za serikali, washirika wa maendeleo ikiwemo *UNICEF, SAVE THE CHILDREN, ILO, na UNDP* pamija na Mabaza ya watoto Zanzíbar,

Mhe. Mwenyekiti, kwa kusema haya naomba kuwasilisha.

Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak: (Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Kazi Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Mwenyekiti, natanguliza maelezo haya ya Kambi ya upinzani katika Baraza hili tukufu, kwa kumshukuru Alla ambae ndie aliyetuwezesha jioni hii kukutana hapa na tukazungumza haya tunayoyasema hivi sasa, mambo yote yamo ndani ya mipango yake pasina na kushirikiana yoyote katika kuipanga.

Mhe. Mwenyekiti namuomba Mwenyezi Mungu mtukufu aniwezeshe kutoa maelezo haya machache kwa salama na amani na utulivu wa moyo, baada ya hapo naomba kutoa shukurani zangu kwako wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kuniruhusu nitoe maoni haya katika Baraza lako hili tukufu. Ni matumaini yangu kwamba wajumbe wa baraza hili watanisikiliza kwa makini na utulivu.

Mhe. Mwenyekiti siku ya tarehe 16 Jun ya kila mwaka ni siku ya maadhimisho ya mtoto wa kiafrika juu ya utekelezaji wa mkataba wa haki za watoto tokea mwaka 1990, kwa kuhakikisha taarifa ya maendeleo ya watoto wa Zanzibar chini ya mkataba na vipengele vyake vinavyotekelezwa kulingana na sera, uhai, hifadhi na maendeleo ya mtoto pamoja na mkataba wa kuondoa umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, sera na mpango huo umezingatia maeneo makuu manne kama yafuatayo:-

1. Haki ya kuishi
2. Haki ya kuendelezwa
3. Haki ya kulindwa
4. Haki ya kushiriki na kushirikishwa

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mambo hayo ambayo ndio msingi mkuu wa kutetea na kulinda haki ya Mtoto wa Kizanzibar, ambayo ni sehemu ya mtoto wa kiafrika kambi yetu inapendekeza kuwa serikali ichukue hatua madhubuti ambazo zitahakikisha kuwa watoto wetu wanaandaliwa mazingira bora ya kisera na kisheria kwa taasisi zote zinazohusika moja kwa moja katika kuwakuza.

Kuendeleza na Kuwalinda Watoto Wetu

Mhe. Mwenyekiti, tabia inayojitokeza ndani ya jamii yetu ya kuwatumikisha na kuwakatisha masomo watoto wetu haikubaliki, tabia ya baadhi ya wazazi kuwatumilia watoto hao kama ngao ya kuombea majiani haikubaliki na inadhalilisha watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, tabia ya kuwakatisha masomo watoto na kuwapa waume nayo haikubaliki, kwa mambo haya na mengi mengineyo ambayo yanaendelea kufanyiwa watoto wetu yanakwenda kinyume na haki hizo na niwakati sasa kwa serikali kuyatolea msimamo endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, tabia ya waoto wetu wanapokwenda Skuli au kurudi na kukaa barabarani kuomba msaada wa magari hupelekea vitendo vinavyosababisha watoto wetu kuambukizwa virusi vya ukimwi, kambi yetu ya upinzani inaomba serikali ihakikishe kuwa inasimamia ile nauli ya wanafunzi iliyowekwa ili kuepushwa kunyanyaswa na makonda wa daladala.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuhitimisha maelezo haya kambi yetu ya upinzani napenda kuchukua nafasi hii adhimu na ni adimu na kuwashukuru wazazi na walezi wa watoto, kwa juhudi kubwa wanazozichukua katika kuwalea watoto wa nchi hii. Namuomba Allah awazidishie uwezo na awape subra katika kazi hiyo ulezi.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunivumilia muda wako niliotoa maelezo haya na namumboa Allah atuzidishie kuwalea watoto wetu kama ilivyoagizwa, na anavyopenda Mwenyezi Mungu ili tupate taifa zuri hapo baadae. Ami

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwanza kabisa na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuuliza masuala machache juu ya taarifa iliyowasilishwa hapa na Mhe. Waziri juu ya haki za watoto, katika kilele cha siku ya watoto Afrika tarehe 16 Juni, 2010.

Mhe. Mwenyekiti katika kitabu hiki Mhe. Waziri ametueleza mengi ya mafanikio na matatizo juu ya watoto wetu, lakini pia kuna mambo ambayo kayataja mazuri lakini kuna mengine yamezidi zaidi juu ya haki ya mtoto ambayo kwa asilimia mia moja inataka kulindwa na kusaidiwa.

Mhe. Mwenyekiti katika kuitetea haki ya mtoto. Hivi sasa kuna manung'uniko kwa baadhi ya taasisi za jamii kwamba inaletwa sheria ya haki ya mtoto na mama kama sikosei, lakini katika kutokuwa na taaluma sahihi au kutokana na semina walizofanyiwa hawakufahamu baadhi ya taasisi zetu hasa za kidini. Kuna maelezo makali juu ya athari ambayo naamini ikija sheria hiyo huenda ikaleta vurumai kidogo, namuomba Mhe. Waziri taasisi ya mashehe wa kiislam tuliokuwa nao Je, walifanyiwa semina wapi na semina hiyo ilizaa matunda gani ili tuelewe? Kama kuna taarifa hizo hapa hapa karibu tulipo wananchi wafahamu na sisi tufahamu ili kunusuru iyo sheria kuilinda.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mtoto anataka kusaidiwa kwa kila hali na katika taarifa hii ukurasa wa thalathini Mhe. Waziri katueleza kwamba Mswada wa watoto wanaolelewa na wazazi au walezi wasio na uwezo wa kuwatunza, katika jadweli yake ametwambia kwamba. Wilaya ya Mjini kuna wazazi kumi na mbili, Wilaya ya Magharibi kuna walezi wanne, Wilaya ya Kaskazini A zero, Wilaya ya Kaskazini B mmoja tu, Wilaya ya Kusini Unguja zero na Wilaya ya Kati zero. Je, Mhe. Waziri namuuliza walifanya utafiti gani juu ya kuhakikisha kwamba huko kote nilikokutaja hakuna watu ambao wanataka kusaidiwa kiasi hicho wanachosaidiwa hawa wengine?

Mwisho ili kuokoa muda labda Mhe. Waziri atuelimishe zaidi au atupe changamoto kwa kuwa watoto wetu wanapata shida sana mitaani na katika taarifa yake Mhe. Waziri kasema, kwamba kuna watoto wanategemea sana kupata msaada wa usafiri lakini mara nyingi huwa wanapata mateso badala ya kupata ile stahili yao. Mhe. Waziri ana mpango gani au kutoa wito gani yeye pamoja na Wizara zinazohusika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ili kuwapatia huduma hiyo rahisi wanafunzi wetu hawa hasa tukizingatia wale waliokuwa hawana uwezo? Ahsante.

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kutoa mawazo yangu mawili matatu na kuuliza swali moja.

Kwa sababu kila mmoja ni mzazi na mzazi anakumbuka majukumu yake ya watoto na ulezi ni kazi kwa mtu yoyote ambae kuwa amekaa na watoto, katika hii idara ya Mahakama ya watoto tangu mwaka tulioiwacha ripoti hii mpaka tarehe ya leo nataka Waziri anieleze ni kesi ngapi za watoto wakiwamo mayatima na wale walemavu ambazo amezipokea katika Wizara yake, na ngapi zimehukumiwa na ngapi hazijahukumiwa?

Lakini la pili nimpongeze Mhe. Waziri kuwathamini watoto kupatiwa haki zao za kimsingi katika Wizara ya Afya na mtoto kuzaliwa kupata cheti, lakini amechukua hatua gani za watoto walioko vijijini hasa tukilingania wale mayatima na walemavu, kwa sababu wengi wanaozaliwa na kufika umri wa miaka tano na sita wengine wengi hawana vyeti?

Je, Mhe. Waziri amechukua hatua gani kuwahamasisha wale na kupata haki hizi, kwa sababu kila tunavyokaa mabadiliko yanatokea watoto wale wanapokosa vyeti itakuja kuwa sakata kama sasa hivi tunavyotaka vitambulisho vya Wazanzibar kama mtu hana cheti hakipati?

Kwa hivyo Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri achukue juhudi za makusudi kuunda vitengo katika vijiji na kuahamasisha watu ili kupatiwa haki watoto walemavu na yatima walio katika vijiji kupatia vyeti.

Baada ya ushauri wangu huo naomba kukaa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuiuliza serikali. Mhe. Waziri namshukuru sana kwa ripoti yake aliyoiwasilisha punde hivi kwa kweli imetufunua macho katika mambo yetu ya kibinaadam, ripoti hii ingawa imewasilishwa na Mhe. Waziri lakini hii imejumlisha serikali nzima kwa hivyo mimi masuala nitakayouliza sio lazima ajibu yeye Mhe. Waziri lakini waziri yoyote inayemgusa basi ajibu.

Kwa sababu yeye amazungumzia kisekta huku la kwanza kwenye utangulizi, historia ya mtoto hasa imeanzia na vijana wetu wa Afrika ya Kusini kwa kuuliwa kinyama hapo ndio inapoanzia. Kwa hivyo kila mwaka sisi tunakumbuka na ulimwengu pia ulipata hisia juu ya kitendo hiki, lakini sasa suala langu lipo hapa Mhe. Mwenyekiti.

Suala la kuuawa kinyama lilikuwa Sekondari, lakini la mwanzo lilikuwa ni kupinga lugha ya kibepari ya kikaburu. Je, kutokana na hili sisi Wazanzibari au Tanzania juu ya hili tunaliona vipi tusikumbuke kuuawa tu lakini sababu ilikuwa ni kupinga na hili tatizo linatufika hata sisi Mhe. Mwenyekiti ndio asili ya kuuliza suala hilo.

Hapa bado vijana wetu wengi wanafeli kwa sababu hawajui kizungu, *biology, Chemistry* kizungu hisabati hivyo kwa miaka yote hiyo na Rais wa Zanzibar tangu alipotangaza lugha rasmi ni kiswahili kwa nini serikali yetu inashindwa kufanya utaratibu wa kutafsiri mambo ya kitaalamu hayo ili tukaweza kusomesha vijana wetu kwa lugha ya Kiswahili ambao wenzetu yaliyowafika hayo waliyapinga na sisi tusisahau kuna wakati wanaweza wakaja kufanya hivi hivi. Kufanya kosa sio kosa sisi tutakapokuja kuiga kama hivi tukirejea kosa ndio itakuwa kosa.

Mimi suala langu naiyuliza serikali

1) Je, juu ya hili makaburu tushaona wameuwawa kiasi hicho hata dunia nzima ikanguruma. Je, sisi katika lugha hizi za kigeni zinazofundishwa na ndio muhimu lakini vijana wetu wanafeli. Kwa nini serikali haijachukua hatua ya kutafsiri mambo ya taaluma yakafundishwa kwa lugha yetu?

Jengine Mheshimiwa katika ukurasa wa 4 namna ya kulisha mtoto na kuwekwa virutubisho, Vitamen “A” na mengineyo. Hii ni moja ya kusaidia lakini mbali ya kupewa vitamen “A” kuna mambo muhimu wakipewa watoto wetu bila ya kupewa haya matone nayo ni maziwa. Maziwa ni chakula chenye vitamen “A”

ya kutosha. Lakini hii ina matatizo kwa wananchi wetu kuipata ipasavyo. Kwanza maziwa yenyewe hayatutoshelezi.

2) Kwa nini hatujaweza kuzalisha maziwa ya kuweza kutosheleza wakapata watoto wetu.

3) Maziwa tuliyonayo ya ziada ni ya makopo bei yake kubwa. Sasa kwa sababu vitamen "A" ni muhimu kwa nini serikali haifanyi juu chini ikaweza kupunguza maziwa haya wakaweza kupewa watoto yakutosheleza kwa bei nafuu.

4) Jumuia za Kimataifa hata UNICEF zimeelekeza nchi za dunia kuwa maziwa ya mama ndio muhimu kwa watoto wanyonyeshwe na baadhi ya serikali zimeanza kufanya utaratibu wa mama wenye watoto ama kwenye serikali kupewa muda maalum wa kwenda kunyonyesha. Na hata hapa safari moja ilitolewa kauli hiyo, sasa hili linatekelezwa vipi angalau wafanyakazi wa serikali kupewa muda na wao wakaweza kwenda kumnyonyesha mtoto ili hiyo vitamen "A" baada ya kupewa matone aipate kutokana na mama yake.

Mheshimiwa eneo jengine katika ukurasa wa 10 mwengine kuhusu maji. Hili nalizungumza kuwa pamoja na miradi ambayo mamlaka ya maji ilisema itatekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 ilikuwemo na Jimbi. Jumbi ni sehemu moja ya Jimbo la Koani, katika utekelezaji hapa imeandikwa kazi ya kujenga mradi huo mpya bado hazijaanza.

Sasa niulize kweli mradi huu ulikuwepo kwa sababu katika vijiji vya jimbo la Koani sehemu ambayo haina njia yoyote ya mradi huu wa maji ni moja. Masuala mengi huwa nikiuliza kuhusu hapa najibiwa kama ifuatavyo. Nakumbuka mara ya kwanza nilijibiwa na nilikuwa mkali mpaka akaingilia Waziri Kiongozi, nikaambiwa mradi upo lakini mtandao wa maji utaanzia Kibondeni halafu utasambaza maji mpaka kijii cha Jumbi.

Mara ya pili nilimuuliza Waziri wa Maji mwenyewe akajibu kuna mradi mkubwa utafadhiliwa na nchi ya kiarabu lakini chanzo chake, tangi kubwa litakuwepo Binguni na maji hayo yatakuja Tunguu hadi Jumbi.

Mheshimiwa humu leo naambiwa kulikuwepo na mradi huo na kama haukutekelezwa kwa mpango wa mwaka huu.

5) Je, jumbi nayo itakuwemo katika kwenye huo mpango ili watu wapate maji. Kwa sababu kuna umuhimu mkubwa sasa hivi kwa Jumbi kupata maji kwa sababu mji unaelekea kule, Chuo Kikuu na kila kitu

kwa hivyo mahitaji ya maji yatakuwepo na chanzo chake bado hapana. Niiyulize serikali ni mapango gani ambao umeandaliwa kwa kijiji cha jumbi ambacho kitakuwa na mji mkubwa na taasisi kubwa ili ziweze kupata maji.

6) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kinga ya maleria, tunashukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada zake. Nawashukuru wafadhili wetu wakubwa Wamarekani, imesaidia mradi wa kupunguza maleria na ugawaji wa vyandarua. Lakini vyandarua vinavyotolewa vinakuwa baada ya miaka miwili au mitatu ndio huwa wanapata. Lakini baada ya miaka mitatu mahitaji kila siku yanazidi, leo watapewa watoto wa mwaka mmoja hadi miaka mine kuanzia leo lakini baadaye mwezi wa Agosti, Septemba, Oktoba, wengine watakuwa wamezaliwa kwa hivyo vyandarua hivi watakuwa hawavipati. Sasa je kuna mpango gani.

7) Lakini pia kwa wenzetu wa bara nasikia kuna hati punguzo kwa vyandarua bei Shs. 500/- unapewa chandarua cha kuweza kumsaidia mtoto. Je, hapa Mhe. Waziri amefanya utaratibu gani na sisi kupata vyandarua kwa njia ya hati punguzo. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nimuulize Mhe. Waziri maswali matatu kama ifuatavyo.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina utaratibu wa kuwapeleka watoto wanaosumbuliwa na maradhi ya moyo nchini Israil kwa ushirikiana na wafadhili wan chi hiyo. Lakini baadhi ya wakati watoto wengi hukosa nafasi hiyo kutokana na ufinyu wa fedha na kusababisha kupoteza maisha.

1) Je, wizara yako ili kumuokoa mtoto wa Zanzibar. Ina mpango gani wa kutenga fungu maalum ili kusaidiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili watoto wote wa Zanzibar wanaopata maradhi ya moyo waweze kupata fursa hiyo kwenda nchi ya Israil kwa matibabu.

2) Wizara ina mpango wa kuwasaidia wazee wanawake wanaojifungua watoto wawili kwa kuwasaidia msaada wa maziwa. Jimboni kangu hivi karibuni nimepata mzazi amejifungua watoto watatu wote wa kiume na kwa bahari mbaya hana maziwa ya kutosha. Nilitaka unifahamishe ni utaratibu gani wa kufuata ili mama yule na yeye aweze kupata msaada wa serikali.

3) Zanzibar lipo wimbi kubwa la watoto wenaozaliwa nje ya ndoa na wengine wazazi wao wa kiume huwakanusha kwa sababu moja au nyengine. Ningetaka nijue Mhe. Waziri kwa sababu ya utata huo wa wazee ni lini Wizara yako itashirikiana na Wizara ya Afya kutafuta kifaa cha DNA ili watoto wale wanaokanushwa na wazee wao kupata haki hiyo. Ahsante.

Mhe. Fatma Abdalla Tamim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Waziri swali dogo.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 18 hapa kuhusu elimu 2.1 imeelezea hapa sera mpya ya elimu ya mwaka 2006 imeelezea kwamba elimu ya maandalizi itakuwa sehemu ya elimu ya lazima kuanzia ngazi ya maandalizi hadi kidatu cha nne.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwa nini serikali hawaajiri walimu wa maandalizi wanaachia walimu wa skuli za *privates* wakati serikali imeamua skuli za maandalizi kuwa zitakuwa ni za lazima.

Mhe. Zahra Ali Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nikunipa fursa ya kuweza kuuliza swali langu.

1) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa katika nchi yetu watoto wanapofanya makosa huwa wanapelekwa Chuo cha Mafunzo. Na kwa kuwa mpaka hii leo haizuru kuwa wana chumba chao lakini mazingira waliyonayo ni ya kutatanisha bado mchanganyiko ni mkubwa wa watoto na watu wazima. Hii inapelekea watoto wale kuathirika kimwili na kiakili.

2) Mhe. Waziri nilitaka kujua kwa kupitia wizara yake anampango gani wa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kuweka mpango wa kuhakikisha kuwa watoto hawa wanatafutiwa sehemu mbadala badala ya zile sehemu hivi sasa walizonazo. Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi niulize swali langu kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwamba leo watoto kawatendea haki kwa sababu wenyewe wapo na tunawaona kwa mara nyengine ilikuwa hawapo watoto na tukawahi kumuuliza vipi leo ni siku ya watoto mbona hatuwaoni. Lakini ametenda haki wenyewe wapo kwa hivyo nampongeza sana na namshukuru.

1) Mhe. Waziri kwa sababu tarehe 16 ni siku ya kukumbuka watoto, ni siku ya watoto duniani. Kwa nini hii siku haishajihishi wakajua watoto wote kama leo ni siku yao. Wanajua watu waliyokuwepo hapa hapa mjini tu, kwa hivyo namuuliza ni lini ataishajihisha siku hii ili na watoto wajue kwamba leo ni siku yetu.

2) Siku za nyuma kulikuwa na utaratibu wa kusaidiwa watoto wale waliokuwa wazee wao kidogo hawajiwezi wanasaidiwa lishe na walikuwa wana utaratibu wa kupita vijijini na watu kusaidiwa. Lakini naona kwa muda mkubwa sijawaona kupita pita na kuwasaidia. Je, hili suala limekufa au bado lipo linaendelea.

3) Mhe. Waziri haki ya mtoto iko mjini na vijijini na iko Unguja na Pemba. Ni lini hasa serikali na kule Pemba itaweka kituo cha kulelea watoto cha serikali hasa. Kwa sababu Unguja kipo lakini Pemba hakuna. Wapo watu wa *Muslim Agency* wanasaidia watoto na wanawasomesha lakini ni lini hasa serikali na kule Pemba itajenga kituo cha kulelea watoto hasa tujue hiki ni kituo cha serikali. Ahsante.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri Kivuli kwa mawasilisho yao ya suala hili la haki ya mtoto wa Kiafrika.

Ningependa kumuuliza Mhe. Waziri kwamba siku hizi hapa Unguja kumejitokeza mtindo wa baadhi ya wazazi hususan akina mama nyakati za usiku hupita na watoto mitaani na huwafanya wale watoto ndio sababu ya kuomba. Bahati mbaya huwa ni wakati wa usiku ambayo moja haki ya mtoto kupata nafasi ya kupumzika, wakati huo watoto huwa kwenye migongo na wazazi wakipita mitaani kwa ajili ya kuomba.

1) Je, Mhe. Waziri suala hili serikali inalifahamu na kama inalifahamu nini kauli ya serikali kwa sababu kitendo kile cha usiku cha kumrandisha mtoto kwa kweli ni kumdhalilisha na kumtesa. Nini kauli ya serikali katika suala hili?

Mhe. Mwenyekiti, watoto wetu hususan vijana wadogo maskulini mwetu hupata tabu sana ya kushinda na njaa kitu ambacho tunakubaliana kwamba ikiwa hushibi na hata ufahamu wa mtoto unakuwa ni mdogo sana. Hii inasababishwa na watoto wengi wa kimaskini kwa kweli wanatoka nyumbani hawajala kitu mpaka warudi skuli.

Lakini vile vile na masafa nayo huwa yanachangia kuwafanya watoto wasipate chochote majumbani mwao. Wenzetu kule Bara huwa tunaona kwamba kuna

mpango maalum kupitia taasisi binafsi wakishirikiana na jamii kuwapitikia watoto angalau kupata mlo mmoja. Ikiwa tatizo hilo sisi tunalo hapa.

2) Je, serikali haioni kwamba wakati umefika wa kuandaa mpango maalum pamoja na kushirikisha na Kamati za Skuli angalau watoto wetu maskulini wapate japo uji?

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni tatizo la usafi. Nakumbuka wakati wa zamani kulikuwa na utaratibu maalum wa madaktari kupita katika maskuli mbali mbali kwa ajili ya kukaguwa watoto hali zao za usafi pamoja na afya. Kitu kile kwa siku hizi hakipo, lakini kipindi kile kilisaidia sana vijana wetu kuwa nadhifu na kuibukia na kukua katika hali ya unadhifu.

3) Sasa ikiwa suala hili ni zuri kwa afya za watoto wetu. Je, serikali ina mpango gani wa kurudisha mpango ule wa kuimarisha afya za watoto wetu katika maskuli?

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni suala la michezo. Taifa letu sasa hivi lina mpango mkuwa wa kuimarisha michezo. Moja kati ya mahala ambapo tunaweza tukatengeneza wana michezo na tukaibua vipaji vya michezo ni katika maskuli. Kipindi cha nyuma kulikuwa kuna utaratibu wa michezo kuwemo katika *curriculum* ya maskuli mbali mbali na kulikuwa kuna utaratibu wa kuwashindanisha watoto katika mambo mbali mbali ya kimichezo. Suala lile limekufa.

4) Je, serikali haiyoni kama kuna umuhimu wa kurejesha michezo na mashindano ya michezo katika maskuli?

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Muhiddyn Moh'd Muhiddyn: Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali machache. Kwanza kabla ya kuuliza maswala niombe nimshukuru sana Mhe. Waziri wa wanawake na watoto pamoja na watendaji wake kwa kutayarisha kitabu kizuri chenye ripoti hizi za watoto. Kwa hivyo tunamwambia ahsante sana na aendelee.

Mhe. Mwenyekiti, hii taarifa kwa nini isiletwe tarehe 16 kwenye kilele ya zile sherehe yenyewe ikawa inaletwa nje ya tarehe ile.

Kutokana na Sera ya Elimu ya sasa inatilia nguvu sana kuanzishwa skuli za maandalizi na wananchi wameitikia sana wito huo wa kuanzisha skuli hizi za maandalizi, nyingi zao vijijini ambao uwezo wa kuanzishwaji wa skuli hizi ni

mdogo kwa hivyo serikali chini ya wizara yake itachukua hatua gani kuweza kuzisaidia skuli hizi za maandalizi ili ziwe endelevu.
Misaada inayotolewa kwa wanawake wanaojifungua zaidi ya mtoto mmoja wanafanya utafiti gani kuweza kuwatambua wanawake hao ili kuweza kutoa misaada hiyo. Kwani ukiangalia katika jaduweli alilolionesha Mhe. Waziri katika Wilaya ya Kusini Pemba hakuna hata Wilaya moja ambayo wameweza kupata misaada wazee walijifungua watoto zaidi ya wawili.

Kama alivyosema Mhe. Hija na mimi katika jimbo langu yupo mzee anafanya kazi vizuri na akaweza kutoa watoto watatu kwa mpigo. Tokea mwezi wa 12 mwaka 2009 mpaka sasa hivi mwezi wa 6 mwaka 2010 hana msaada wowote alioupata. Namuomba Mhe. Waziri atueleze ni vipi anafanya utaratibu wa kuweza kuwatambua watu kama hao na kuweza kusaidiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ni taratibu gani zinazotumiwa ili kuweza kupata misaada kwa wazazi au walezi ambao hawana uwezo wa kuwalea watoto hao. Ukiliangalia jaduweli hili kuna Wilaya takriban za Unguja 6 lakini hakuna h ata Wilaya moja ya Pemba ambayo Wazee kama hao walezi wanasaidiwa. Hii ina maana kwamba kule Pemba hakuna wazee au walezi ambao hawana uwezo wa kulea watoto wao.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri baada ya taarifa yake nzuri naomba kumuuliza maswali haya yafuatavyo:-

1) Bado wanafunzi wetu wanaendelea kusota kwenye majamvi na kwenye sakafu je, wizara yako imeshirikiana vipi na Wizara ya Elimu ili kulimaliza kabisa suala la vikalio kwa watoto wetu wa maskulini hasa shule za msingi kwa sababu ndio wanaanza sasa.

2) Kuanzia mtoto anapozaliwa mpaka miaka miwili ni umri ambao upo katika malengo ya melinium Wizara yako inashirikiana vipi na Wizara ya Afya kuona watoto hawa wa umri wa 0 – 2 wanapata matibabu yaliyokuwa hayana malipo yoyote.

3) Viwanja vingi ambavyo vinasemekana viwanja vya wazi vinachukuliwa na vinajengwa. Je, Mhe. Waziri anafanya utafiti wa kiasi gani kuona baadaye watoto itabidi wacheze ndani tu na hawatakuwa na fursa tena ya kucheza nje isipokuwa watapiga na gari na kugongwa na baskeli?

4) Kwa sababu mtoto anapozaliwa anahitaji kupata cheti chake cha kwamba yeye amezaliwa na wazee wake ni fulani na fulani anashirikiana vipi na Afisi ya Utawala bora ili kuhakikisha kwamba wazee wanapata vyeti vya watoto wao chini ya miezi 6 ambavyo sasa inachukua zaidi ya miaka mitatu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nami nina maswali kidogo tu ya kuuliza kwa sababu mengine Mhe. Muhiddiyn kayachukua.

1) Katika ukurasa wa 21(2.5) tunaneshwa wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi mwaka 2009 wanafunzi hawa walianza wangapi darasa la kwanza mpaka wakamaliza elimu ya msingi wakiwa hawa.

2) Kuna jaduweli nam. 9 inaonesha wanafunzi waliofaulu michipuo mwaka 2010 wanafunzi hawa walikuwa wangapi waliofanya mitihani hata hawa ndio wakapasi michipuo.

3) Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 28 kuna huduma za ujenzi wa tabia katika kifungu cha 3.3, hapa kumeoneshwa kesi za watoto zilizopelekwa Mahakamani naomba kujua kupelekwa watoto mahakamani wanajengwaje tabia wakati Mahakama hizo kama zitawahukumu kwenda Chuo cha Mafunzo mambo wanayofanyiwa kwenye Chuo cha Mafunzo ni mabaya mno kuliko kuwa nje.

4) Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri kuhusu suala la maji, hivi watoto wa vijini ambapo maji mpaka leo hayajafika kama vile Wambaa kuna mpango gani wa kuwapatia maji.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti

Mhe. Ali Abdlla Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza maswali.

1) Mhe. Mwenyekiti, Katika ukurasa wa 42 Jaduweli Na. 22 Kesi zilizopokelewa kituo cha huduma za sheria.

Aina ya tukio	**Pahala**	**Hatua zilizochukuliwa**
Kubaka	Kinyasini Micheweni Pemba	Kesi imepelekwa Mahakamani Ushahidi haukupatikana Pemba.
Kubakwa	Tumbe Micheweni Pemba	Kuozeshana
Kubaka	Maziwa Ngo'mbe M/Pemba	Kesi imeripotiwa Polisi Micheweni Pemba
Kulawitiwa	Kisiwa Panza Mkoani Pemba	Suluhu imefanywa katika familia

Mhe. Mwenyekit, kwani hakuna utaratibu maalum wa kuhukumiwa kesi hizi, kwa utaratibu huu huoni kama kesi zitaendelea kuongezeka badala ya kupungua.

Ukurasa wa 27 hapo kuna jaduweli namba 10

"Matokeo ya utambuzi wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Jaduweli hapa imeonesha ni Wilaya ya Magharibi na Wete.

2) Je, hapa ni majaribio tu au Wilaya nyengine tayari imeshafanyiwa kazi kama hii na kama imefanyiwa kazi kama hii je, ni Wila ya gani ambayo imezidi nyenzake katika hali mbaya?

3) Ukurasa wa 29 misaada inayotolewa kwa watoto pacha. Hii imeoneshwa takwimu ya mwaka 2009/2010 basi. Je, utaratibu huu umeanza mwaka gani. Na je rikodi hizi zinachukuliwa hospitali mojwa kwa moja zinaletwa Wizarani au nyie mnakusanya?

Nataka nijue kwa sababu na mimi watu hawa ninao. Nashukuru.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii.

Katika wajibu huu wa kumuendeleza mtoto suala la elimu ndio lililopewa kipa umbele kwamba ndio njia ambayo inatumika zaidi katika nchi zetu katika kuendeleza watoto. Tatizo la elimu ambalo bado linajitokeza ni usafiri kwa

watoto. Hivi karibuni kwa upande wa Tanzania Bara tulisikia namna ambavyo Benki ya CRB ilianza kujitolea kuwatafutia mabasi watoto ili wapungukane na kadhia hii ya usafiri. Kwa sababu tunazo taasisi hapa za kibenki katika nchi yetu.

Je, serikali inaweza kufanya utaratibu wa kukutano na taasisi hizi kuona kwamba tunaiga mfano huo mzuri ambao umeanzishwa na wenzetu Tanzania Bara kwa taasisi hizi kuona wajibu wa kijamii wa kuwapatia mabasi wanafunzi walioko Zanzibar?

Iwapo kutakuwa na wafanyabiashara ambao wangependa kuendesha mabasi haya ya kuwasaidia wanafunzi. Je, serikali ipo tayari kuwapunguzia kodi ili waagizishie mabasi hayo pamoja na kuwapunguzia urasimu huu wa utitiri ambao wanapewa jawa operatars wengine wa mabasi?

Suala jengine ni suala linalohusu mambo haya ya *tuition* ambayo katika nchi yetu yameongezeka sana. watoto tumeona namna ambavyo wanapata shida sana kutembea mchana na usiku mwahala mbali mbali kutafuta elimu ya ziada. Sasa swali linakuja hapa.

(a) Kuongezeka huku kwa *tuition* kunasababishwa na upungufu wa walimu wenye ujuzi wa kufundisha masomo yale au ni tatizo gani hasa linalosababisha kuongezeke kwa tuition?

(b) Kwa watoto wanaume angalau huwa wana fursa ingawa si jambo zuri vile vile nao kutembea usiku. Lakini kwa wanawake inakuwa ni tatizo zaidi kwa sababu ya kuepusha mambo mengi ambayo huwa tunayapigia kelele humu. Serikali ina mpango gani wa muda mrefu kuona kwamba, kwa sababu sasa *tuition* ni suala la lazima. Hivyo kuna mpango gani wa kuona kwamba hili wanalizingatia ili kupunguza usumbufu kwa wanafunzi?

Swali langu la mwisho linahusu mambo ya malezi. Inaonekana kwamba kwa sababu kumezuka hofu katika jamii ya kwamba sasa serikali inataka kujiingiza katika jukumu lote la malezi ya watoto, kutunga sheria na wana wasi wasi sheria ambazo zinaweza zikapitishwa mara nyingi ni zile ambazo wanazitaka wafadhili wa Magharibi, ambapo wazee wa hapa wanaona ni kinyume kabisa na maadili, silka na mila za nchi hii.

Je, Mhe. Mwenyekiti, waziri anaweza akaiondosha hofu hii kwa kuwaeleza wananchi vipi kuhusu masuala haya ambayo yanajitokeza na mashahidi ni wengi. Kwa sababu juzi katika misikiti yote ya Ijumaa kulikuwa kunazungumziwa masuala haya, kwamba kunakuja sheria hapa ambazo kwa

kweli zitakuwa zinakwenda kinyume na maadili, silka, dini na utamaduni wetu. Je, suala hili ni kweli?

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi niulize maswali kidogo yanayohusiana na watoto wetu. Mhe. Mwenyekiti, kwenye jadweli *page* 31 hapa pana kesi ambazo ziko Mahakamani na nyengine zimetolewa ushauri nasaha, kesi zenyewe ni za kubakwa au kunajisiwa kwa watoto wanaume.

(a) Nimuulize Mhe. Waziri. Hizi kesi ziko Mahakamani na nyengine zimetolewa ushauri nasaha. Hakuna hata kesi moja iliyoamuliwa akapatikana mhalifu akatiwa adabu?

(b) Hizi kesi zinaonesha zote zinatoka Mikoa ya Unguja. Je, Pemba matokeo kama hayo hakuna? Kama yapo mbona hayajatiwa hapa?

Lakini niulize swali jengine la pili. sasa hivi wimbi la madawa ya kulevya linazidi marudufu na linasababisha kupoteza nguvukazi na linaongeza UKIMWI katika nchi yetu. Mhe. Waziri, kuna hatua gani ambayo serikali inachukua kukamata watelaji madawa ya kulevya. Mpaka hii leo hatujasikia hata mtu mmoja ameshikwa badala ya kushikwa walaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. Waziri, utatusaidiaje kwa sababu nguvu kazi zetu zinapotea bila ya kiasi. Watoto chini ya umri wa miaka 18 sasa hivi wameshaanza kula madawa ya kulevya. Je, waziri serikali na wewe mwenyewe mtatusaidiaje kuwakamata hawa watu ili tupungukiwe na hii balaa tuliyokuwanayo katika nchi hii? Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ame Ussi Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata fursa hii ya kuuliza maswali mawili. Katika ukurasa wa 10 jadweli ya 4 linalozungumzia miradi iliyoharibiwa kutekelezwa vijijini. Hapa kuna kifungu nambari 5 kinazungumza naomba kunukuu. “Mamlaka ya Maji imefanikiwa upelekaji umeme, ufungaji wa *pump* pamoja na uwekaji wa bomba la mita 150 na wananchi wanatumia huduma ya maji”. Mimi nataka niulize.

Uchunguzi huu uliofanywa kweli? Maafisa walifanya uchunguzi wa uhakika? Kwa sababu ninavyofahamu mimi na ninavyoijua Kigongoni, baada ya kuchimbwa kisima na kuwekwa *pump*, hakuna bomba lililofungwa wala hao wananchi kisima kile hawakitumii. Hivi kweli kuna uhakika gani wa haya maji kwa sababu hayajatumiwa na wananchi? Mabomba bado yapo pale yamelazwa na mengine ambayo tumepeleka juzi ya *three quarters* yanahitaji kufungwa.

Pili, katika jadweli ya 14 kunazungumza msaada wa watoto wanaolelewa na walezi wasio na uwezo kuwatunza. Hivi katika hizi takwimu zilizofanywa kweli Kaskazini hakuna watu kama hao hata mmoja basi inaonekana *zero*? Ni hayo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nataka niulize maswali machache sana kama ifuatavyo. Kwanza nataka niulize swali katika jadweli la 22 ambalo Mhe. Ali Abdalla Ali amelieleza sana lakini kule mwisho kuna kitu hakukisema. Kuna watoto wawili Micheweni katika ajira mbaya waliofariki, ambao watoto wawili anasema walifariki dunia wakati walipokuwa wakichimba mawe na kuelemewa na kifusi.

Je, hawa watu walioajiri watoto ajira mbaya kama hizi mpaka wakafariki. Serikali iliwachukulia hatua gani?

Halafu katika jadweli hili hili nambari 3 kunajisiwa, Konde, Micheweni Pemba kuozeshana. Sasa huyu mtu aliyenajisiwa akaozeshwa, aliyenajisiwa alikuwa ni mwanamke au mwanamme? Kwa sababu hapa haikuoneshwa.

Halafu swali jengine katika ukurasa wa 40. Kwanza nazishukuru sana hizi asasi za kiraia ambazo zimewatoa watoto katika ajira mbaya kama ulivyozitaja hapa sitaki kuzirejea. Lakini swali langu, hawa watoto 351 wa Wilaya za Pemba ambao walitolewa katika ajira za watoto na hizi taasisi ambazo umezitaja. Nyinyi mmewapa msaada gani?

Pili, mmefuatilia kuona kwamba hawarejei tena katika ajira hizo walizotolewa? Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Najma Khalfan Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami kupata nafasi jioni hii kuuliza maswali mawili matatu. Kwa kuwa watoto wa hapa Mjini Unguja wana sehemu za kupumzika na kucheza wao na wazee wao. Kwa mfano, *Jamhuri Garden* pamoja na Forodhani.

Je, Mhe. Waziri kuna mpango gani kwa watoto wa wilaya za Pemba na wao wakapatiwa sehemu kama zile wanazopatiwa wenzao hapa Mjini Unguja pamoja na watoto wa mashamba hapa Mjini Unguja wakapata na wao sehemu za kupumzika kama wenzao wa mjini.

Pili, kuna mpango wowote kuona kwamba wanafunzi wanaosoma sekondari hawa wale wanaosoma *science* kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuona kwamba wanafunzi hawa wanapata kufanya *science* kwa vitendo badala ya kusoma kama hivi wanavyosoma hivi sasa bila ya vitendo?

Tatu, kwa kuwa kwa bahati mbaya baadhi ya wanawake hujifungua kwa operesheni, na wanapojifungua hutakiwa walipe shilingi 40,000/-hapo Hospitali ya Mnazi Mmoja. Jambo hili tumeshalipigia kelele sana hapa katika Baraza letu la Wawakilishi, lakini inaonekana bado linaendelea. Je, kwa kushirikiana na wizara yako pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuna mkakati wowote wa kuwaondolea wanawake pamoja na waume zao bila shaka mzigo huu wa kulipa fedha? Ahsante.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mimi naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba katika ukurasa wa 42, jadweli nambari 22, *Item Nom. 2* inazungumzia tokeo la kupigwa watoto lililofanyika Shamiani Chake Chake Pemba, taarifa zilizotolewa kwa mwalimu wa madrasa, polisi na Kituo cha Huduma za Sheria.

a) Je, ni aina gani ya pigo walilopigwa watoto hao?

b) Ni nani aliyepiga, ni mwanafunzi au mwalimu wa madrasa?

c) Ni kweli Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekataza wanafunzi kupigwa bakora. Je, kwani amri hiyo nayo inawahusu kwa walimu wa madrasa na wazazi?

Swali langu jengine ni kwamba, katika jedwali nambari 21 ukurasa wa 40 kuna watoto 351 waliotolewa katika ajira katika Wilaya ya Mkoani, Chake Chake, Wete na Micheweni.

(a) Je, Mhe. Waziri amefanya utafiti wowote wa sababu hiyo ambayo imewafanya watoto hao kufanya kazi hizo?

(b) Kwa sababu wilaya zinazoongoza kwa tabia hizo ni Micheweni na Wete kwa mujibu wa jedwali hilo, ambazo pia kwa mujibu wa *house of budget survey* ndizo zinazoongoza kwa umasikini hapa Zanzibar. Je, haiwezekani kuwa ni sababu za umasikini wa wazee wao ndio imesababisha watoto hao kufanya kazi?

(c) Ikiwa ni hivyo. Je, kuna jambo lolote ambalo Mhe. Waziri anaweza kutwambia kwamba serikali itafanya kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba ili waondokane na umasikini uliokithiri?

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi. Nilikuwa nina maswali mawili lakini na moja nilikuwa nataka kumuomba Mhe. Waziri afanye masahihisho.

Ukurasa wa 15 katika jadweli kifingu nambari 5 kimeandikwa, 'Koani Mradi wa Maji umekamilika na wananchi wanafaidika na huduma hiyo'. Mhe. Waziri mradi haujakamilika. Kutokana na barabara inayojengwa mtandao wote umevurugika sasa hivi tunaanza kuweka mtandao mwengine. Lakini pia katika mradi huo tulipofanya mabomba yalikuwa hayajatosha kuna sehemu bado mabomba hayajafika. Kwa hivyo, mradi huu haujakamilika. Marekebisho.
Lakini jengine swali langu liko katika jadweli nambari 22 kifungu cha 9, pameandikwa kulawitiwa Gando – Wete Pemba, moja. Lakini pia wameandika suluhu imefanyika kifamilia. Sasa swali langu kwanza huyu aliyelawitiwa ana umri gani? Lakini je, wizara haioni kwamba huyu mtoto amekuwa *effected psychologically?* Wameridhika na suluhu ya kifamilia ndio wameliacha hivi hivi?

Swali langu la mwisho la tatu, nimeangalia kitabu chote sijaona pahala panapoonesha watoto waliyoolewa wakiwa chini ya umri wa miaka 18 na wako wengi. Sasa wizara haijapokea kesi kama hizo? Kwa sababu hivi karibuni mimi nilipata taarifa ya kesi kama hiyo, kwamba kuna mtoto katika shehia moja anataka kuolewa. Tumekwenda tumezuia ile ndoa na yule mtoto tumemrudisha skuli anaendelea kusoma. Sasa kesi kama hizi sijaziona hapa. Je, hawajazipata? Nashukuru Mwenyekiti.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali machache kama ifuatavyo. Watoto wako wa namna nyingi lakini na sisi hapa Zanzibar tuna wale ambao wana ulemavu wa ngozi, jina maarufu wanaitwa albino. Je, Mhe. Waziri anaweza kuniambia tuna watoto wangapi maalbino Unguja na Pemba na kuna msaada gani maalum watoto hao wanaopewa na serikali?

Swali la pili ni kwamba, kuna baadhi ya skuli hata katika Jimbo langu la Ole, wanafunzi ambao ni watoto wanaposhindwa kulipa ada maalum ya kuingilia darasa jengine adabu yao huwa ni kupewa uhamisho kupelekwa skuli iliyo mbali zaidi na pale walipo. Hili linasababisha baadhi ya watoto wanashindwa kutii uhamisho ule kwa sababu ya umbali na hivyo wanaacha masomo.

Je, hili waziri analijua? Kama analijua, anajua kwamba sababu moja ya kumnyima haki mtoto ni hii ambayo imesababishwa na skuli yenyewe na bila shaka si skuli itakuwa ni serikali?

Je, hii ni haki ya serikali kuweka masharti kama hayo ambayo yanamnyima mtoto wa kimasikini haki ya kupata elimu?

Swali la tatu naongezea swali alilouliza Mhe. Said Ali Mbarouk jadweli nambari 21. watoto waliotolewa katika ajira Pemba. Jadweli kama hili hasa

kwa vile umeweka wilaya zote nne, mtu anasoma kwamba watoto 351 ndio wa Pemba nzima. Mimi ninavyokumbuka jimbo langu peke yake watoto ambao wametolewa kwenye ajira ni zaidi ya 100, lakini hapa siwaoni.

Je, jadweli hili ni pungufu au ndio utafiti pekee uliofanywa kwa wilaya hizi na maeneo haya? Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nami kunipa nafasi hii ya kuchangia taarifa ya haki ya mtoto. Mhe. Mwenyekiti, mimi nakuja na swali langu lamwanzo ambalo limechangiwa lakini na mimi nitalichangia kwa muono ninaouona mimi, linalohusiana na dawa za kulevya.

Kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti, madawa ya kulevya yameathiri kwa muda mrefu watoto wetu na watu wa aina mbali mbali ambao wakubwa wanavuta na wadogo wanafuata chini ya umri wa miaka 18. nataka kumuuliza waziri tu. Je, amejipanga vipi au amejianda vipi kuwatafutia sehemu vijana hawa ambao wameathirika na madawa ya kulevya ili kuwahifadhi kupunguza ule uvutaji na athari zinazowasababisha madawa ya kulevya. Je amepata eneo la kuhifadhi vijana hawa?

La pili linahusiana na chanjo ambazo baadhi ya watoto wetu chini ya umri wa miaka mitano huwa zinawaathiri na vile vile huathirika kwa yale madawa wanayopewa. Wakati huo huo wanapolazwa kunakuwa na mafaili ya kumbukumbu za dawa walizotumia na athari walizozipata kwa kuathirika na madawa hayo.

Je, ana mpango wowote wa kufuatilia katika mafaili hayo ili kujua watoto walioathirika na kuwapatia msaada wowote wa kuwasaidia?

Suala la tatu linahusiana na ajira kwa watoto. Kwa kuwa baadhi ya vijana wetu na watoto wetu chini ya umri wa miaka 18 wanashughulika na biashara za ajira zisizo rasmi. Utakuta watoto wanapiga deme kwenye daladala, wengine wanapara samaki, wengine wauza biashara ndogo ndogo kama samaki na maandazi. Je, wizara yake anahisi kwa kipindi hiki cha miaka mitano wamepungua kwa asilimia ngapi watoto wanaofanya biashara hii au limeondoka kabisa tatizo hili?

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya skuli zetu zina watoto wadogo wadogo wa msingi na ambapo mahitaji ya maji ya kunywa wanapata katika visima vilivyokuwa sio rasmi, madimbwi madogo madogo. Kwa mfano, Skuli ya Kilimihewa Jimbo la Amani maji yao mara nyingi wanachukua ya kuokotoa na wanayo sehemu kubwa ya kuchimba kisima cha *boo hole* na wakapata maji salama.

Je. atakuwa na mpango wowote wa kuwasaidia hawa kwa kuchimba kisima kile ambacho kina gharama ya kiasi shilingi milioni tatu ili wapate maji salama na kuepukana na kichocho na maradhi mengine?

Mhe. Mwenyekiti, swali la mwisho. Barabara zetu nyingi zinazojengwa huwa haziwekewi sehemu ya watu wanaotembea kwa miguu kama vile ilivyowekwa barabara ya Kinazini kwenda Bububu. Mule mara nyingi hupita watu mbali mbali na hata watoto wetu wanapokwenda skuli.

Je, ana mpango wowote wa kushauriana na wizara husika ili zikijengwa njia ziwekwe sehemu za wapita kwa miguu? Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nimpongeze sana waziri kwa kuwasilisha taarifa hii kwetu sisi pamoja na wasaidizi wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, naona maswali yameanza mapema kabla ya bajeti yangu, lakini yote baraka na kuzimua ukali kwa huko mbele. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana maswali ya kimsingi yameulizwa na yote yanalenga katika kuleta ubora zaidi katika sekta yetu ya elimu.

Suala la kwanza ambalo limeulizwa nilipofika hapa nimemsikia Mhe. Haji Mkema Haji akizungumza kwamba kuna lugha ya kikoloni inafundishwa na pengine ni kama lugha ya Kiswahili hatuipi nafasi.

Napenda kumhakikishia Mhe. Haji Mkema na waheshimiwa wengine wote kwamba, lugha ya Kiswahili ina nafasi maalum katika nchi yetu na ndio lugha ya taifa. Ndio maana lugha ya Kiswahili inafundishwa tokea maandalizi hadi Chuo Kikuu kama ni ligha , lakini wakati huo huo tumeanzisha Taasisi yetu ya Kiswahili na Lugha za Kigeni kwa madhumuni ya kuendeleza lugha hiyo ya Kiswahili.

Lakini sasa tunapokuja kuzungumzia suala la lugha ya Kiswahili katika baadhi ya maeneo na Sera yetu ya Elimu imepitisha sera kwamba darasa la tano na sita siku si nyingi kuanzia sasa hivi tutafundisha kwa lugha ya Kingereza. *Medium Instruction* katika madarasa ya tano na sita itakuwa ni lugha ya Kiingereza. Tukumbuke na tuelewe kwamba mpaka sasa hivi tungekuwa na nia nzuri hata namna gani kwa kufundisha Kiswahili sekondari ingetuchukua muda kidogo kwa sababu vitabu vyote dunia nzima vimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza vikiwemo na hivyo vyetu ambavyo tumeviandika hivi karibuni.

Kuna vyombo hivi vya mitandao ambavyo vinatumia kompyuta, ukiacha vile vya Kiarabu, Kifaransa na wengineo, lakini sisi huku katika bara letu bado tunatumia kwa lugha ya Kiingereza. *Information* zilizomo mle ni za Kiingereza na inabidi tuziimarishe kuzifundisha katika skuli zetu.

Lakini tunapokwenda kwenye mambo ya utandawazi, lugha ya Kiingereza nayo ina nafasi yake. Tunaposema tuimarishe utalii hatuwezi kuwa na idadi kubwa ya watalii hapa petu halafu tukashindwa kuwa na watu wa kushindwa kuzungumza nao. Kwa hivyo, lisiwe tatizo hili na namuomba Mhe. Haji Mkema asione kwamba tunafanya makosa kufundisha lugha ya Kiingereza, dunia nzima wanafundisha lugha ya Kiingereza.

Mimi hivi karibuni nilikuwa Oman na kuna skuli wao wanazungumza zaidi Kiarabu lakini kuna skuli ambazo zinafundisha lugha ya Kiingereza makusudi ili waendane sambamba na mahitaji ya dunia.

Kuna suala jengine ambalo limeulizwa na Mhe. Fatma Abdulla Tamim kwamba kwa nini hatuwaajiri walimu wa maandalizi wakati skuli za binafsi zina walimu wa maandailizi. Skuli za serikali hazizidi 37 za maandalizi, wakati za binafsi ziko zaidi ya mia mbili na zaidi. Sasa wao lazima watawatafuta walimu waweze kuwaajiri. Lakini hapa Zanzibar bado hatujawa na Chuo cha Ualimu cha Maandalizi isipokuwa tuna Kituo cha Mafunzo ya Maandalizi hapo Saateni na kule Pemba vile vile tunacho kimoja.

Hivi sasa serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inatafuta uwezekano na tuko katika hatua nzuri ya kutayarisha mahali kujenga chuo hasa cha maandalizi ambacho kitakuwa kinawapatia mafunzo walimu. Lakini pia tunakusudia tukijaaliwa kuviimarisha vile vituo vya jumuiya. Lakini pia tukumbuke kwamba serikali imekuwa ikihimiza ubia na hivi sasa tunashirikiana vizuri na taasisi binafsi katika kuendeleza elimu hii ya maandalizi. Tunaposema *PPP* zile tatu zina maana hiyo, *Public Private Partnership* za kuweza kushirikiana nao katika masuala mbali mbali.

Serikali pia kwa kuona umuhimu wa kuwapatia haki yao watoto, tumeanzisha ujenzi wa skuli maalum za maandalizi. Tunajenga moja Msuka sasa hivi na taarifa nilizokuwanazo za uhakika ni kwamba tayari tushaezeka na hatua za kuweka madirisha na milango zinaendelea. Nyengine moja maeneo ya Potoa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na tunakusudia kujenga nyengine kama hizo katika kila mkoa ili tuwe na skuli za maandailizi maalum na zitakuwa *concentration* yetu kuwapeleka vijana wetu kusoma katika maeneo yale. Kabla hatujawapeleka vijana wa pale, tunahakikisha kwamba walimu wa maeneo yale na wao wanapatiwa mafunzo maalum ya maandalizi. Kwa hivyo, hilo tutalifanya.

Pia nizungumze suala la *School Feeding Program*. Kweli ni jambo zuri na mimi ni mmoja katika tulio-*benefit* wakati nikiwa *primary school*, tulikuwa tunaletewa maziwa na Wamarekani kwenye *boxes*, tulikuwa tunatamani hata ikikaribia hatumsikilizi tena mwalimu, tunangojea wakati tu wa kupewa maziwa yale ambayo tulikuwa tunakunywa wakati ule.

Ni eneo ambalo tunaweza kushirikiana na wizara hii pamoja na *UNICEF* na wengineo kwa kuweza kuwasaidia vijana wetu. Kwa sababu wengine wanaondoka nyumbani hali zao kidogo sio nzuri. Kwa hivyo, tutafanya utaratibu wa kuweza kulifanyia njia ili liwezekane hili.

Lakini vile vile Mhe. Omar Ali Shehe sijui anapozungumza kwamba michezo haipo skuli anakusudia vipi. Michezo ipo kutoka *Preschool* hadi *University* michezo ya aina zote. Kuna michezo iliondoka siku hizi naiona ya watoto wadodo kukimbiza wakiwa wamejifunga mabofu, kula maandazi, wamefungwa mikono nyuma, riadha, *potatao race* zile, zote zinaendelea mpaka leo. Tuna mashindano ya elimu bila ya malipo wanashindana vijana wetu katika *level* ya *primary school*, *secondary school* na vyuo vyengine mpaka kwenye vyuo vikuu. Kwa hivyo, michezo ipo na tutaidumisha. Mimi mwenyewe napenda sana michezo na ndio maana mambo ya michezo yamekuwa mazuri.

Lakini pia kuna suala zima hapa ambalo limeulizwa na Mhe. Mohamed Ali Salim na napenda nimjibu. Aliuliza swali la kwanza uandikishaji wa msingi walianza darasa la kwanza wangapi?

Mhe. Mohamed Ali Salim takwimu tulizozifanya kwamba kila unapofika darasa la saba hasa kwa hesabu hii ambayo tumeipata ya 2009, kwa sababu 2010 bado hatujafanya mitihani, asilimia 7 ya wanafunzi wana-*drop*. Sasa hao ukitizama waliomaliza hapa walikuwa ni 22,179. Kwa hivyo, ukifanya hesabu unapata kama wanafunzi walioanza darasa la kwanza walikuwa 23 na mia nne mpaka mia tano hivi.

Kwa hivyo, asilimia 7 ime-*drop* na hii ni *problem* kubwa ambayo tunahitajia kui-*address* kwa wananchi wenyewe waelewe. Kwa kweli inatu *disappoint* kidogo kwamba hawa ni watoto wako kwenye *basic education* na wana-*drop*. Tatizo tunalijua *offcourse* wakati mwengine hali ya kiuchumi na mambo mengineyo huko mitaani, lakini umaskini isiwe sababu ya kutokupata elimu. Sote tumesoma katika mazingira hayo na tumefika hapa. Kwa hivyo, hilo ni moja ambalo napenda nikuhakikishie kwamba tunalifanyia kazi.

Lakini michipuo waliofanya mitihani ndio hawa 22,179 tukapata hawa 780. Kiwango ambacho tumeweka ni kikubwa kwa sababu tunachukua michipuo

wanaopata asilimia 80 na kuendelea na wale vipawa tunachukua asilimia 85. kwa hivyo, inabidi kidogo uchujaji pale unakuwa ni mkubwa sana. Lakini pamoja na hayo yote bado kwa kiwango cha *primary* tunahitajia kuimarisha. Kwa sababu *primary* ukipata asilimia 50 chini ya hapo utakuwa umefeli kwa mujibu wa takwimu zetu, yaani una kiwango cha F. Kuanzia 51 na kuendelea ndio unaanza ile D,C na mpaka unapata ile A yenyewe.

Kwa hivyo, ni kweli bado hatujafikia kiwango hicho. Lakini ukichukua *graph* yako ukichora miaka 10 iliyopita na sasa hivi, vijana waliokuwa wanaingia michipuo kwa wakati ule walikuwa hawazidi hata 300 au 400. Sasa hivi tumefika 780, si haba tunajikongoja kidogo kidogo.

Suala la usafiri ni la msingi kabisa, hasa ambalo linanitia uchungu sana mimi mwenyewe nikiwa kama waziri kuona wanafunzi wa kike pale Chuo cha Kiislam jioni wamekaa pale wanasubiri usafiri. Tena Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili nilipopata nafasi ya kwenda Oman hivi juzi, nilizungumza na wenzangu na nimeomba mabasi *Alhamdulillah*, nadhani yatatosha kwa kwa mahitaji yetu. Maana niliomba kidogo, nikaambiwa ongeza kidogo, kwa hivyo nimepata tamaa kwa ajili ya Chuo chetu cha Kiislam cha hapa na Chuo cha Kiislam cha Kiuyu na pia tunakusudia kuwasaidia na wenzetu wa afya kule pindi tukipata idadi kubwa kidogo, lakini kwanza tutaanza na wizara ya elimu.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, hapa palikuwa na suala la *tution*, sio la mwisho. Kwa nini tunakuwa na *tuition*, *tuition* hazikuanza jana na leo, kwa tafsiri ya *tuition* ni *extra classes. Tuition* zimeanza kabla ya Mapinduzi na baada ya Mapinduzi tulikuwa na *tuition* hizi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kaka yangu ni mwalimu kafundisha miaka mingi tu. Nilikuwa mdogo wa darasa la pili na la tatu nilikuwa naona kwenye miaka ya 59,60 na 61 wanakuja watu pale nyumbani kusoma, ile ni sehemu ya ziada ya darasa vile vile. Kwa hivyo *tuition* hizi ni nyongeza ya kupata elimu.

Lakini tatizo jengine ambalo linafanyika, kuna mambo mawili hapa ya kimsingi. Kuna baadhi ya masomo bado tuna matatizo nayo nayo ni ya sayansi. Moja katika *challenge* ambazo nimekuwa nazo mbili hizi ninazo ambazo nazitafutia *solution.* Kweli bado tuna upungufu wa walimu wa sayansi, mathematics na suala la *furniture* ambalo nitalitolea ufafanuzi. Haya ni mambo mawili ambayo tunajitahidi tuyakamilishe haraka iwezekanavyo ili tuondokane nayo yameshakuwa ni ya siku nyingi, hasa suala hili la walimu. Ndio maana tumeanzisha programu maalum sasa hivi, walimu 500 tunawachukua kila mwaka kuwapatia programu za sayansi ili waweze kufundisha katika madarasa ya sekondari.

Chuo Kikuu chetu kina utaratibu, nadhani hivi karibuni tutaanzisha programu ya diploma ya sayansi. Tayari tumeshapata wanafunzi wa digrii ya kwanza ambao wanasoma sayansi hapo na kwenye vyuo vikuu kama vya Chukwani kule na nje ya Zanzibar. Kwa hivyo, tunajitahidi kujiimarisha huko na safari ni hatua tunatarajia baada ya muda sio mrefu basi tutafika pahala pazuri kwa kutatua tatizo hili.

Kwa hivyo, *tuition* zinafanyika moja ni kwamba tunakuwa na ukosefu wa walimu hasa katika maeneo maalum. Wengi wa wanafunzi hao utaona wanatafuta walimu katika masomo ya sayansi, kwa sababu ndiko ambako kuna matatizo kidogo. Pamoja na matatizo hayo bado wanafunzi wetu wanafanya vizuri. Hivi karibuni tumetoa matokeo ya A *level* nilifarajika sana kuona kuna wanafunzi wanapata A ya hesabu, A ya *physics* na A ya *Chemistry* sio mwanafunzi mmoja wala wawili. Kwa hivyo, bado tuna imani kubwa kwamba wanajitahidi wanafunzi na hizi *tuition* zinasaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa nimezipiga marufuku zisiwe zaidi ya saa 2:00 usiku na marufuku hii bado ipo, kama inatekelezwa sawa na kama haitekelezwi basi watu wanavunja agizo la waziri. Hili ni agizo la serikali tumesema *tuition* zisizidi saa 2:00 usiku, makusudi ili kudhibiti na kuweza kulinda maadili yetu. Kwa hivyo, natarajia kwamba amri hii itaendelea kutekelezwa na sitoifuta kwa sasa hivi mpaka nitakapomaliza muda wangu, sijui lini.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abass Juma Muhunzi katika suala hili napenda nimwambie kwamba, wakati ni muhimu sana. Unapokuwa skuli muda wa kusoma unakuwa ni mdogo kusema ukweli, lakini ukenda kwenye *tuition* usifikiri kwamba unafukia mashimo yale ambayo asubuhi ulikuwa uyafukie. Lakini tatizo linakuwepo ni baadhi ya walimu wakati mwengine ninapata taarifa ambazo sina uhakika nazo kwamba wana-*pay constitution* kubwa kwenye *tuition classes* kuliko kwenye madarasa. Sasa hili najaribu kulifuatilia kwa makini ili kuona kwamba walimu wa aina gani wanaofanya hivyo. Kwa sababu jukumu la mwalimu kwanza ni kufundisha katika madarasa ya kawaida, haya ya baadae ya nyongeza yawe ya nyongeza kweli, yasiwe kwa utaratibu mwengine wowote.

Mhe. Mwenyekiti, sidhani kama nimebakisha namaliza na hili la *furniture*, ni kwamba sasa hivi tumetega bajeti karibu kila fedha tunazopata za muda wetu kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi na ninashukuru tunazipata vizuri na kwa wakati, tunatenga Shs.100,000,000/= kwa ajili ya *furniture*.

Vile vile tunatarajia kupata msaada mkubwa katika suala la elimu kutoka nchi hiyo hiyo niliokwenda ya Oman katika elimu na tunataka tutumie kiwango

kikubwa cha fedha ambazo tutapata kununulia *furniture* kwa ajili ya kupunguza tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, nimshukuru Mhe. Asha Abdallah Juma. Nawaombeni mtuombee Mungu *Inshaallah* siku ya Alhamis ndio tunakwenda kuchukua ile *form* ya mambo yenyewe, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri dua umeshaombewa siku nyingi. Sasa tumsikilize Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, aje kujibu maswali yaliyojitokeza hapa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kabla sijajibu napenda tukumbushane kwamba wizara yetu hii ni wizara mtambuka, ambayo imegusa *sector* nyingi zimekutana hapa pamoja ambazo tumeziripoti humu. Kwa bahati mbaya sasa hivi naona humu ndani watu wengi hawamo wameshakwenda kushughulika na mambo mengine, kwa hivyo mimi nimefikiri kwa yale masuala ambayo yanawagusa moja kwa moja *sector* nyingine kwa mfano maji, nilifikiri labda yatakuja kuulizwa kwenye bajeti *speech*, kwa sababu hapo ndio mtapata majibu ya kina hasa. Vyenginevyo mimi siwezi kuwa mtaalamu kwa mambo yasiyonihusu, nitakuwa mtaalamu kwa mambo yangu yanayonihusu mimi.

Mhe. Mwenyekiti, haya masuala yamekuja wakati mzuri kwa sababu watu wengi hawajawasilisha bajeti zao kwa hivyo, nitarudisha tena maswali hayo kule kwa wale wanaohusika. Lakini nitajibu yale ambayo yananihusu mimi moja kwa moja.

Mhe. Ali Suleiman Ali, aliuliza kuwa ana wasi wasi Masheikh wa Kiislamu wana manung'uniko kuhusu sheria na haki za watoto, sheria ambayo tunataka tuipitishe hivi karibuni na akauliza ni mara ngapi wamefanyiwa semina. Niseme kwamba semina imefanywa kama mara tatu, sehemu tofauti kwa siku tofauti na watu wameweza kuchangia na kutoa maoni yao namna gani ya kuboresha sehemu hiyo.

Mhe. Ali Suleiman aliendelea kuulizia kuhusu msaada. Naomba nimwambie tu kuwa sisi tunajitahidi kwa kadiri ya nguvu yetu na mfuko wetu. Kwa sababu utafiti ni gharama inabidi uzunguke huku na huku, kwa ile nguvu ambayo tumeweza kufanya ndio tumeweza kupata hizo taarifa ambazo tumezileta katika kitabu hiki.

Pia alilalamika kuwa kuna mateso katika usafiri. Hili jambo ni kweli kila mtu ameliona na lipo. Nafikiri hapa tunahitaji mpango wa pamoja ili kuona namna

gani kwa sababu hili sio tatizo la wizara yetu peke yetu, ni tatizo la jamii nzima. Kwa hivyo, kila mtu achangamshe bongo lake afikirie na yeye tatizo hili anaweza akalitatua vipi au ana mchango gani ili tuweze kuwaondolea hawa vijana wetu matatizo haya na sio kungoja hapa Barazani aje kuuliza na yeye awe na mchango kwa sababu hili ni tatizo kweli.

Mhe. Omar Ali Jadi, yeye alisema kwamba ulezi ni kazi. Nakubali ulezi ni kazi na sio kazi ya mtu mmoja ni kazi ya watu wote. Aliuliza kuhusu idadi ya ripoti za watoto ni ngapi. Sisi hizi tulizozipata hapa ndizo ambazo zimeletwa kwetu na tumeweza kuzipata katika hizo sehemu husika kama Mahakama.

Vile vile tunaamini kuwa masuala haya kwa kuwa mara nyengine hayaripotiwi kikamilifu, kwa hivyo tunaamini kwamba pengine idadi ni kubwa zaidi kuliko ile ambayo tunaipata sisi katika mikondo yetu.

Kuhusu suala la vyeti, tunatambua kwamba cheti cha kuzaliwa ni lazima na ndio haki moja wapo ya mtoto naamini wizara husika inafanya utaratibu na kama mtu atakuwa amepata kuchelewa basi sio kwa makusudi, kwa sababu kama wewe hujenda kutoa ripoti kwa wakati muafaka halafu uje ulalamike basi inakuwa wewe mzazi ndio mkosa.

Mimi nakumbuka hapo zamani nilipokuwa mdogo nilikuwa nasikia watu wanashtakiwa kama hujenda kuripoti uzazi au kifo, inakuwa ni kosa. Kwa hivyo, sasa hivi tushajihishane kwamba hawa watu wenyewe nao waone umuhimu wa kuripoti na kuorodhesha uzazi wa mtoto mapema. Kwa hivyo, serikali inaendelea kwa sababu afisi ipo na vyeti vipo, sijasikia kwamba kuna upungufu wa vyeti.

Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban eti kuna upungufu wa vyeti?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Hakuna.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Hakuna. Kwa hivyo tuendelee tu kuzaa na tuendelee kuandikisha kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, naambiwa hapa kwamba kuna vyeti vingi vya kuzaliwa bado havijachukuliwa katika afisi hiyo inayohusika. Kwa hivyo, tukavichukuwe hivyo na vingine tukaviandikishe.

Mhe. Haji maswali yake yameshajibiwa na hili jengine la *vitamin* A na kwamba watu wapewe nafasi ya kwenda kunyonyesha. Nafikiri fursa hiyo ipo, watu wanakwenda kunyonyesha. Kwa hivyo, tuhimizane kwamba kunyonyesha maziwa ya kifua ni muhimu, kwa hivyo hiyo vitamini A mtu ataipata moja kwa

moja, kuliko kupeana maziwa ya kopo, maziwa ya kopo yawe ni ya mwisho kama ni hatua ya mwisho ikiwa haya ya kifua yanakosekana.

Kwa sababu kuna utaalamu mwengine maziwa pia unaweza kuyavuta kwa *pump* ukayaweka kwenye vichupa, ukayaweka kwenye friji ukatumia kwa mujibu wa anavyotaka kunyonya mtoto. Sio lazima kila wakati uende huko nyumbani, kama una vifaa hivyo unaweza kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hili suala la maji, nafikiri Mheshimiwa aje aliulize siku ya bajeti ya maji na hili la vyandarua tutaendelea kushauriana na wenzetu tuhimize, ili vyandarua vipatikane kwa wahusika kwa mujibu wa mahitaji yenyewe.

Mhe. Hija Hassan Hija alizungumzia hili suala ambalo linahusu moja kwa moja Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika upelekaji wa watoto wenye maradhi ya moyo Israel. Naamini kwamba serikali inajitahidi sana kuwapeleka kwa kadiri ya nguvu yake na uwezo wake. Naamini pia tutaendelea kupeleka watoto kwa sababu maisha ni muhimu, hatupendi watoto wafe. Kwa hivyo, tutaendelea kujitahidi na kuongeza jitihada ili watoto wote wenye matatizo yaweze kutatuliwa.

Suala jengine lilikuwa ni msaada wa maziwa kwa wazazi ni utaratibu gani unachukuliwa. Kwa suala hili mimi sina jibu lake, nafikiri Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itakuwa inao utaratibu inaofanya.

Suala lake jengine lilikuwa ni kuhusu watoto wanaozaliwa nje ya ndoa ni lini kifaa cha *DNA* kitapatikana. Tumebahatika hapa leo Waziri wa Fedha na Uchumi mwenyewe Dk. Mwinyihaji yupo atashirikiana na Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mhe. Sultan Mugheir ili kuona katika mwaka ujao pengine kama kuna uwezekano basi kifaa hiki kipatikane, kwa sababu ni muhimu sana kuweza kuwagundua wale wakorofi. Kwa sababu endapo sheria yetu ya mtoto itapita, basi itabidi wale wanaokwepa malezi pia tuwajuwe. Kwa sababu kuna wengine wana mtindo wa kukimbia wakati wameshafanya mambo, halafu wakakataa dhamana zao tutaweza kuwagundua kwa *DNA* halafu tutawawajibisha kwa kutunza watoto. Kwa hivyo, naamini Dk. Mwinyi hilo litawezekana.

Suala la Mhe. Fatma limeshajibiwa. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Zahra Ali Hamad alizungumzia kuhusu kupelekwa watoto Chuo cha Mafunzo. Ni kwamba sheria yetu mpya ambayo tunatarajia itoke ya sheria ya mtoto, imeziita hizo kama shule maalum ambayo itaitwa *approved school.*

Vile vile mara nyingi hatupendi watoto wapelekwe kwenye vyuo vya mafunzo, lakini inakuwa ni hatua ya mwisho pale inapokuwa usugu umezidi au ukorofi umezidi sana. Lakini mara nyingi huwa tunawapeleka kwenye hizi wanaziita *reformatory schools* ambapo kule wanajitahidi kutengenezwa tabia na kuwekwa na tabia njema kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Subeit Khamis Faki alisema hii siku ya tarehe 16 ni siku ya kumbukumbu ya watoto je watashajihishwaje. Watoto wanashajihishwa sana. Kulikuwa na shughuli nyingi tu ambazo zimefanywa na wizara yetu kwa siku hiyo, kwa kupitia redioni, televisheni na majarida mbali mbali kwa kuadhimisha siku hiyo.

Pia aliuliza ni lini serikali itajenga kituo kule Pemba. Kweli kituo cha kulelea watoto kwa kule Pemba hakipo, lakini naona ni wazo zuri sana. Kwa hivyo, niseme kwamba nitachukua jitihada tutakapomjua mgombea wetu ambaye atapita na kuwa Rais wetu wa Chama cha Mapinduzi, basi mimi nitamwambia kwamba Wajumbe Baraza la Wawakilishi wanaomba hili, kwa hivyo tutafute namna ya kujengwa hicho kituo kule Pemba. Nafikiri hilo wazo ni zuri na huyo mgombea *Inshaallah* atakayepatikana atalipata, na mimi nakuhakikishieni nitamfikishia hili.

Mhe. Omar Ali Shehe, alilalamika kuhusu mtindo uliozuka siku hizi wa kina mama kubeba watoto kisha kwenda kuomba usiku na anauliza kama serikali inafahamu. Kwa sababu jambo hili linafanyika na sote tunaona sio serikali tu na serikali ni sisi. Kwa hivyo, sote tunaona na hapa panahitaji pia mbadiliko wa utamaduni ili tufahamishane na hii jamii. Kwa sababu hayo mambo ambayo yanafanywa hayapendezi na wengine kusema kweli wala hawana shida kufikia kiasi hicho cha kwenda kufanya utaratibu huo wa kuomba na watoto usiku.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hatujawa na sheria ya kuweza kudhibiti wakina mama na watoto basi inakuwa ni vigumu kwa upande wa serikali kuwatia hatiani hawa kwa sababu hakuna kifungu cha sheria kinachosema kwamba ukizurura na mtoto usiku ni kosa, ingawaje uzururaji ni kosa kwa namna yake, lakini wao wanachukua wale watoto ili wapate thimpace. Lakini sisi wenyewe tukiwakuta basi tuendelee kuwaambia, kutoa maelezo na kufanya nao mazungumzo.

Mhe. Mwenyekiti, hili nafikiri linasababishwa na wale kina baba ambao wanakwepa kuwatunza watoto. Sifikiri kama mtu anatunza mtoto wake anapeleka huduma anavyotakiwa basi mwanamke hawezi kufanya hivyo. Kwa hivyo, tuendelee kuelimishana na tuwe na jamii ambayo inastaha, maana yake kuzurura usiku na mtoto sio jambo la staha.

Kuhusu mambo ya skuli ya chakula. Mheshimiwa keshayajibu na mambo ya michezo pia. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin aliuliza kwa nini taarifa haikuletwa siku ya 16 ile ile. Siku ya tarehe 16 Mhe. Muhyddin kama atakumbuka nafikiri na yeye alikuwa hapa kulikuwa kuna bajeti kuu ya serikali ilikuwa inachangiwa changiwa, ambayo yote ndio inatuwezesha kufanya haya mengine. Kwa hivyo, kwa vile hii ni taarifa tuliona tunaweza kuileta siku ile ile, lakini pia ile siku ya tarehe 16 pia maadhimisho yalifanywa na watoto wenyewe. Watoto wenyewe hao hapo, kama huamini basi geuka huko pembeni uwaulize. Kwa hivyo, maadhimisho walifanya lakini ripoti ndio imeletwa huku kwa sababu siku hiyo kulikuwa na hiyo shughuli ya kibajeti ambayo ndio inazaa haya yote ya utekelezaji pamoja na haya yote ambayo unaniuliza mimi basi hayawezi kufanyika kama bajeti hiyo haikuzungumzwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Muhyddin Moh'd aliuliza kuwa umefanyika utafiti gani. kama nilivyosema masuala ya utafiti ni gharama, utafiti huo mdogo wa kupata taarifa hizo tumeweza kukusanya ndio huo ambao tumeweza kuufanya. Misaada ndio kama hiyo ambayo tumeweza kuitoa kwa kipindi hicho.

Pia aliuliza kuwa Pemba hakuna walezi. Walezi na wazazi wapo kila mahala, naamini tutahakikisha kwamba hizi nafasi tunazigawanya kila mtu anaweza kuzipata. Kama kunatokea kitu basi Unguja wapate, Pemba wapate, Kiembesamaki wapate, Dimani wapate, Koani wapate na Shengejuu wapate.

Mhe. Rashid Seif Suleiman, suala lake nimeshalijibu na nimeshamueleza ni jinsi gani tunavyoshirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wewe mwenyewe umeona hapa, Waziri wa Elimu alikuwepo hapa, keshatoa maelezo yake kwa kina na yamefahamika. Sasa nyinyi kazi yenu mumgoje huko atakapokuwa mtarajiwa mkubwa amalize mengine.

Suala la matibabu kwa watoto kuanzia umri wa 0 mpaka 2 nafikiri linaweza likawezekana litategemea hali yenyewe. Serikali yetu inajitahidi kwa kiasi inachoweza ili kuhakikisha kwamba suala hili la matibabu hata kwa wanyonge wanapata tiba na wanaondolewa matatizo yao waliokuwa nayo.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la michezo na viwanja vya wazi. Kweli hilo ni tatizo, kwa hivyo tushirikiane na tuendelee kuhimizana ili tuweze kuwapatia hawa watoto wetu nafasi ya kucheza wasije wakapigwa na magari barabarani kama hivyo ulivyosema, kwa sababu sio jambo zuri. Viwanja vilivyokuwa wazi basi visijengwe. Suala hili ukija kuliuliza siku Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi atakapokuwepo kwa sababu yeye ndiye anayeshughulika na kugawa na kufanya vile anavyojua, maana mamlaka hayo

ni yake sio yangu mimi. Kwa hivyo, msisitize kwamba katika huo ugawaji wako basi ukumbuke viwanja vya watoto.

Kuhusu suala hili la vyeti nimeshalizungumzia na tutahakikisha kwamba wanapata na vile vilivyokuwepo wanakwenda kuvichukua. Halafu Mhe. Mohamed Ali Salim, kwa kukujibu haraka haraka kuhusu sasa hivi watoto walioanza mwanzo. Hili nafikiri atakuwa keshajibu mwenyewe Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Maalim Haroun Ali Suleiman, kuhusu masuala ya skuli hayako kwenye mamlaka yangu, lakini mimi ni mkusanyaji tu wa ripoti kuu. Kama kutakuwa na masuala ya ziada basi mtayapeleka siku hiyo.
Vile vile suala hili la maji kwa watoto wa Wambaa tuna mpango gani. Nalo hili litajibiwa siku hiyo, kwa sababu mamlaka ya maji hayako kwangu. Lakini hii ripoti ni kukupeni changamoto tu ya kuweza kuona mambo mbali mbali.

Mhe. Ali Abdalla Ali kuhsu kesi za kubaka. Tunajua kwamba kweli mpaka sasa hivi kulingana na hayo matendo na hizo hukumu zenyewe zinavyokuwa bado hali haijaridhisha sana. Ndio maana tunaamini kuwa hii sheria yetu tukiifanyia utaratibu ikija kutoka itaweza kuangalia haya mambo mengine na kuyashughulikia ipasavyo. Lakini masuala haya yanahitaji ushirikiano kwa pamoja na yanahitaji sheria hiyo ambayo itamlinda mtoto moja kwa moja.

Kwa hivyo, na mimi nakubali kuwa hakuna adhabu ya kutosha, nakubali pia utaratibu mzima wa kuendesha hizi shughuli za kubaka unakuwa mgumu. Haiwi kesi ya ng'ombe tu anaibiwa ni ng'ombe wako mwenyewe na unamjua na bado kesi hiyo ikachukua miaka miwili na huyo ni ng'ombe. Kwa hivyo, kidogo kuna matatizo katika uendeshaji wa hizi kesi, lakini wahusika tunakuwa tunazungumza nao na wanatuambia kuwa wataendelea kushughulikia. Mhe. Mwenyekiti, ni vizuri pia inapotokea tatizo na kasoro tuendelee kuambizana kwa kupitia vyombo hivi, basi kila mwenye sehemu yake airekebishe.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu misaada ya watoto kwa watu wenye watoto zaidi ya mmoja ambaye hakupata msaada. Nafikiri Idara ya Ustawi wa Jamii ingekuwa na jibu. Lakini nitapata taarifa baadae na nitatolea maelezo zaidi. Kwa kweli wako watu wanahitaji msaada, kwa sababu kuwa na watoto wawili na kipato chenyewe kikawa ni cha chini si jambo dogo. Kwa hivyo, sisi tunahusika na hilo na tunashauri kuwa jambo hilo lipatiwe ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Abass Juma Muhunzi, suala lake limeshajibiwa na la *tuition* limeshajibiwa na kuhusu sheria kuwa inakwenda kinyume na silka. Ni sheria ipi inayokwenda kinyume na silka, kama anazungumzia sheria ya mtoto, basi sheria ndio inaandaliwa na imejaribu kukusanya maoni ya watu wengi. Hata yeye kama anayo maoni basi bado kuna muda ataweza kutia maoni yake, lakini kazi kubwa imefanywa na wataalamu mbali mbali ndio kama hivyo Masheikh

wamekwenda na watu wameulizwa. Hata hivyo, sheria haiwezi kukamilika kwa mara moja ni lazima itapita katika njia mbali mbali, halafu mwisho ndio tunaona kuna kasoro hii, tunaipitisha tena. Kwa hivyo, tusiwe tunavunjana moyo, tupate hii sheria halafu angalau tuweze kuwadhibiti hawa wabakaji na hawa wakorofi wengine. Lakini tukianza kuvunjana moyo kitu hata bado itakuwa hatwendi mbele. Sasa kama mtu una maoni huwezi kuandika.

Kwa hivyo, mtu unatakiwa uandike maoni yako na upeleke kwenye mtandao, andika kwenye gazeti na andika sehemu yoyote usingoje hapa tu, ni lazima kuwe na mwanzo. Hatua moja ndio mwanzo wa safari, hivyo hii sheria ni muhimu tufanye utaratibu ili tuweze kuipitisha ili kuweza kufanya hayo mambo mengine. Tutakuwa hapa kila siku tunakuja kusema kabakwa, kakanyangwa, kakabwa na kafanywa nini basi tutakuwa hatwendi kokote. Kwa hivyo, watoto hatuwatendei haki. Tufanye tuwe na sheria ili tuwadhibiti hawa wakorofi wachache jamani.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Aziza Nabahan Suleiman ndio swali lako linaendana na hili kuwa kesi kweli zinakuwepo lakini nakubali kuwa hazijachukua mkondo mzuri kutokana na kwamba hata hiyo sheria yenyewe bado haijapita, hivyo wanakwenda tu wanafanya mambo yao wanakwenda zao, wanatambaa na kuwa wengi sasa. Kama ni maradhi ya kuambukiza basi yanaendea tu na sisi tunakuja hapa tunaanza kuulizana nini na nini. La msingi tujitahidi ili tuweze kuwabana kwa kupitia sheria zetu hizi tunazozipitisha hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu madawa ya kulevya. Suala hili ni tatizo kubwa sana na serikali inajua na inaendelea. Sasa hivi inaandaa sheria mpya ya madawa ya kulevya ambayo inafanyiwa mchakato sasa hivi. Lakini nakubali kwamba hilo ni tatizo na kwamba watoto wetu wanaendelea kuumia na sio kuumia tu, lakini wengi wanakufa. Sasa sisi hatuzai watoto ili wafe, tunazaa watoto ili waje kuendeleza *generation* iende mbele. Sasa kama haya madawa ya kulevya yanakuja kufanya mambo kama haya inakuwa matatizo juu ya matatizo, inakuwa sio lengo letu wala sio utaratibu tunaoutaka. Sisi tunataka hili tatizo liishe kabisa na serikali inajitahidi.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tuna idara nzima ambayo inashughulikia mambo haya. Juzi niliwahi kuwa kwenye kikao kimoja na nikaona jinsi wanavyofanyakazi ili kuharakisha hili suala, mpaka tulikuwa tunaona ni jinsi gani hivi karibuni, hata hicho chuo kinataka kujengwa huko Uwanja wa Ndege, ili kuweza kuwapata wale na kuwashughulikia. Kwa hivyo, serikali inajitahidi kweli kweli na ina mipango kabambe ya kuweza kufanya. Lakini hao watu wenye kutumia haya madawa ni watu ambao wana akili sana. Unajua wahalifu wakiwa wamekolea na pesa wanazo basi wanakuwa na mbinu nyingi. Kwa hivyo, serikali nayo

inajitahidi na inahitaji iwe na mbinu nyingi ya kifedha vile vile ili kuweza kukabiliana nao. Hata hivyo serikali inafanya juhudi kweli kweli.

Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban unakumbuka juzi tu tulikuwa tunajadili mambo haya. Sisi wote tunaguswa na tunaumia sana. Kwa sababu hawa watu sio tu kutuletea matatizo katika familia, unyonge, huzuni na kufiwa bali pia ni hasara wanapoumwa, wanaigharimu serikali gharama kubwa sana katika kuwatibu. Maana yake mtu ataumwa huwezi kumuacha, hata kama kala unga, lakini ni binadamu haki yake mojawapo ni hiyo ya kuuguzwa mpaka apone.

Mhe. Ame Ussi Juma suala lake la kuhusu uchunguzi uliofanywa kwamba huko mabomba bado hayajafanyika. Suala hili mimi siwezi kulijibu, lakini naamini kwamba Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi atakuwa na jibu hilo na wataharakisha kwa sababu mabomba kama yamekwishawekwa pale, kazi iliyobakia ni kufungwa tu basi itakuwa sio kazi kubwa sana. Hivyo itafanyika haraka sana ikamilike ili kuwaondolea wananchi shida ya maji.

Pia aliuliza kuna mpango gani wa kuwasaidia wazazi wasio na uwezo.
"Nyinyi mnaniuliza maswali hapa halafu mnazungumza ndio mtasikia majibu".

Pia aliuliza kuna mpango gani wa kuwasaidia wazazi wasio na uwezo. Mhe. Mwenyekiti, mipango hii siwezi kuisema hapa kwa sababu sielewi mpaka sasa hivi. Lakini kama likipendelezwa jambo lolote la kupendekezwa basi iko haja ya kuwasaidia zaidi ya hawa waliopata kusaidiwa hizo Shs.15,000/= lakini na wengine tunawasaidia kwa sababu serikali yetu inawasaidia wazee wasiojiweza na kuwasaidia wazazi pia wasiojiweza inawezekana.

Vile vile nitowe angalizo tu kwamba wawe ukweli hawajiwezi, wasifanye ujanja. Unakuwa na watoto halafu unakwepa dhamana zako kwa sababu ya kutaka msaada. Kila mtu ajuwe kwamba yeye madhali kalete kiumbe hapa duniani basi ni dhamana yake, ni wajibu wake na ni haki yake ahakikishe anamsomesha vizuri mtoto huyo, anamlisha vizuri, anamlaza vizuri na anamuhifadhi. Hilo ndio jukumu la kila mmoja wetu hapa. Tusije tukafikiria serikali kazi yake itakwenda kumchukua mtoto ikamkoshe, ikampandishe kitandani. Serikali hii itakuwa haifanyi kabisa.

Mhe. Faki Shaali Alhaj alisema watoto hawa wawili waliotiwa katika ajira mbaya walifariki Je, huyo mtu aliyefanyisha hivyo kachukuliwa hatua gani?

Sina hakika hatua aliyochukuliwa kwa sababu hapa mara nyingi huwa tunasema mtu akifa tena inakuwa ndio siku yake imefika, lakini kwa kweli kama sehemu nyengine mtu kama huyo awajibishwe kwanza ana makosa

mengi, hayo ya kumfanyisha mtoto kazi kosa, na kutokumtunza vizuri pia ndio kosa zaidi, kwa hivyo serikali kwa umoja wetu ndio tutakuwa tunarekebisha haya mambo ili watu waone kwamba mtu anapotenda kosa ukasababisha maisha ya mtu kupotea, basi wewe lazima ujibu. Kwa sababu nchi yetu tunakuwa kimya sana mtu anafanya jambo la kumharatarishia maisha au kumpotezea maisha yake halafu inakuwa kama hakuna kitu chochote, sasa haya mambo hayafai.

Huyu aliyenajisiwa kama mwanamke au mwanamme mimi kwanza hasa sipendi habari hizi kwa hivyo hata sijataka kujua, na ilivyokua hili jambo lenyewe baya sijataka kujua au mwanamke au mwanamme mimi nalilani moja kwa moja. Sasa sina uhakika huyu mtu ni wa jinsi gani lakini kwa kweli haya mambo hayapendezi hata kama unakwenda kusoma hupendi kuona mtu ananajisiwa vitu ambavyo anapenda mtu kuona kashinda (a) kapata nishani au katokea wa mwanzo kafanya vitu vya msingi vya sifa ndio tungependa kuvisoma katika jamii yetu kuliko haya mambo ambayo zamani nilikuwa siyasikii nilikuwa nasikia huko Nairobi lakini sasa hapa imekuwa balaa kama nyimbo sasa mambo gani haya tunakwenda wapi tutoke huko?

Anasema hizi asasi za kiraia wametolewa wamepata msaada gani na kuona kama hawarejei? Kwa kweli tulipata msaada mwingi kutoka kwa mradi wa GT 5 ambao unasaidia na kuweza kuwatoa hao watoto, habari za juu juu tu mpaka sasa hivi hawajarudia wanaendelea na masomo yao kama vile matarajio yetu. Kwa hivyo kwa kiasi fulani mradi huu umefanikisha kwa sababu umewarudisha skuli, umewakatia sare mabuku na vitabu na kama wengi wenu mtakuwa mnaangalia taarifa zetu za habari mara nyingi mtaweza kutuona, tunakwenda sehemu nyingi kutoa vitabu, mikoba, viatu na nguo pamoja na soksi ndio kazi zetu wizara yetu inafanya mambo kwa uhakika pamoja na kifungu kidogo tunachokuwa nacho nyote mnajua, lakini bado tunaweza kukamilisha mambo kama haya kwa niaba ya serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Najma Khalfan Juma yeye alizungumzia kuhusu *Jamhuri Garden* au Forodhani au mashamba kwa nini hakuna viwanja vya kuchezea watoto kama hivi vya kuburudishia? Nakubaliana nae na ndio nikasema tungojee mtarajiwa wetu atakayekuwepo kipindi hicho atakayeshika madaraka, basi sisi kama ni wazazi tutashawishi ili kuona haki ya mtoto inatekelezeka basi vitu hivi viweko hata kama havitakuwa vikubwa lakini viweko katika sehemu hiyo, ndio hali ngumu ya uchumi lakini katika sehemu nyingi ukienda ukikaa dirishani tulikaa mimi na Rahma tunaona vituo vya kuchezea watoto. Hatukumuona kule Zai anacheza, ni vitu vya kawaida tu kule watu wanajenga vipembea nyuma nyuma nyumba tano mpaka kumi hizi, kwa hivyo na sisi *inshaalla* tutafika huko hasa ikipatikana ile hazina yetu.

Mhe. Mwenyekiti hili la Mhe. Fatma Abdalla Tamim nimeshalijibu.

Mhe. Said Ali Mbarouk kuhusu tokeo la kupigwa watoto hili vile vile mimi kwa kuwa sio mwalimu nafikiri Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ameshalisema, lakini mambo ya kupigwa ndio tumeambiwa hayatakiwi tusipige watoto, vile vile *punishment* haitakiwi jambo ambalo kinadharia linakatazwa na kimataifa pia tunakatazwa, lakini tena akili zako alojionea Mhe. JK unaongeza na zako halafu tena uruke. *(Kicheko)*

Mhe.Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja alisema tufanye marekebisho hayo tumekubali, kuhusu mradi huo haujakamilika yeye ndio yuke kule sisi tulifikiri umemalizika na umevurugwa basi hilo ni tatizo jengine, sisi tunakubali kwamba yeye ameona na atahakikisha atasimamia utakamilika huo mradi kwa sababu hilo ndio jukumu lake yeye ndio Mkoa wake anatakiwa asimamie maendeleo ya Mkoa ule.

Kasema kuna kesi ya kulawitiwa sasa suluhu ya kifamilia inaruhusiwa nasema haitoshi ndio maana tukasema tuhakikishe hii sheria tunaitoa haraka sana ili iweze kudhibiti mambo yote kama haya, unapofanya kaso kuwe kuna adhabu fulani. Mfano kama umenitukana mimi basi adhabu yako kama nakupa mimi nitakupiga ngumi kama ninatoa mimi adhabu. Sasa kule kutakuwa kumepangwa adhabu gani kwa kosa hili la kulawiti? Hili la kumbusu kutakuwa na adhabu maalum. Kwa hivyo tukipitisha kule haya masuala yatakuwa yamekwisha kwa sababu mtu atajua nikifanya hivi adhabu yangu hii. Lakini kuwa na suluhu ni mambo ya kienyeji, hayo suluhu nini mtu kafanya kosa aadhibiwe kwa mujibu wa kosa. Suluhu , suluhu ndio nini hapa sasa hivi tena haifai!

Kwa hivyo hili la watoto walioolewa kama yeye nimpongeze kwa kuchukua hatua, lakini kama sisi Wizara mara nyengine hatupati hizi taarifa mpaka tuletewe kwa hivyo hatuwezi kujua kwamba mtoto wa miaka kumi huku anaolewa au miaka kumi na mbili huku anaolewa. Sisi itakuwa vigumu kama hizi taarifa hakutoka mtu akatuletea lakini nyinyi mliokuweko kule mtuletee zile taarifa tushirikiane ili tuwakabili hawa. Kwa sababu upo umri uliowekwa wa kuolewa mtu sio mtu kwa sababu mkubwa mkubwa kama mie ndio uje unioe hata kama nina miaka kumi itakuwa kosa.

Mhe. Hamad Masoud Hamad yeye aliuliza watoto wangapi tunao Unguja na Pemba? Mimi hesabu hiyo sinayo lakini nafikiri ni jambo muhimu pia, lakini hatukuweza kuhesabu kwa sababu ule uhalifu na uharamia wa hali ya juu Mungu atupishie mbali haujafika na Mungu autokomeze huko huko, kwa hivyo hatukuwa na hesabu ya kuwahesabu wangapi kwa wangapi kwa sababu hakuna

jambo baya lililotokezea kama jua linawaunguza tunawapa kofia, na mwengine yupo kwenye Baraza ni Kiongozi tumempa kwa sababu ya kutambua kwamba watu wote ni haki sawa, sisi Wizara tunae jana walichaguana wenyewe yuko katika baraza la vijana yuko kijana moja Albino.

Hili suala la ada nafikiri mwenyewe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ameshalitolea majibu.
Hili la ajira haikuonesha *break down* lakini ni hiyo ambayo tumeitoa ambayo tumepata msaada kutoka kwa GT 5.

Mhe. Ali Denge Makame yeye alisema serikali inajiandaa vipi na kuhifadhi hao vijana wanaotumia madawa ya kulevya? Jitihada kwa kushirikiana na NGO's nyingi ikiwemo ZAYADESA na nyengine wameweza kuandaa vituo, kwa mfano kipo kituo kinaitwa SOBA HOUSE Miembeni huko cha kuweza kuwasaidia watu kutoka katika hali waliyokuwa nayo na Rahaleo na kwa Mchina vipo vituo hivyo, kwa hivyo kazi hizi zinafanyika kwa ushirikiano wa ZAYADESA, ZAIYADA na ziko NGO's nyengine lakini na sisi wazazi na walezi pia tunashirikiana na kupambana na hali ngumu ya watu wetu wanaotumia madawa ya kulevya.

Sasa hii habari ya chanjo nafikiri itasubiri kwa sababu sina jibu lake mpaka siku ya bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Kuhusu wapara samaki wamepungua kwa kiasi gani? Wapara samaki ambao sisi tulikuwa tumewafanya kama *target* hofu yetu ni hawa wa Mkokotoni na Micheweni ni kwamba wale tuliowapeleka skuli mpaka sasa hivi tumefuatilia inaonekana wanaendelea hatujapata taarifa ya kwamba kuna waliotoroka wakarudi tena kwenye kupara samaki. Kama nilivyogusia kwamba shughuli hizi zote zinahitaji fedha nyingi za ufuatiliaji na nyinyi wenyewe nyote mashahidi wa ufinyu wa bajeti yatu, kwa hivyo tuendelee kushirikiana ili kuyatatua matatizo mengine ambayo yako kwenye uwezo wetu na tuendelee kuelekezana na penye mapungufu milango ya Wizara yetu iko wazi serikali yetu inakaribisha maoni na mashauri na tutaendelea ili kuhakikisha watoto wetu wanapata haki zao zote zile ambazo tumezikubali na zile ambazo ni wajibu wetu na majukumu yetu.

Nawashukuru sana Waheshimiwa na nawatakieni kila la kheri na mimi pia munitakie kila la kheri katika shughuli zangu maana msije mkashangaa mkasema na mimi nataka kuwa kiongozi wa nchi hii kwa tiketi ya Urais *(Makofi)* Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wanaoafiki wanyanyue mikono na wasioafiki, walioafiki wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja ilaimuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Rashid Seif Suleiman. Mhe. Mwenyekiti taarifa ni kwamba kanuni zimebadilishwa na Mhe. Mwenyekiti una uwezo moja kwa moja wa kuahirisha kikao.

Mhe. Mwenyekiti: Nakumbuka hilo lakini kwa hili nampa nafasi Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora: Hata mimi nilikuwa nataka nikukumbushe vile vile kwamba kanuni imekupa uwezo vile vile moja kwa moja kama shughuli zetu za leo tulizozipanga zimekwisha basi moja kwa moja uwe unaahirisha.

Lakini hata hivyo kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kutoa hoja kwamba kwa kuwa shughuli zetu za leo zimekwisha basi Baraza uliahirishe kabla ya wakati wake hadi kesho saa 3.00 Asubuhi.

(Saa 1.45 Usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 22/06/2010
Saa 3.00 asubuhi)